ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
56.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Ishirini – Tarehe 12 Julai, 2012

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, (Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 87

Upatikanaji wa Vitambulisho vya Ukaazi

Mhe. Kazija Khamis Kona - Aliuliza

Kwa kuwa vitambulisho vya Mzanzibari ni muhimu na ni haki kwa Wazanzibari kuwa navyo, na kwa kuwa baadhi ya Wazanzibari wengi wameikosa haki yao hiyo kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo za kuwepo kwa masharti na taratibu ngumu zilizowekwa ili kuipata haki hiyo.

Jee, Mhe. Waziri, wizara yako haioni kuwa kuna haja hivi sasa ya kuwapunguzia vikwazo hivyo vigumu Wazanzibari hao ili waweze kupata haki hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 87 kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Usajili ya Kadi za Utambulisho Zanzibar inasajili na kutoa vitambulisho kwa Wazanzibari waliotimiza masharti kwa mujibu wa sheria Na. 7 mwaka 2005, ambayo ilipitishwa hapa Barazani pamoja na Kanuni iliyotungwa chini ya kifungu nambari 16 cha sheria hiyo.

Masharti yaliopo katika usajili huo ni kama hivi ifuatavyo.

a) Awe Mtanzania anayeishi Zanzibar
b) Awe na umri wa miaka 18 au zaidi
c) Afike mwenyewe kwa Sheha wa Shehia anayoishi na kupatiwa barua ya uthibitisho kama anaishi katika Shehia hiyo.
d) Awe na cheti za kuzaliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa watu waliozaliwa chini ya mwaka 1964, afisi imetoa muongozo wa kwamba hawana vyeti vya kuzaliwa wanaweza kusajiliwa kwa kutumia hati ya kiapo kutoka mahakamani kwa uthibitisho wa kuzaliwa kwao.

Hizo ndizo taratibu zilizopitishwa kisheria kwa sasa nchini mwetu.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Waziri kwa kuwa vitambulisho vya Mzanzibari ni muhimu kwa Wazanzibari wote na keshokutwa tunatakiwa vitambulisho vya Mtanzania, jee Mhe. Waziri kwa kuwa Wazanzibari wengi bado vitambulisho vya Uzanzibari, jee watahitajika kupewa vitambulisho vya Mtanzania.

Pili kusema kweli Mhe. Waziri yaliyoekwa ni magumu kwa wananchi wetu hasa wa vijijini kufuatilia. Jee, Mhe. Waziri ni lini wizara yako itafanya marekebisho ituletee hiyo sheria hapa Baraza ili tuifanyie marekebisho wananchi wetu waondokane na kadhia hiyo.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kuna baadhi ya wananchi wetu tayari wameshakamilisha utaratibu ambao ulioutaja. Mfano kama watu wazima waliotimiza miaka 60 na kuendelea tayari wameshakwenda kwa Sheha, wameshakula viapo na bado hawajapatiwa vitambulisho hivyo.

Ni sababu gani za msingi zilizopelekea wananchi hao wasipewe vitambulisho hivyo na ushahidi upo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kwanza naomba kumjuulisha Mhe. Mwakilishi kwamba vitambulisho vya Zanzibar ni tofauti kabisa na vitambulisho hivyo vitakavyokuja vya Mtanzania. Yeye kishasema wazi wazi kwamba hivyo vinaitwa Mtanzania, hivi ni vya Mzanzibari. Kwa hivyo kuna tofauti kubwa kabisa.

Naomba baadae nikumbushe ni kupatia sera ya vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi na wale Wajumbe ambao pia hawana tutawapa hii sera ili waone yale yaliyoazimiwa hasa maana yake nini. Lakini kwa kifupi tu, nisome nini Mzanzibari kwa mujibu wa sheria Na. 5 ya mwaka 1995:-

1. Mzanzibari kwa asili. Yeye amekuwa akiishi Zanzibar kabla na hadi tarehe 12 Januari, 1964.

2. Amezaliwa Zanzibar na walau mmoja wazazi wake ni Mzanzibari
3. Amekuwa ni Mzanzibari kabla ya tarehe 26 Aprili, 1964 na ambaye hajapoteza uraia wa Tanzania.

Halafu kuna Mzanzibari wa kujiandikisha. Sasa ninataka kusisitiza kwamba Mzanzibari Mkaazi ni mtu mwenye sifa ya Uzanzibari kama ilivyofafanuliwa katika sheria Na. 5 ya mwaka 1985, na pia awe ametimiza sharti la kuwa makaazi yake ya kudumu Zanzibar.

Sasa hapo ndipo penye matatizo, wengine huwa hawatimizi yale masharti. Lakini wale ambao umesema wanatimiza masharti basi hakuna tatizo kama wapo hao, mimi naomba nikabidhi hiyo orodha tutaifanyia kazi wapate haki yao.

Sasa ninasema kwamba kuwa Mzanzibari pana *trick* hapa kidogo. Si kila Mtanzania ni Mzanzibari, lakini kuupata utambulisho wa Mzanzibari lazima uwe Mtanzania, hiyo ni mojawapo ya hati, sio kinyumenyume kwamba lazima mtu yeyote apate utambulisho wa Mzanzibari basi lazima awe Mtanzania, lakini sio kila Mtanzania anayo haki ya kupata Uzanzibari, ni lazima uwe na sifa zile ambazo nimezitaja.

Marekebisho Mhe. Mwenyekiti, mimi na sisi kwa upande wetu wa serikali tunavyoona kwa sasa hizi sifa zimekidhi, sasa kama unahisi kuna mapungufu tunakaribisha fikra, mawazo ili tuirekebishe sheria hii halafu tuilete hapa tuone.

Tatizo liliopo ni kwenye utekekelezaji na hiyo sisi kwenye serikali tumesharekebisha, tushawaelekeza Masheha taratibu za kufuata kila mmoja wetu au kila mmoja aliyekuwa na sifa apate haki ile ya Uzanzibari.

Tatizo linakuja hapo sifa wengine wanakuwa hawatimizi. Hao uliosema wanatimiza tunawakaribisha na taratibu zipo za kufuata. Mimi ninakuomba Mheshimiwa nikabidhi hiyo orodha ambao wanastahiki wamekamilisha tutaifanyia kazi.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kuna fununu kwamba vitambulisho vingi vya Mzanzibari havijachukuliwa na wenyewe. Sasa ninataka kujua ni sababu gani za msingi zinazopelekea vitambulisho hivyo vikawa havichukuliwi.

Pili jee wizara yako ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa vitambulisho hivyo vitachukuliwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Ni kweli kwamba kuna orodha kubwa ya Wazanzibari ambao vitambulisho vyao vipo katika Afisi za Wilaya havijachukuliwa, na wakati nikifanya majumuisho ya hotuba yangu ya bajeti nilitoa orodha kamili.

Sababu kwa kweli sizijui siwezi kusema sababu gani za kwa nini hawa hawajaenda kuvichukua. Lakini nina wasi wasi tu labda pengine hawa hawapo nchini, wamejiandikisha wakaondoka au labda walijiandikisha sehemu moja, sasa wamejiandikisha sehemu nyengine, na ile *system* akenda kuchukua pengine ana wasi wasi labda itawakamata.

Sasa sababu za msingi sijui, lakini wizara yangu kwa kweli inashajihisha wananchi hawa kupitia afisi zetu za Wilaya kwa Masheha katika Shehia zao kuwasaidia kuwapelekea orodha katika sehemu zao zote, kwa sababu tunataka vitambulisho lazima wakavichukue afisini pale pale. Sasa kwa wale hawajavichukua tunawashajihisha kwa orodha kupelekwa katika Wilaya zao kuonesha kwamba jamani katika Shehia vitambulisho hamjachukua watu hawa. Kwa hivyo munaombwa mukavichukue. Hiyo tunajitahidi sana kuwashajihisha.

Mhe. Abdalla Mohamed Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, katika majibu ya suali hili ni kwamba moja katika masharti ya kupata huu ukaazi au kitambulisho cha ukaazi ni kwamba uwe na cheti cha kuzaliwa.

Sasa jee katika hiki cheti cha kuzaliwa. Kinachozingatiwa pale kwamba athibitike kuwa umri umefikia au ithibitike kwamba yeye ni mzawa wa kisiwa hiki. Kwani ikiwa ni umri wengi wanaonyimwa wanakuwa wameshapitia dalili za umri zinaonekana, kama sisi wengine tuliokuwa na mvi tunaonekana tayari miaka 18 tumeshapita, na kama ni uzawa watu wengi waliopo hapa wanapatiwa huduma kama zile za skuli, hospitali. Sasa kama ni hivyo kwa nini mpaka leo iwe hiki ni kipengele kikubwa cha kuwakosesha watu wakaazi wetu haki yao ya msingi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, hili limefanywa kwa makusudi ili kuwatambua hawa watu wanaotakiwa kupata hiyo kadi ya Mzanzibari. Maana yake tunaona tutumie njia gani, hakuna njia nyengine, ndio hapa tumepata malalamiko wanapewa Wamasai, watu wa Msumbiji na watu wengine.

Sasa uthibitisho moja wapo kwamba huyu kazaliwa Zanzibar, wazee wake wanatoka Zanzibar kama taratibu na kama nilivyosoma pale. Sasa tunaona uthibitisho tunaona ni huu tu hakuna mwengine. Kama huu hautimizi labda umezaliwa kabla ya mapinduzi, ndio tunasema ukale kiapo, ukisha kula kiapo basi kwa umri wake inathibitisha na ku-*qualify* ukale kiapo na kile kiapo kinathibitisha wewe tena utapewa kitambulisho chako.

Sasa tatizo kwamba kuna watu hawataki yote mawili haya, hapo ndipo panapotokezea matatizo. Lakini pia kuna malalamiko kwamba kama alivyosema Mheshimiwa aliyetangulia kwenye swali lake, kuwa kuna wengine wana sifa zote lakini hawapewi. Ndio ninasema kama wapo hawa basi sisi upande wetu wa wizara au Afisi ya Vitambulisho tupo tayari kufanya kazi na watu hawa kuhakikisha wanapata haki yao ili hizi haki za msingi za kwenda skuli, benki wasinyimwe.

Tupo tayari wizara kuhakikisha kwamba haya yanafanikiwa. Tunakubali matatizo madogo madogo yapo, lakini tunahisi kwa utaratibu kwa sasa hakuna *substitute* utaratibu huu. Lakini pia tunakaribisha mawazo, kama unahisi turekebishe vipi basi serikali ipo tayari kupokea mawazo tuone jinsi ya kurekebisha.

Na. 61

Huduma za Bima ya Afya Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibiwa swali langu Na. 61 naomba uniruhusu kusema machache.

Kwanza ninataka nimpongeze Waziri wa Afya kwa kutekeleza ahadi zake jana hiyo hiyo usiku baada ya kupitisha bajeti na kuanza kuondoa kero hizo. Nimpongeze kwa uungwana alioufanya usiku huo huo jana, huyu ndiye Waziri anayestahili sifa.

Baada ya maelezo hayo naomba suali langu Na. 61 lijibiwe.

Mfuko wa Taifa ya Bima ya Afya (NHIF) Tanzania tangu kuanzishwa kwake umewanufaisha watu wa Zanzibar 28,048. Kitendo ambacho kimepunguza mzigo kwa Serikali katika kuwapatia huduma za matibabu bure wananchi wake.

a) Ni sababu gani zilipelekea Wizara ya Afya Zanzibar kutoruhusu hadi sasa wanachama wa mfuko huo kutibiwa katika hospitali za serikali zikiwemo za Wete, Chake-Chake, Abdalla Mzee, Makunduchi na Kivunge na kuacha mamilioni ya fedha yanayolipwa kila mwezi mfuko huo kunufaisha hospitali za watu binafsi Zanzibar.
b) Sababu gani zimepelekea serikali kukalia maombi ya mfuko huo ya kutaka kutumia hospitali hizo na kusababisha usumbufu kwa wagonjwa kufuata huduma mbali na maeneo wanayoishi wakiwemo mama wajawazito.
c) Kuna taarifa kwamba Serikali ya SMZ ina mpango wa kuanzisha mfuko wa Bima ya Zanzibar. Kauli hiyo ina ukweli wa kiasi gani, na kama ni kweli ni lini mfuko huo utaanzishwa rasmi Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na. 61 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi ninapenda kutoa maelezo mafupi juu ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Tanzania. Mfuko huu umeanza kufanya kazi zake hapa Zanzibar kuanzia mwaka 2007, na una jumla ya wanachama 5,393, ukichanganya pamoja na familia zao idadi inafikia 28,044 wanaofaidika na mfuko huu.

Wanachama wa mfuko huu kwa upande wa Zanzibar ni wafanyakazi wa taasisi zilizo chini ya Serikali ya Muungano ambao wanaingia kwa mujibu wa sheria za kuanzishwa kwa mfuko huu pamoja na taasisi za binafsi.

Ili kuwapa huduma wateja wa mfuko huu, NHIF iliwapa mafunzo wafanyakazi wa afya Zanzibar juu ya kuendesha mfuko huo kwa hospitali zote za serikali, binafsi na NGO’s Unguja na Pemba.

Wanachama wa mfuko huu wanapata huduma katika hospitali za Mnazi Mmoja, Hospitali ya Jeshi Bububu, Dispensary ya Polisi, Al-Rahma, Kituo cha Afya-Nia kupitia Kanisa la SBA na duka la dawa la Sanas.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ninapenda kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake yenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo.

Wizara ya Afya haijaweka pingamizi zozote kwa wananchi wa mfuko huu kutibiwa katika hospitali ziliopo nchini chini ya Wizara ya Afya. Suala la kuchagua wapi wateja wao watibiwe ni NHIF wenyewe.

Utekelezaji wa kutoa huduma za mfuko huo kwa kuanzia, walianza kwa awamu. Kwanza Unguja na mambo yakishakukaa sawa yatekelezwe kwa upande wa Pemba. Lakini kwa sababu ya matatizo ya kiutawala hata Unguja utekelezaji wake ulikuwa na matatizo kutokana na mfuko kutokuwa na ofisi, wafanyakazi pamoja na vitendea kazi ambapo vingesaidia ufuatiliaji na uhamasishaji wa wanachama kujiunga na mfuko Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ninapenda kumjuulisha Mhe. Mwakilishi kwamba kikwazo kwa sasa hakipo, kwani mfuko umeshafungua afisi yake hapa Zanzibar na kuajiri watendaji wa fani mbalimbali, akiwemo daktari, mhasibu na dereva.

Ni matumaini yangu kwamba mfuko utaendelea na juhudi hizo ili hospitali zetu za serikali za Unguja na Pemba ziweze kunufaika na mfuko huo, pia kuwapunguzia wananchi usumbufu wa kuzifuata huduma hizo mbali na sehemu wanazoishi.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa za kuanzishwa kwa mfuko wa Bima Zanzibar ni za kweli na mchakato wa kuanzishwa kwa mfuko huo upo katika hatua za awali. Utafiti wa awali kujua utayari na uwezo wa wananchi umeshaanza na mara tu baada ya kupata matokeo yake timu ya kitaalamu itapendekeza aina ya mfuko utakaokuwa muafaka kwa mazingira ya Zanzibar.

Dhamana ya uanzishwaji wa Bima ya Zanzibar itasimamiwa na Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa amekiri mfuko huu haujaruhusiwa hadi kutumika katika hospitali za serikali Pemba, serikali haioni ni kuendelea kupoteza mapato, na lini mfuko huo utaruhusiwa ili wananchi wa Pemba waweze kunufaika na matibabu hayo.

Pili, kwa kuwa mfuko huo umeanza kutoa huduma muda mrefu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, jee, anaweza kutwambia imenufaika kiasi gani hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na hospitali za *private.*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Bima wa Taifa ni wa Tanzania au niseme ni wa Serikali ya Muungano haupo katika Serikali yetu. Kwa hivyo maamuzi yao vipi itakavyokuwa yapo katika mamlaka yao. Sisi ni watoa huduma tu.

Nimesema katika utangulizi kwamba mambo yalikuwa hayakukaa sawa, lakini sasa hivi yameshakaa sawa. Ni matumaini yangu kwamba kwa kipindi kitakachokuwa si kirefu watafungua tawi Pemba, na wananchi walioko kule nao watafaidika. Lakini siwezi kusema lini kwa sababu hilo halipo katika mamlaka yetu.

Katika Hospitali ya Mnazi Mmoja taarifa nitamtafutia nitamletea, lakini za *private* hizo itabidi zitafutwe kwenye hospitali za *private*, na kwa kweli sijui ni hospitali zipi *private* lakini tutafuta taarifa baadae tutawatumia, kwa sababu afisi hiyo ya Bima ipo hapa Zanzibar tutalifuatilia hilo na tutaleta jawabu.

Na. 146

Ukarabati wa Barabara ya Donge

Mhe. Panya Ali Abdalla – Aliuliza

Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Donge inayotokea Mtambile kuelekea Muanda ni barabara iliyojengwa zamani na hadi sasa ipo katika hali mbaya. Katika kipindi cha awamu ya sita barabara hiyo iliwahi kutiwa kifusi kwa lengo la kuifanyia ukarabati ila ujenzi huo haukuendelea tena.

Hata hivyo, Mhe. Rais wa awamu ya sita katika ziara zake alipotembelea Donge alitoa ahadi ya kuifanyia matengenezo barabara hiyo, lakini hadi sasa barabara hiyo haijatengenezwa na kuifanya izidi kuharibika na hata kuwapatia usumbufu wananchi wanaoitumia barabara hiyo.

a) Jee Mhe. Waziri huoni kwamba kutotekelezwa kwa ahadi ya Mhe. Rais Mstaafu ni kuwapatia usumbufu wananchi wetu.
b) Jee, ni lini barabara hiyo itajengwa ili wananchi wa Donge nao wanufaike na maendeleo yanayofikiwa na Serikali ya awamu ya saba.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na. 146 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Donge/Mtambile hadi Donge/Muanda ni miongoni mwa barabara muhimu kwa wananchi wa maeneo hayo kwa usafirishaji wa mazao kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine.

Barabara hiyo yenye urefu wa zaidi ya kilomita mbili kama alivyosema Mhe. Mwakilishi wizara yangu kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara ilitia kifusi ili iweze kupitika wakati wowote, serikali ikiwa inaendelea kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo. Hata hivyo, barabara hiyo imeharibika kutokana na mvua za masika msimu uliopita.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imekuwa ikitenga fedha kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo mbali mbali barabara nyingi nchini katika maeneo tofauti kwa kiwango cha kifusi hasa zile sehemu korofi ili ziweze kupitika na kuondoa usumbufu kwa wananchi.

Katika mwaka wa fedha 2012/13, wizara yangu imetenga shilingi milioni ishirini na tano na laki tano kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo sehemu korofi kwenye barabara hiyo.

Baada ya maelezo hayo sasa ninapenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.

a) Mhe. Mwenyekiti, serikali inatambua ahadi ya Mhe. Rais Mstaafu awamu ya sita kama nilivyoeleza kwenye utangulizi kwamba serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara hiyo.
b) Barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami mara tu serikali itakapopata fedha na ujenzi utakaporuhusiwa. Hata hivyo, wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini B itaendelea kuifanyia matengenezo barabara hiyo ili iweze kupitika na kuondoa usumbufu kwa wananchi.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini pia naomba nimuulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa ni muda mrefu umepita bila ya ahadi ya Mhe. Rais ya awamu ya sita haijatekelezwa au haijatimizwa. Jee ni lini hasa serikali itatimiza ahadi hiyo.

Na kwa kuwa kutimizwa kwa ahadi hizo kutawaondoshea usumbufu wananchi wa Donge na wenye kutumia barabara hiyo. Jee serikali inawaambia nini juu ya ujenzi wa barabara hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Ahadi ya Mhe. Rais Mstaafu ni kuona kwamba barabara ile inajengwa kwa kiwango cha lami. Ahadi hiyo tumeipokea na tunaendelea kuifanyia kazi kwa kutafuta fedha hizo. Lakini kwa kutambua kwamba wananchi wetu wanapata taabu hasa shughuli za usafirishaji wa mazao, wizara yangu katika bajeti inayokuja imetenga fedha.

Matumaini yetu kwamba fedha hizi tukizitumia vizuri zinaweza zikapunguza changamoto ya usumbufu wa barabara na kuweza kutumika vizuri, ili kuondosha huo usumbufu wanaoupata wananchi wetu katika shughuli zao za usafirishaji wa mazao.

Hivyo basi naomba tu wananchi wa Donge na ninaamini Mwakilishi wao anasikia vizuri na serikali inawathamini wananchi wao kwa msingi kwamba serikali ina dhamira ya dhati ya kutaka kujenga barabara hiyo. Lakini katika kipindi hiki tutajenga kwa kiwango cha kifusi ili kuondoa usumbufu wakati utaratibu wa kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya lami tukiwa tunaendelea nao serikalini.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Pamoja na majibu mazuri sana aliyotoa Mhe. Naibu naomba kuuliza swali dogo kama ifuatavyo.

Kwa kuwa juzi tu hapa tulipitisha sheria ya kuwaenzi viongozi wetu wastaafu, na kwa kuwa Rais wetu Mstaafu kishaeka ahadi, sio tu ya kujenga barabara ile ya Donge lakini hata ujenzi wa Skuli ya Vikunguni iliopo katika Jimbo la Wawi, na kwa kuwa ahadi hizi kila siku serikali munaendelea kuzichelewesha.

Jee, kuendelea kuzichelewa ahadi hizi si itakuwa kuwadhalilisha viongozi wetu wastaafu badala ya kuwaenzi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwakilisi swali la msingi lilikuwa linahusu Donge.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Donge Mhe. Rais Mstaafu ameiwekea ahadi na haijatekelezwa, na kwa kuwa juzi tulipitisha sheria ndani ya Baraza hili kuwaenzi viongozi wetu wastaafu.

Sasa kutoendelea kuwatekelezea ahadi zao ikiwa ni pamoja na kutojenga barabara ya Donge si kuwadhalilisha viongozi hawa jamani.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri kama unayo majibu mjibu lakini si kwa ulazima.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi mwana mapinduzi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli tumepitisha sheria za kuwaenzi viongozi na imani yangu kwamba Serikali itaendelea kuheshimu ahadi na kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na viongozi.

Ninapenda tena kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba ahadi ile ya Mhe. Rais wa awamu ya sita kwa barabara ile ya Vikunguni, wizarani kwetu tumeipokea na tunaifanyia kazi, na nina hakika Mhe. Mwakilishi unatambua na kuthamini hatua tuliopo katika kufanikisha ahadi ile.

Mategemeo yangu kwamba Mhe. Mwakilishi uulizaji wako hapa ulikuwa ni kutia chaa tu kuona jambo lile linakamilika kwa haraka. Ninapenda kukuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba ahadi hiyo tutaitekeleza kama tulivyoanza kutekeleza.

Na. 147

Ukarabati wa Barabara ya Jozani

Mhe. Panya Ali Abdalla – Aliuliza**:-**

Sote tunaelewa kwamba barabara zetu nyingi huharibika kutokana na kutumika kwa muda mrefu, na hali ya hewa hasa nyakati za mvua za masika na kadhalika. Imekuwa kama ni kawaida sasa kwa barabara nyingi hasa ziliopo vijijini kuwekwa kifusi ili kuzifanya ziweze kupitika.

Barabara ya Jozani kuelekea Ukongoroni, na ile ya kuelekea Charawe ni kati ya barabara iliyokuwa katika hali mbaya na baadae kuwekwa kifusi ili iweze kutumika kwa urahisi. Ni muda mrefu sasa tangu kulivyowekwa kifusi hicho na barabara hiyo imeshaanza kuharibika tena.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kwamba kuchelewa kwa muda mrefu kuzijenga barabara hizi ambazo zimeshawekwa kifusi ni kupoteza fedha za Serikali.

(b) Je, Mhe. Waziri ni lini barabara hizi zitajengwa kwa kiwango cha lami ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata usafiri wa uhakika kwa wakati wote.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 147 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Jozani – Ukongoroni na ile ya Charawe ni miongoni mwa barabara 6 zitakazofanyiwa upembuzi yakinifu na sadifu kwa ajili ya kuzijenga kwa kiwango cha lami. Mradi huo umefadhiliwa na benki ya Maendeleo Afrika (ADB) ambapo jumla ya Tshs. 12 bilioni zimetengwa kwa kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, ADB imeshairuhusu Wizara yangu kuendelea na mchakato wa tathmini wa kumtafuta Mhandisi Mshauri atakayezifanya kazi hizo baada ya kuwasilisha maombi hayo kwao. Serikali inaendelea na mazungumzo na ADB ya kupata fedha za ujenzi ambao unajumuisha barabara zifuatazo:-

- Barabara ya Matemwe (Kiashange) – Muyuni (6.5km)
- Barabara ya Njia nne – Umbuji – Uroa (11km)
- Mkwajuni – Kijini (5.5km)
- Kichwele – Pangeni (4km)
- Jozani – Ukongoroni – Charawe (15km)
- Fuoni – Kombeni (6.7km)

Kujengwa kwa barabara hizo kutawawezesha wananchi wa maeneo hayo kuwa na usafiri wa uhakika kwa msimu wote wa mwaka, na hivyo kuwaongezea vipato vyao na uimarishaji wa huduma za usafiri kwa wananchi hao.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake lakini nimuulize swali moja dogo la nyongeza.

Mimi nilitaka kujua tu jee ndani ya bajeti yake hii ambayo tumeielekea barabara hizi zitaweza kujengwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika jibu mama tumeeleza kwamba kwenye bajeti hii tumetenga shilingi bilioni mbili kwa kuendeleza usanifu, yaani *feasibility study and design*. Baada ya kukamilisha utaratibu huo tutaendelea kufanya na wenzetu wa ADB kwa ajili ya kutafuta fedha za kujenga mradi huo. Hivyo baada ya kukamilika utaratibu huo wa *study* ndipo itakapokuja hatua ya pili ya kujenga. Kwa hivyo katika bajeti hii ni jukumu letu sisi ni kufanya *study* na baada ya kukamilisha *study* tutawapelekea wenzetu wa ADB ili kuweza kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo sita.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Naomba nimuulize kwamba ujengaji wa barabara zenye kiwango cha lami unazingatia vigezo gani katika barabara hizo. Ni maeneo yepi ambayo yanapewa kipaumbele katika uwekaji wa kiwango cha lami.

Lakini swali la pili ujengaji huu wa barabara yenye kiwango cha lami unazingatia mtawanyo wa Kiwilaya ili Wilaya moja isiwe na barabara nyingi zenye lami lakini Wilaya nyengine ikawa hazipitiki.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, vigezo vya kujenga barabara kwa kiwango cha lami sote tunavijua. Dhamira ya serikali ni kuona kwamba wananchi wake wote wanapata huduma safi na nzuri ikiwemo suala la barabara ya lami.

Lakini kumekuwa na maeneo ambayo yanakuwa na *economic zone* yanapewa kipaumbele kwa serikali yetu. Sasa maeneo tuliyoyataja ni miradi ambayo imechukua muda mrefu katika kupata ufadhili, na kuona kwamba ina *mature*

miradi hii, kama vile tulivyoanza kuomba miradi ya MSP, miradi ya NORAD iliyojengwa kule Kusini Pemba na miradi iliyojengwa Kaskazini Pemba.

Miradi hii nayo imo katika utaratibu huo huo wa kuona kwamba ule mgawano wa keki ya taifa unakwenda katika kila eneo. Ukiangalia katika barabara hizi sita, zipo ambazo katika Wilaya ya Kati, Kaskazini B, Wilaya ya Kaskazini A.

Sasa namna ya kugawa barabara hizi kwa yale maeneo husika, kuna yale maeneo ambayo ukiangalia humu kuna maeneo kwenye mawe, yapo maeneo yanaekezwa katika maeneo ya wawekezaji, kwa maana kwamba kama upande wa Matemwe ili kuvutia wawekezaji ambayo ni hiyo *economic zone.*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ugawaji huu wa barabara hizi ingawa haupo moja kwa moja katika Wilaya, lakini katika kutimiza azma ya serikali ya kuona kwamba kila mwananchi wa nchi hii naye ananufaika katika upatikanaji wa huduma bora ikiwemo suala la ya lami.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wa Ukongoroni Charawe wameathirika kiuchumi na wanaendelea kuathirika kiuchumi, vile vile wanafarajika kupata mwakilishi mpya na ambaye ni Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

(a) Je, ni lini watanufaika wananchi hao kwa kupitia matunda yako.
(b) Umetumia kipaumbele gani kujenga barabara za Makunduchi, Kiwengwa na kuiwacha barabara hii ya Ukongoroni Charawe.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, samahani swali lake la pili sikumfahamu. Ni barabara ipi hiyo ya Makunduchi ile ya lami au zile nyengine.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ni ile ya lami, na kuiwacha hii ya Ukongoroni Charawe, umetumia kipaumbele gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze na hilo la pili. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi ni mwenyeji wa Kusini, hivyo anatambua fika kwamba Makunduchi ndio makao makuu ya wilaya. Ni imani yangu kwamba tungekuwa kama wenzetu wa Bara, tungesema kwamba Makunduchi ndio mjini kwa watu wa Kusini. Kwa hivyo, si dhani kama serikali ilifanya makosa kwenda kuimarisha barabara ya makao makuu ya wilaya yake.

Sote tunaamini kwamba inapotajwa barabara ile ya Makunduchi ilikuwa ni chachu kwa uimarikaji wa barabara nzima ya Kusini, ikiwemo Kizimkazi, Mtende, Kibuteni na maeneo mengine. Kwa msingi huo serikali haijaunda utaratibu wa matabaka, lakini barabara ile ya Makunduchi ina muda mrefu na ilikuwa ndio kiungo muhimu kwa wananchi wa Wilaya ya Kusini, kwa kutambua kuwa Makunduchi ndio katikati ya Wilaya ya Kusini.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba wananchi wa Ukongoroni Charawe na kama walivyo wengine wa Jimbo la Chwaka wamemchagua mwakilishi mpya na mimi nawashukuru sana kwa maamuzi yao hayo na ninawaomba waendelee kumuunga mkono mwakilishi wao. Lakini suala la kwamba lini watanufaika tayari maelezo tumeshatoa, kwamba serikali ina mpango mzuri na madhubuti wa kuona kilomita 48.7 za barabara hizi sita zinakamilika na wao kupata huduma ya barabara ya lami kama wanavyopata wananchi wengine katika maeneo ya Zanzibar.

Nam. 69

Bei ya Mwani Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Wananchi katika vijiji vya Jambiani, Paje, Bwejuu na Muungoni wamekuwa mstari wa mbele katika kilimo cha mwani, lakini bei imeendelea kuwa ni tatizo kwao jambo ambalo linawavunja moyo kutokana na kupanda kwa gharama za maisha.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kupandisha bei ya zao la mwani kama iilvyopandisha bei ya zao la karafuu na kuleta matumaini mapya kwa wakulima wa zao hilo.
(b) Kwa kuwa tatizo kubwa ni upatikanaji wa vifaa vya kuzalisha zao la mwani jambo ambalo limekuwa na usumbufu mkubwa kwa wakulima. Je, serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wakulima wa zao hilo kwa kuanzisha maduka ya ushirika katika maeneo yao ili kuwaondoshea usumbufu wanaoupata.
(c) Katika msimu uliopita wakulima wangapi wa mwani wamefaidika na mikopo inayotolewa na serikali ya kuwasaidia wajasiriamali wakiwemo wazalishaji kupitia sekta ya kilimo Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 69 lenvye vifungu (a), (b) na (c). Kwanza kabisa nakubaliana na Mhe.

Mwakilishi kwamba wananchi katika vijiji vya Jambiani, Paje, Bwejuu, Muungoni na vijiji vyenginevyo wamekuwa mstari wa mbele katika kilimo cha mwani, ingawa bei ya mwani inaendelea kuwa tatizo kwao, jambo ambalo linawavunja moyo kutokana na kupanda kwa gharama za maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 69 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia idara ya mazao ya baharini inaendelea na mchanganuo wa kutathmini gharama za uzalishaji na usafirishaji nchi za nje na bei ya zao la mwani katika soko la ndani na nje, ili kuweza kujadiliana na wenye makampuni ya kusafirisha mwani juu ya bei itakayolingana na gharama anazozipata mkulima katika uzalishaji wa mwani. Aidha, wizara yangu ipo katika mazungumzo na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ili kuweza kutafuta masoko zaidi ya bei ya mwani kwa nchi za nje. Pia wizara inaendelea na mazungumzo na Ubalozi wa China na washirika wengine wa maendeleo, juu ya kutoa taaluma ya kusarifu na kuongeza thamani zao la mwani na kuwahamasisha wananchi kuweza kuutumia mwani katika matumizi mengine. Kama vile chakula, sabuni na vipodozi ili kuliwezesha soko la ndani.

(b) Wizara ya Mifugo na Uvuvi imefanikiwa kuwahamasisha wakulima kuanzisha Jumuiya ya wakulima wa mwani wa Zanzibar, yaani JUWAMWAZA, Jumuiya ambayo tayari imeshasajiliwa na ni Jumuiya ambayo inawaunganisha wakulima wote wa mwani wa Zanzibar, ili kuwa na sauti moja katika kukiendeleza kilimo cha mwani na kutatua changamoto zinazowakabili. Zikiwemo upatikanaji wa vifaa, bei ya mwani. Aidha, wizara inaendelea kuwahamasisha wakulima wa mwani na wa mazao mengine ya baharini kupitia kamati zao za vijiji, kuanzisha vikundi vya kuweka na kukopa, yaani vya SACCOS ili kujiunga na vikundi kama hivyo vilivyopo ili waweze kujiendeleza kiuchumi na kijamii.

(c) Kwa kuwa mikopo kwa kawaida hutolewa kwa vikundi vya wajasiriamali. Kwa hivyo, na wakulima wa mwani wapo mmoja mmoja, hiyo inakuwa ni tatizo kwa taasisi za fedha kuweza kutoa mikopo kwa wakulima. Aidha, wizara yangu inawashajihisha wakulima wa mwani kuondokana na utegemezi zaidi wa mashirika ya mikopo yenye masharti magumu na badala yake wajiunge na *SACCOS* ambazo zina masharti nafuu. Hata hivyo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaendelea na mazungumo na taasisi husika ili

kuweza kufikiria utaratibu muafaka wa kuweza kuwasaidia wakulima wa mwani kufaidika na mikopo inayotolewa na taasisi hizo kwa masharti nafuu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri.

(a) Kwa nini serikali imekuwa ikipandisha bei ya mwani, wakati wakulima hawa wanalipwa bei ya chini na mwani huo umekuwa na soko kubwa katika soko la China.

(b) Ni chombo gani kinachodhibiti bei ya mwani badala ya kujitokeza kampuni moja kununua mwani, tofauti na bei ilivyokuwa mwanzo. Mwanzo bei ilikuwa shilingi 200, baada ya kutokea kampuni nyengine ndio ikanunua kwa bei ya shilingi 4,000. Hebu tueleze Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kuna tofauti ya mwani na karafuu. Karafuu ni zao la serikali, kwa maana linadhibitiwa na serikali, lakini mwani sio zao la serikali ni zao binafsi, kwa hivyo ni zao ambalo liko huru kabisa kibiashara na ndio maana serikali haiwezi kutia mkono wake. Kubwa ambacho inaweza kukifanya serikali ni kujaribu kukaa kama nilivyoeleza awali, kukaa na makapuni yale ili kuona vipi wanaweza wakarekebisha bei zao, lakini sio kuwalazimisha, bali ni kukaa kuzungumza na kufikia muafaka. Mwani ni tofauti na karafuu, hili ni zao binafsi na liko huru kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la bei kutoka shilingi 200 mpaka shilingi 400, ni kweli bei imepanda na kubwa ambalo tunalifanya hivi sasa ni kuwashajihisha makampuni mengine ili waingie katika suala hili, yaani wanunuwe mwani ili kushajihisha ule ushindani. Kwa sababu hivi sasa kuna makampuni mawili tu, au makampuni matatu, kwa hivyo kuna kitu kinaitwa *monopoly* na siku zote hii ni ghulka au ni utamaduni wa makampuni ya kibiashara, siku zote wanapohodhi wanakuwa na nguvu zaidi, lakini tunachokifanya hivi sasa ni kuwahamasisha makampuni mengine binafsi ili na wao waingie pale ili kuwe na ushindani mkubwa, naamini utakapokuwa ushindani mkubwa bila shaka mkulima wa mwani atafaidika.

Vile vile kama nilivyosema awali kwamba serikali bado haijasita, tunaendelea kukaa na taasisi nyengine husika, yaani taasisi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ili kufanya uchunguzi wa hizi gharama na tutakapofika pahala tukahisi kweli kuna haja ya kuongeza bei zaidi ya hiyo, basi tutatizama kama je, ZSTC wanaweza wakafanya biashara na wao wakanunua mwani huu

kama walivyokuwa wananunua karafuu. Kwa hivyo, suala hili bado tumo ndani ya utaratibu nafikiri tutafikia hatma hivi karibuni, ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri, kwa sababu mwani hupandwa katika sehemu za mazalia ya samaki. Je, katika hizo sehemu zinazopandwa mwani hauharibu mazingira.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, sitosema kama unaharibu mazingira. Kwa upande mmoja nitasema unaharibu mazingira, labda katika sekta ya utalii, lakini kwa upande wa pili, mwani vile vile ni sehemu ya chakula cha samaki pia. Kwa hivyo, nafikiri samaki kwa upande mwengine wanafaidika na hilo. Kwa hivyo, sisemi kama ni uharibifu wa mazingira, ahsante.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, lakini inanipasa nimuulize swali la nyongeza. Mhe. Waziri katika swali mama ulikubali kama kweli bei ya mwani iko chini kabisa na wakulima wetu wanalalamika kuwa wanafanyakazi kubwa lakini kipato kidogo. Je, Mhe. Waziri huoni sasa hivi iko haja ya kuwatafutia mitambo wakashindika wao wenyewe na wakapata fursa ya kuweza kuuza wenyewe nje, ili kupata kuwa matajiri.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tunachokifanya hivi sasa ni kuwashajihisha wakulima wa mwani kusarifu huu mwani, ili kuweza kutengeneza soko la ndani na kuweza kutengeneza matumizi mengine kama chakula, sabuni, vipodozi na kadhalika. Nimesema hapa kwamba tayari hivi sasa vikundi vyengine vimeshajitokeza, kama kule Kidoti na Paje, tayari wameshaanzisha huo utaratibu wa kusarifu huo mwani kwa kutengeneza sabuni. Vile vile tuko karibu sana na Ubalozi wa China ili kuona kwamba mwani vile vile unakuwa ni sehemu ya chakula hasa katika mahoteli yetu ya kitalii hapa Zanzibar, nahisi tukifikia hatua hiyo, basi lile lalamiko kubwa au kilio kikubwa cha masuala ya bei kwa soko la nje, nafikiri kitapungua.

Kwa hivyo, tunaendelea na tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe ndani ya majimbo basi wawahamasishe wakulima wa mwani waingie katika hatua hii ya kusarifu mwani ili kutengeneza sabuni na vipodozi na kuweza kuongeza thamani ya lile zao. Tunashukuru hivi sasa hali inakwenda vizuri kama Kidoti kule tumekwenda na tumeona wanatengeneza sabuni na wanawauzia mahotelini, wanauwanika mwani ule na kuusaga wanatengeneza juisi. Hivi sasa tuko katika juhudi ya kuwatafutia masoko ndani ya mahoteli ili kuona

kwamba mwani soko lake linakwenda vizuri, hususan ndani badala ya kutegemea soko la nje zaidi, nashukuru.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii, kwa idhini yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa wanawake wa ukanda wa pwani wengi wao ni wakulima wa mwani na kwa kuwa wanawake hawa wanapata tabu sana wakati wa mavuno kukodi vyombo vya kwenda kuwachukulia mwani huo kule baharini. Je, Mhe. Waziri wizara yako ina mpango gani wa kuwatafutia vyombo ama kwa mkopo au kwa misaada wanawake hawa, ili waweze kufaidika na kupunguza gharama ile ya uchukuzi wa mwani wao huko baharini.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, hili ni swali zuri sana. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu katika ziara yangu nilivitembelea vikundi vingi tu, hasa ukanda wa pwani ambavyo vinajishughulisha na kilimo cha mwani. Wengi wao wameleta kilio hicho, hususan ghuba ya Chwaka hii ambayo inabidi lazima uvuke ule mkondo ili uende kwenye maji ambayo ni kidogo kwa kilimo cha mwani. Kilio chao kikubwa ni kwamba hawana usafiri, hata kama upo usafiri hauna uhakika.

Mhe. Mwenyenyekiti, mimi kama waziri wa wizara hii niliwaahidi kwamba mara tu tutakapopata vyombo vile vya *fiber*, basi tutawatizama zaidi wakulima wa mwani na tutawakopesha na wengine kama ni kuwasaidia basi tutawasaidia *fibus*. Kwa hivyo, kipaumbele tumewapa zaidi wakulima wa mwani na hasa ukichukulia kwamba asilimia kubwa ya watu waishio ukanda huo ni wanawake, na wanapata tabu kwa kweli. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe hilo suala tayari tumeshaliingiza katika ratiba yetu ya watu wa kupewa *fibus* hizo, ahsante.

Nam. 139

Baraza la Vijana Zanzibar

Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati
Kwa mwaka wa Fedha 2012/2013

UTANGULIZI

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa liingie katika Kamati ya Matumizi ili niweze kutoa maelezo kuhusu malengo yaliyomo katika makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kutujaalia afya njema na uzima na kwa kuniwezesha kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu, kuwasilisha hotuba ya Wizara hii mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, aidha kwa niaba ya viongozi na wafanyakazi wote wa wizara ninayoiongoza, napenda kuchukua nafasi hii adhimu, kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dokta Ali Mohammed Shein, kwa ufuatiliaji wake makini wa utendaji wa Serikali anayoiongoza, uliopelekea kurekebisha safu ya viongozi wakuu wa mawizara, nikiwemo mimi mwenyewe. Naamini ni uamuzi wa kufanikisha zaidi maendeleo ya wananchi wa Zanzibar katika Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote waliohusika na mabadiliko hayo. Ni imani yangu kwamba watayachukulia mabadiliko hayo na upya wao katika wizara wanazoziongoza kuwa ni changamoto kwa upande mmoja na chachu kwa upande mwengine ya kuwatumikia wananchi wenzao kwa moyo, bidii na maarifa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiwa mmojawapo wa Mawaziri hao, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwangu ya kuniteua kuiongoza Wizara hii. Namuahidi yeye, Wananchi na Baraza lako hili Tukufu kwamba nitaienzi imani hiyo kwa kutekeleza majukumu yangu ya nchi kwa uzalendo, juhudi na maarifa kwa kadri ya uwezo wangu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu anisaidie, pamoja na wajumbe wote wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, aidha nachukua nafasi hii kutoa pole kwa wenzetu waliopatwa na msiba katika ajali iliohusisha meli ya MV Spice Islanders iliotokea tarehe 10 Septemba, 2011. Namuomba Mwenyezi Mungu (S.W) azilaze roho za marehemu mahala pema peponi na atupe subira sote ambao kwa namna moja au nyengine tumeguswa na msiba ule.

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Wizara yangu kutoa mkono wa rambi rambi kwa Baraza hili Tukufu, familia pamoja na Wazanzibari wote kwa vifo vya waliokuwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu, marehemu Salum Amour Mtondoo (Jimbo la Bububu na Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi) na marehemu Mussa Khamis Silima (Jimbo la Uzini na Mbunge kupitia Baraza hili) ambavyo vilitokea kwenye Mwaka wa Fedha unaomalizika. Wote walikuwa na mchango mkubwa katika Baraza hili na kwa wizara yangu, michango ambayo imesaidia sana kuifikisha wizara katika upeo wa utekelezaji iliyoufikia. Tunamuomba Mwenyezi Mungu (S.W) azilaze roho za marehemu mahala pema peponi - Amin.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ni mojawapo ya Wizara kumi na sita (16) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo imeundwa na Taasisi zifuatazo:-

i. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti,
ii. Idara ya Utumishi na Uendeshaji,
iii. Afisi Kuu Pemba
iv. Idara ya Ardhi na Usajili,
v. Idara ya Mipango Miji na Vijiji,
vi. Idara ya Upimaji na Ramani,
vii. Idara ya Ujenzi,
viii. Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi,
ix. Idara ya Nishati na Madini,
x. Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe,
xi. Mamlaka ya Maji,
xii. Shirika la Umeme,
xiii. Mahakama ya Ardhi,
xiv. Afisi ya Mrajis wa Ardhi,
xv. Bodi ya Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo,
xvi. Bodi ya Wakandarasi,
xvii. Bodi ya Nyumba,
xviii. Bodi ya Uhaulishaji Ardhi,
xix. Bodi ya Wapimaji Ardhi,
xx. Bodi ya Kondominio.

Mhe. Mwenyekiti, katika upangaji na utekelezaji wa malengo, kazi na shughuli za Wizara, msisitizo umewekwa kwa kuangalia Sera na Mipango Mikuu ya Taifa kama vile Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020, MKUZA II, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2010 - 2015 pamoja na Sera na Mpango Mkakati wa Wizara.

Mapato na Matumizi:

Mhe. Mwenyekiti, ukusanyaji wa mapato ni kigezo muhimu sana cha mafanikio ya utekelezaji. Wizara yangu katika Mwaka wa Fedha 2011/2012 ilipangiwa kukusanya jumla ya Tsh 2,198,343,000 kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato ya Taasisi zake. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2011 jumla ya Tsh 1,825,477,503 zilikwishakusanywa, sawa na asilimia 83.04 ya makadirio. Matarajio ya Wizara yangu ni kuwa ifikapo Juni 2012 tutakuwa tumefikia malengo yaliyowekwa.

Kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatanisho "A"

11. Mhe. Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2011/2012, Bajeti ya Wizara yangu ilikuwa ni Tsh 10,022,902,000. Kazi za Maendeleo zilipangiwa Tsh 4,996,902,000 na kazi za kawaida zilipangiwa Tsh 5,026,000,000. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2012 Wizara yangu ilikwishapatiwa Tsh 4,052,254,000 kwa kazi za Maendeleo sawa na asilimia 81 na Tsh 4,153,742,548 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 83 ya makadirio, hivyo kufanya jumla ya fedha zote zilizoingizwa kuwa ni Tsh 8,205,996,548 sawa na asilimia 81.87 ya makisio yote.
Kwa ufafanuzi zaidi angalia kiambatanisho "B1 na B2"

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2011/2012 NA MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kukamilisha muhtasari huu wa mapato na matumizi ya Wizara yangu, sasa naomba uniruhusu kuelezea kwa kina utekelezaji wa kazi za kawaida na za maendeleo kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2011/2012 na malengo ya Mwaka wa Fedha 2012/2013 kupitia kila Taasisi zilizomo ndani ya Wizara hii.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

UTEKELEZAJI

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii inawajibika kusimamia na kuratibu kazi zote za kawaida na za maendeleo za Wizara. Kazi za maendeleo zilizojumuisha ufuatiliaji na tathmini (*Monitoring and Evaluation*) zilizosimamiwa na Idara hii ni pamoja na Miradi ya Maendeleo ifuatayo:

i. Usambazaji Maji Vijijini
ii. Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini
iii. Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji (Awamu ya Pili)
iv. Maji na Usafi wa Mazingira. (AfDB)

v. Kuimarisha Miundombinu ya Maji na Kuijengea Uwezo Mamlaka Kifedha (ADF12)
vi. Uimarishaji wa Mji wa Zanzibar (ZUSP)
vii. Usambazaji Umeme Vijijini.
viii. Kuweka Njia ya Pili ya Umeme Ubungo hadi Mtoni (MCC)
ix. Kufunga Mita 10, 000 za TUKUZA Unguja na Pemba
x. Uhuishaji na Uimarishaji wa Miundombinu ya Umeme kwa Unguja (JICA)
xi. Matengenezo ya Kituo cha Umeme Mpendae
xii. Utekelezaji wa Sera ya Nishati.
xiii. Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Uhifadhi wa Mazingira (SMOLE II)
xiv. Utafiti wa Maji na Nishati Mbadala
xv. Ujenzi wa Ukuta wa Ukingo wa Bahari Mizingani.
xvi. Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo Mpapa
xvii. Kuimarisha Mazingira ya Biashara Kupitia Sekta ya Ardhi (MKUMBITA)

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ni kiungo cha utekelezaji wa shughuli za Wizara na Taasisi zake zote, sambamba na kushirikiana na Taasisi nyengine za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jumuiya mbali mbali za Kiserikali na zisizo za Kiserikali na Jumuiya za Kimataifa.

Kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Idara imefanikisha vikao na Wizara ya Maji kwa ngazi ya Makatibu Wakuu ambapo Rasimu ya Mpango Kazi wa Kuimarisha mashirikiano na Kubadilishana uzoefu katika uimarishaji wa huduma za maji nchini imetayarishwa. Haikuwezekana kufikia ngazi ya Mawaziri kutokana na mabadiliko ya uongozi wa Safu hiyo kwa pande zote mbili.

Aidha Idara ilifanikisha mikutano hadi ngazi ya Mawaziri wa Wizara za masuala ya Nishati, ambapo suala la deni la Umeme wa *TANESCO* na *ZECO* lilifikia muafaka.

MALENGO

Mhe. Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inakusudia kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ifuatayo:

i. Usambazaji Maji Vijijini
ii. Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini

iii. Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji (Awamu ya Pili)
iv. Maji na Usafi wa Mazingira. (AfDB)
v. Kuimarisha Miundombinu ya Maji na Kuijengea Uwezo Mamlaka Kifedha (ADF12)
vi. Uimarishaji wa Mji wa Zanzibar (ZUSP)
vii. Usambazaji Umeme Vijijini.
viii. Kuweka Njia ya Pili ya Umeme Ubungo hadi Mtoni (MCC)
ix. Kufunga Mita 50, 000 za TUKUZA Unguja na Pemba
x. Uhuishaji na Uimarishaji wa Miundombinu ya Umeme kwa Unguja (JICA)
xi. Utekelezaji wa Sera ya Nishati.
xii. Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Uhifadhi wa Mazingira (SMOLE II)
xiii. Utafiti wa Nishati Mbadala
xiv. Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo Mpapa
xv. Ujenzi wa Ukuta wa Ukingo wa Bahari Mizingani
xvi. Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA).

Mhesimiwa Spika, Idara pia imepanga kuimarisha uhusiano wa kisekta baina ya taasisi zake na za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kusimamia utayarishaji na utekelezaji wa Sera, Tafiti na Mipango ya Sekta za Wizara.

Mhesimiwa Spika, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza malengo yake kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, naomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Tsh. 2,174,000,000 kwa ajili ya kazi za kawaida na Tsh. 4,832,000,000 kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

UTEKELEZAJI

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kueleza utekelezaji wa idara hii, naomba kuipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa hatua ya kuwaongezea mishahara watumishi wa umma, hatua hii imeleta faraja kwa wafanyakazi na kuongeza ari katika utendaji kazi kwa ufanisi na uwajibikaji katika maeneo yao.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Idara hii imeendeleza jitihada zake katika kuangalia zaidi suala la rasilimali watu kwa kuwapatia fursa na haki mbali mbali ikiwemo kuwaendeleza kimafunzo na kimaslahi, kwa kuelewa

kuwa wafanyakazi ndio rasilimali muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imeajiri wafanyakazi 66 kwa kujaza nafasi zilizokuwa wazi kutokana na kustaafu, vifo au nafasi mpya. Aidha, wafanyakazi 86 wamestaafu kazi na 12 wamefariki dunia (Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahala pema peponi - AMIN)

Mafunzo kwa Wafanyakazi

Mhe. Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 wafanyakazi 84 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali vya ndani na nje ya nchi kwa viwango tofauti vya elimu. Aidha, Wizara imewapatia wafanyakazi 91 mafunzo ya muda mfupi ili kuwaimarisha kiuwezo na kiutendaji. Kwa kiwango kikubwa mafunzo hayo yamedhaminiwa na miradi mbali mbali iliyomo katika Taasisi zetu.
Kwa ufafanuzi zaidi naomba angalia viambatanisho “C1 na C 2”.

Masuala ya Jinsia na Ukimwi

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu haikuacha kuyapa kipaumbele masuala ya Jinsia na Ukimwi kwa kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Kutoa elimu kwenye masuala ya Ukimwi na Jinsia kwa wafanyakazi wa Wizara, pia kuwashajiisha wafanyakazi kupima afya zao kwa hiari.

ii. Aidha kwa kuwa Wizara ina mfuko wa Afya kwa wafanyakazi uliyoanzishwa na wafanyakazi wenyewe, kwa sasa umo katika harakati za uzinduzi (*launching*) ili uweze kufanya kazi ipasavyo.

MALENGO

Mhe. Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 Idara ya Utumishi na Uendeshaji inakusudia kusimamia utekelezaji wa kazi zifuatazo:

i. Kuimarisha ufanisi wa utendaji kwa kuhakikisha upatikanaji wa nyenzo za kufanyia kazi kwa wakati na viwango thabiti pamoja na kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi.

ii. Kuhakikisha kuwa maslahi ya wafanyakazi yanaimarishwa kwa kuwapatia haki na huduma stahiki kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

iii. Kuimarisha uwezo wa watendaji kwa kuwaendeleza kimasomo kwa kuzingatia program ya mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi pamoja na kubadilishana uzoefu.

iv. Kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanatekeleza majukumu yao kwa uelewa mkubwa wa elimu ya Jinsia na Ukimwi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Utumishi na Uendeshaji iweze kutekeleza malengo yake kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, naomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Tsh. 738,000,000 kwa kazi za kawaida.

IDARA YA ARDHI NA USAJILI

UTEKELEZAJI

Usimamizi wa Ukodishaji Ardhi

Mhe. Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2011/2012, Mikataba 61 ya ukodishaji ardhi ilitiwa saini na kupewa wawekezaji mbali mbali. Miongoni mwao Mikataba 40 ni kwa ajili ya mahoteli, 2 kwa ajili ya Vituo vya mafuta, 1 kwa ajili ya Kiwanja cha kufurahishia Watoto, 1 Skuli, 12 makaazi kwa wageni na Mikataba 5 kwa viwanda.

Utayarishaji na Utoaji Hati:

Mhe. Mwenyekiti, kuna dhana ya ucheleweshwaji wa Hati za haki ya matumizi ya ardhi, lakini ifahamike kwamba azma ya Serikali ni utowaji wa hati kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za ardhi. Jambo hili limekuwa likifanyika kwa sababu ya uwelewa mdogo wa Sheria na taratibu zinazoongoza masuala ya ardhi.

Sheria ya Uhaulishaji Nambari 8 ya mwaka 1994 pamoja na marekebisho yake nambari 10/2007 inatambua na kusisitiza kuwa uhaulishaji wowote wa ardhi ni lazima upitie kwenye Bodi ya Uhaulishaji Ardhi kwa uhakiki. Kwa bahati mbaya, kuna baadhi ya wananchi wamekuwa wakikengeuka Sheria hiyo kwa kuhaulisha ardhi bila ya kupitia katika Bodi na wamekuwa wakiomba Hati ya haki ya Matumizi ya Ardhi. Jambo hili limekuwa likichangia ucheleweshaji huo kwa kukosekana uthibitisho wa umiliki wao.
Vile vile, ucheleweshwaji wa upatikanaji wa Hati ya haki ya matumizi ya ardhi hutokea kutokana na baadhi ya waombaji kutokuwa na viambatanisho vya uhakika juu ya umiliki wao wa ardhi, jambo ambalo huilazimu Wizara kuchukua muda mwingi katika kujiridhisha kabla ya Hati kutolewa.

Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa na utaratibu wa Hati zote za Haki za Matumizi ya Ardhi kupelekwa kwa Waziri kama vile za manunuzi, hiba na urithi kwa ajili ya kupatiwa hati. Hii ilitokana kwa kipindi kirefu kutokuwepo kwa Mrajis wa Ardhi ambapo hati hizo zilipaswa kupelekwa kwa Mrajis bila ya kupita kwa Waziri. Lakini kwa sasa Mrajis ameshateuliwa hivyo tunategemea kuondokana na mlundikano wa hati zote kupelekwa kwa Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Ardhi na Usajili imeendeleza utayarishaji na utoaji wa Hati, ambapo hadi kufikia Machi 2012 Hati 649 zilikwishatolewa kwa maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba. Kati ya hizo, 62 zimetolewa kwa ajili ya kilimo na 380 kwa ajili ya maeneo mapya ya Tunguu na Ukanda wa Pwani. Hati 207 zimebadilishwa kutoka Hati za muda ambazo vilevile zitapaswa kufanyiwa usajili na Mrajisi wa Ardhi. Zoezi la Kubadilisha Hati za muda kuwa za kudumu ni endelevu.

Kuimarisha Uwekaji Kumbukumbu za Ardhi

Mhe. Mwenyekiti, katika utayarishaji na uwekaji kumbukumbu za maeneo yaliyotolewa na Serikali, Idara imezifanyia kazi Hati 806 za maeneo mbalimbali kwa kuziingiza katika kompyuta.

Uthamini na Uhaulishaji

Mhe. Mwenyekiti, kazi 419 za uthamini, uhaulishaji na ugawaji wa ardhi zimekamilika na kukabidhiwa wenyewe, kutoka katika taasisi mbali mbali. Aidha, maombi ya uhaulishaji wa ardhi 459 yamepokelewa ambapo 278 yamekubaliwa na 25 yamekataliwa na maombi 110 yametolewa maelekezo.

Kiwango hichi cha maombi yenye kasoro kinaainisha uwelewa mdogo wa jamii, wakiwemo watendaji wa ngazi tofauti, juu ya Sheria za ardhi kwa jumla, hali inayochangia katika ongezeko la migogoro ya ardhi.

Sheria na Kanuni za Uthamini

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Ardhi na Usajili imeendeleza utayarishaji wa Sheria na Kanuni za Uthamini ambapo Rasimu ya kwanza imeshawasilishwa kwa Kamati Tendaji ya Wizara.

Kuimarisha Udhibiti Ardhi

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha udhibiti wa matumizi endelevu ya Ardhi Idara kwa kushirikiana na Baraza la Manispaa na Idara ya Mipango Miji na vijiji imeyapitia na kuyakagua maeneo yote ya mjini ili kujiridhisha kutokana na maombi ya ujenzi yaliopokelewa. Maombi hayo ni kama yanavyoonekana katika Jaduweli ifuatayo:-

Jaduweli Nambari 1

AINA YA MAOMBI	IDADI YA MAOMBI	MAOMBI YALIOKUBALIWA	MAOMBI YALIOKATALIWA
Ujenzi wa Nyumba katika maeneo mapya	14	12	2
Matengenezo madogo madogo	58	40	18
JUMLA	72	52	20

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa maeneo ya uwekezaji jumla ya miradi 172 imefanyiwa ukaguzi katika ukanda wa utalii wa Zanzibar katika maeneo ya Paje, Bwejuu, Dongwe, Tunguu, Mkokotoni, Michamvi, Chuini, Kendwa, Kizimkazi, Nungwi, Chwaka, Pwani Mchangani na Matemwe.

Mhe. Mwenyekiti, Idara pia imefanya uhakiki wa viwanja vilivyotolewa na Serikali kabla ya mwaka 2000 na ambavyo havijaendelezwa katika maeneo ya Mazizini, Mbweni, M'Kwerekwe, Mombasa na Kidichi. Takriban viwanja 206 viligundulika kuwa havijaendelezwa. Hatua za kuvibatilisha (*termination*) zinaendelea.

AFISI YA MRAJIS WA ARDHI:

Mhe. Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2011/2012, Afisi ya Mrajis wa Ardhi imeendelea na utekelezaji wa shughuli zake za Usajili wa Ardhi nchini. Shughuli hizo zilikwama kwa muda kutokana na kutokuwepo Msajili wa Ardhi, hata hivyo, hivi karibuni Mheshimiwa Rais amefanya uteuzi wa nafasi hiyo, na shughuli zote za usajili zimepangwa kuendelea kwa ufanisi.

Kwa upande wa Kisiwani Pemba shughuli za majaribio ya Usajili wa ardhi zinaendelea katika shehia ya Mkoroshoni Chake Chake Pemba. Shughuli hizo zinafadhiliwa na Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Uhifadhi wa Mazingira (*SMOLE II*).

MAHAKAMA YA ARDHI:

Mhe. Mwenyekiti, Mahakama ya Ardhi imeendelea kupokea na kusikiliza kesi mbalimbali zinazohusu Ardhi. Hadi 31 Machi, 2012 kesi 188 zilikwishafunguliwa. 101 Unguja na 87 Pemba.

Kesi zilizohukumiwa baina ya Julai, 2011 na Machi, 2012 ni 95; 15 Unguja na 80 Pemba.

MALENGO

Mhe. Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 Idara ya Ardhi na Usajili inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendeleza ubadilishaji hati za muda kuwa za kudumu, sambamba na kutoa hati mpya kwa watakaopewa viwanja.

ii. Kuendeleza uwekaji kumbukumbu za viwanja kwa njia za kisasa.

iii. Kuendeleza uimarishaji wa shughuli za Mahkama ya Ardhi kwa lengo la kupunguza migogoro ya Ardhi nchini.

iv. Kuendeleza utambuzi na uthibitishaji wa wenye haki za matumizi ya ardhi ndani ya Shehia za Ng'ambo pamoja na vijijini.

MUSSA 3

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: (anaendelea) kwa upande wa maeneo ya uwekezaji jumla ya miradi 172 imefanyiwa ukaguzi katika Ukanda wa Utalii wa Zanzibar katika maeneo ya Paje, Bwejuu, Dongwe, Tunguu, Mkokotoni, Michamvi, Chuini, Kendwa, Kizimkazi, Nungwi, Chwaka, Pwani Mchangani na Matemwe.

Mhe. Mwenyekiti, idara pia imefanya uhakiki wa viwanja vilivyotolewa na Serikali kabla ya mwaka 2000 na ambavyo havijaendelezwa katika maeneo ya Mazizini, Mbweni, Mwanakwerekwe, Mombasa na Kidichi. Takriban viwanja 206 viligundulika kuwa havijaendelezwa. Hatua za kuvibatilisha (*termination*) zinaendelea.

AFISI YA MRAJIS WA ARDHI:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Afisi ya Mrajis wa Ardhi imeendelea na utekelezaji wa shughuli zake za Usajili wa Ardhi nchini. Shughuli hizo zilikwama kwa muda kutokana na kutowepo Msajili wa Ardhi. Hata hivyo, hivi karibuni Mhe. Rais amefanya uteuzi wa nafasi hiyo, na shughuli zote za usajili zimepangwa kuendelea kwa ufanisi.

Kwa upande wa Kisiwani Pemba shughuli za majaribio ya Usajili wa ardhi zinaendelea katika shehia ya Mkoroshoni Chake Chake Pemba. Shughuli hizo zinafadhiliwa na Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Uhifadhi wa Mazingira (*SMOLE II*).

MAHAKAMA YA ARDHI:

Mhe. Mwenyekiti, Mahakama ya Ardhi imeendelea kupokea na kusikiliza kesi mbali mbali zinazohusu Ardhi. Hadi 31 Machi, 2012 kesi 188 zilikwishafunguliwa. 101 Unguja na 87 Pemba. Kesi zilizohukumiwa baina ya Julai, 2011 na Machi, 2012 ni 95; 15 Unguja na 80 Pemba.

MALENGO:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Ardhi na Usajili inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

v. Kuendeleza ubadilishaji hati za muda kuwa za kudumu, sambamba na kutoa hati mpya kwa watakaopewa viwanja.

vi. Kuendeleza uwekaji kumbukumbu za viwanja kwa njia za kisasa.

vii. Kuendeleza uimarishaji wa shughuli za Mahakama ya Ardhi kwa lengo la kupunguza migogoro ya Ardhi nchini.

viii. Kuendeleza utambuzi na uthibitishaji wa wenye haki za matumizi ya ardhi ndani ya Shehia za Ng'ambo pamoja na vijijini.

ix. Kuendeleza usimamizi wa ukodishwaji ardhi (*Land leases*) nchini.

x. Kuimarisha udhibiti wa matumizi endelevu ya Ardhi na kuwachukulia hatua za Kisheria wote watakaovamia ardhi.

xi. Kusimamia shughuli za uendelezaji wa Bodi ya Uhaulishaji Ardhi.

xii. Kufanya uthamini na ugawaji wa ardhi kwa shughuli mbali mbali ikiwemo kilimo, makaazi na biashara, ili kukuza kipato cha wananchi wa Zanzibar.

xiii. Kuifanyia mapitio Sera ya Ardhi pamoja na kuimarisha Sheria mbali mbali za Ardhi.

xiv. Kutunza na kuimarisha maeneo ya ukodishaji wa ardhi kwa kuhakikisha kwamba wanaendesha kwa mujibu wa makubaliano yaliyoainishwa kwenye mikataba na miongozo ya matumizi ya ardhi.

xv. Kutayarisha muongozo rasmi kwa maombi yote ya usajili wa ardhi.

xvi. Kuendelea kutayarisha hati za usajili wa ardhi kwa maeneo yaliyotolewa na serikali, yaliyomaliza utambuzi kama Mji Mkongwe, yaliyohaulishwa na maombi binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 706,000,000 kwa ajili ya kazi za Kawaida katika Idara ya Ardhi na Usajili, Afisi ya Mrajis wa Ardhi na Mahakama ya Ardhi.

IDARA YA MIPANGO YA MIJI NA VIJIJI:
UTEKELEZAJI:

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango ya Miji na Vijiji ndio Mpangaji, Mratibu na Msimamizi wa mipango bora ya uendelezaji, uhifadhi na matumizi endelevu ya ardhi nchini. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Idara hii ilitekeleza kazi zifuatazo:-

Kuratibu na Kusimamia Kazi Zote za Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi Nchini Katika Ngazi za Mikoa, Wilaya , Miji na Vijiji:

Mhe. Mwenyekiti, idara imeanza utekelezaji wa Mpango wa Majaribio ya matumizi bora ya ardhi nchini katika ngazi ya Wilaya, ambapo tathmini ya ardhi itakayowezesha kuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi katika wilaya tisa za Unguja na Pemba imeshakamilika. Kazi iliyobakia ni kutoa elimu juu ya mipango hiyo na utekelezaji wake.

Kwa ngazi ya vijiji, idara imeanza utekelezaji wa kazi hiyo kwa kuvichagua vijiji vya Nungwi kwa Unguja na Mgelema kwa Pemba kuwa ni sehemu ya majaribio hayo.

Kutayarisha Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi Nchini (*National Land Use Plan*):

Mhe. Mwenyekiti, Mpango Mkuu wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Ardhi ambao ulitayarishwa mwaka tisini na tano (1995) umeshafanyiwa mapitio, ili uende sambamba na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kimazingira na kiteknolojia ambayo yametokea nchini na duniani katika kipindi cha miaka ishirini iliyopita.

Hatua iliyofikiwa ni kukamilisha Mpango wa utekelezaji na kukutana na wadau na wananchi kuwaelewesha juu ya Mpango huo.

Vile vile, idara inaendelea na mapitio ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi za Kanda za fukwe. Eneo la Nungwi lenye changamoto nyingi za utalii ndilo linalofanyiwa kazi hivi sasa.

Kuangalia na Kutayarisha Upya Mfumo wa Mipango ya Uendelezaji wa Maeneo Mapya ya Makaazi Pamoja na Huduma Mbali mbali:

Mhe. Mwenyekiti, uendelezaji wa maeneo mapya ya makaazi pamoja na huduma zake unahitaji mashirikiano ya taasisi mbalimbali. Kwa kulielewa hilo, Idara ya Mipango Miji na Vijiji inaendelea kutayarisha mfumo utakaoshirikisha kikamilifu taasisi zote za serikali zinazohusika na utoaji wa huduma na uwekaji wa miundombinu katika maeneo mapya ya makaazi.

Ripoti ya awali ya kazi hiyo inaendelea kujadiliwa, ili hatimae kuwa na mfumo madhubuti wa uendelezaji wa maeneo mapya ya makaazi. Lengo kuu la Mpango huu ni kuwa na maeneo ya makaazi yenye huduma zote za kijamii na miundombinu (*Site and Services*) na kuachana na mtindo uliozoeleka wa kujenga katika maeneo mapya bila ya kuwa na huduma na miundombinu. Utaratibu huu unahitaji muda mrefu zaidi kuliko ule uliozoeleka wa kutoa viwanja kwenye maeneo ambayo miundombinu bado haijakamilika.

Utaratibu utakaoanzishwa unakusudia kuhakikisha kila taasisi inawajibika katika eneo lake katika suala la uendelezaji wa maeneo, kwani suala hilo likiachiwa taasisi moja peke yake haliwezi kufanikiwa.

Kutayarisha Mipango Bora ya Kuyarekebisha na Kuyaendeleza (*Improvement Plans*) Maeneo Mbali mbali Yaliyojengwa bila ya Mpangilio:

Mhe. Mwenyekiti, zaidi ya asilimia sabini ya miji yetu imejengwa bila ya mpangilio maalum (*Unplanned Settlements*). Sababu zilizochangia ni nyingi, zikiwemo za kihistoria, kiuchumi na kitaalamu.

Zanzibar ni miongoni mwa nchi zinazoongoza Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya watu kulinganisha na rasilimali ya ardhi iliyonayo, hivyo umuhimu wa mipango bora ya matumizi ya ardhi na ujenzi hususan katika maeneo ya miji si jambo la hiari. Ni lazima tuwe na mipango bora na endelevu ya kuendeleza miji yetu.

Mhe. Mwenyekiti, idara imedhamiria kuandaa Mipango Bora ya kuyaendeleza maeneo yaliyojengwa ovyo na kuyarekebisha kutoka yalivyo sasa kuwa yaliyopangwa (*Planned Area*) au angalau "Semi Planned Area''. Mpango huu ni mkubwa na endelevu unaohitaji ushirikiano endelevu wa wananchi wote.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, kwa kuwatumia wanafunzi wa Vyuo Vikuu mbali mbali, idara ilianza kwa kufanya utafiti katika sehemu ya eneo la Kikwajuni na kutayarisha Mpango mdogo wa mfano wa kurekebisha maeneo ambayo yamejengwa bila ya mpangilio.

Tafiti hizo zimetusaidia kupata sura ya matatizo yaliopo katika maeneo hayo na njia mbalimbali za kuyatatua. Mbinu nyingine inayotumika ni kuwapa miongozo (*guidelines*) wananchi wanaokusudia kuvunja nyumba zao za chini na kujenga za ghorofa. *(Makofi)*

Kuendeleza Mashirikiano na Baraza la Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya Katika Kudhibiti Ujenzi:

Mhe. Mwenyekiti, kwa miaka mingi suala la kusimamia ujenzi nchini limekuwa na matatizo mengi yakiwemo ya kisheria na kiutendaji.

Katika kuikabili changamoto hiyo, idara iliendelea kutoa elimu pamoja na kubadilishana uzoefu na taasisi zinazohusika na utoaji wa vibali vya ujenzi, ili kuwa na mfumo bora zaidi wa utoaji wa vibali vya ujenzi nchini pamoja na usimamizi wake, ili kuhakikisha matumizi bora ya ardhi mijini na vijijini yanafanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa jitihada za hivi karibuni ni kukifanyia mapitio chombo kinachohusika na udhibiti ujenzi mjini yaani "*Urban Development Control Authority – UDCA*". Ili kuwa na chombo kipya na madhubuti kitakachoshirikisha wajumbe kutoka taasisi mbalimbali. Kazi ya chombo hicho "*Planning, Development and Management Authority –PDMA*" haitakuwa kutoa vibali vya ujenzi tu kama ilivyo *UDCA* ya sasa, bali pia kupanga, na kusimamia maendeleo na matumizi ya ardhi pamoja na kuhifadhi urithi wa eneo lote la Mkoa wa Mjini Magharibi.

Pia, *PDMA* itahusika na kutoa ushauri wa kitalaamu kwa taasisi za Ardhi, Mamlaka ya Mji Mkongwe, Baraza la Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya kuhusu masuala yote ya uendelezaji wa miji na ujenzi.

Hatua zilizofikiwa ni kukamilika kwa Ripoti pamoja na Kanuni za chombo hicho, tayari kwa kupelekwa katika ngazi za juu kwa ushauri na maamuzi ya mwisho.

Kufanya Tafiti Mbalimbali Zinazohusiana na Maendeleo na Ukuaji wa Miji na Vijiji Nchini:

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuelewa umuhimu wa utafiti kwa maendeleo, idara inajishughulisha pia na tafiti mbalimbali kuhusu maendeleo ya miji na matumizi bora ya ardhi. Idara imekiimarisha kitengo cha uwekaji kumbukumbu pamoja na kuwapeleka baadhi ya wafanyakazi masomoni kupata mafunzo yatakayowasaidia katika utendaji wa kazi zao ukiwemo utafiti.

Aidha, idara katika mwaka wa fedha 2011/2012 imepokea wanafunzi kutoka vyuo mbalimbali duniani ambao walikuja nchini kufanya tafiti zao za kukamilisha masomo yao. Idara huwaunganisha wanafunzi hao na wafanyakazi wetu ili kubadilishana ujuzi na uzoefu baina yao.

Mradi wa Uimarishaji wa Mji wa Zanzibar (*ZUSP*):

Mhe. Mwenyekiti, mbali ya kazi hizo za kawaida, idara hii pia inahusika katika utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji wa Mji wa Zanzibar (*Zanzibar Urban Service Project – ZUSP*) katika masuala yanayohusiana na kazi za Mipango Miji.

Kwa upande wa Sekta ya Ardhi, Mradi huu unatarajiwa kusaidia katika utayarishaji wa (*Master Plan*) mpya ya Mji wa Zanzibar. Hatua za kupata Kampuni itakayopewa kazi ya utayarishaji wa (*Master Plan*) hiyo zinaendelea kupitia Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kupatikana kwa *Master Plan* mpya ya Mji wa Zanzibar kutasaidia sana katika usimamizi na uendelezaji wa Mji wa Zanzibar, kwani *Master Plan* iliyopo ya mwaka 1982 imeshapitwa na wakati na haikidhi tena mahitaji ya sasa.

MALENGO:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Mipango Miji na Vijiji inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo :-

1. **Kuanzisha na kusimamia Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Ardhi Nchini (*National Spatial Developement Strategy*):**

   Katika kufanikisha Mkakati huu Idara inatarajia kufanya kazi zifuatazo:-

   a. Kutayarisha Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Ardhi Nchini (*National Spatial Developement Strategy*),
   b. Kuandaa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi katika Mji Mkuu wa Zanzibar (*Zanzibar Metropolis Master Plan*),
   c. Kuweka mipango ya kukuza miji ya Mikoani (*Regional Urban Centres* Chake-Chake, Chwaka au Mkokotoni),
   d. Kuweka Mpango wa matumizi ya sehemu za uhifadhi (*Heritage Planning Strategy*).

2. **Kudumisha na Kusimamia Mipango Endelevu ya Uendelezaji wa Miji. (*Sustainable Urban Development and Management*):**

   Katika kufanikisha lengo hili, Idara inatarajia kufanya kazi zifuatazo:

   a. Kutayarisha Sera ya Mipango ya Maendeleo ya Miji (*Urban Development Policy*),
   b. Kutayarisha miongozo ya uendelezaji wa miji pamoja na mipango mbali mbali ya uendelezaji wa maeneo ya miji (*local schemes*).

3. **Kuendeleza Mikakati ya Utayarishaji wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi katika Ngazi za Taifa, Wilaya, Vijiji na Katika Ukanda wa Maeneo ya Utalii.**

   Katika kufanikisha mpango huu idara inatarajia kufanya kazi zifuatazo:-

   a. Kuelimisha na kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi,
   b. Kuelimisha na kusimamia utekelezaji wa Mipango Mikuu ya matumizi ya ardhi ya wilaya,
   c. Kutengeneza mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji,
   d. Kuupitia Mpango Mkuu wa Utalii.

4. **Utayarishaji wa Sheria za Mipango Miji na Kanuni zake:**

Katika kufanikisha mpango huu, Idara inatarajia kufanya kazi zifuatazo:-

a. Kuifanyia mapitio Sheria ya Mipango Miji na Vijiji ya mwaka 1955,
b. Kutayarisha Kanuni na Miongozo mbalimbali inayohusiana na kazi za upangaji wa miji na vijiji nchini, (*Planning Policy Guideline –PPG*),
c. Kukamilisha hatua za kuifanyia mabadiliko *UDCA*.

5. Kuijengea Uwezo Idara Kitaaluma, ili Iweze Kukabiliana na Kazi Zake Mbalimbali Zikiwemo za Utafiti na Kazi za Kawaida:

Katika kufanikisha mpango huu, idara inatarajia kufanya kazi zifuatazo:-

a. Kusomesha wafanyakazi 5 katika ngazi ya digirii ya kwanza, wafanyakazi 3 kwa ngazi ya digrii ya pili na wafanyakazi angalau 4 katika ngazi ya cheti na diploma katika fani za Mipango miji, usanifu majengo, *computer science*, uwekaji kumbukumbu na kadhalika.
b. Kukiimarisha kitengo cha kumbukumbu.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Mipango Miji na Vijiji iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 293,000,000/= kwa ajili ya kazi za kawaida.

IDARA YA UPIMAJI NA RAMANI:
UTEKELEZAJI:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Upimaji na Ramani ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

Kushirikiana na Idara ya Mipango Miji na Vijiji Katika Kutayarisha Mpango Bora wa Upimaji Viwanja Vya Makaazi, Huduma, Biashara na Uwekezaji:

Mhe. Mwenyekiti, idara imepima viwanja 303. Kati ya hivyo, Viwanja 154 kwa ajili ya makaazi, 15 kwa huduma za jamii, 45 kwa taasisi za serikali, maeneo 77 kwa kilimo na 12 kwa ajili ya vitega uchumi.

Kuendelea na Kazi za Upimaji wa Mipaka ya Wilaya na Mikoa:

Mhe. Mwenyekiti, idara imekamilisha mapitio ya awali na kufanya masahihisho (*map editing*) kwa ramani kuu za kipimo cha 1:10000. Pia imeanza kukagua mpaka wa Wilaya ya Kaskazini – A na Kaskazini – B. Upimaji mipaka ya kudumu ni kazi muhimu sana, itakayosaidia kuondosha migogoro ya mipaka ya kiutawala, ambayo imeanza kujitokeza katika maeneo mbalimbali nchini.

Kuendeleza Mapitio ya Ramani za Zanzibar:

Mhe. Mwenyekiti, utengenezaji wa ramani za visiwa vya Zanzibar (*Base Map*) una umuhimu mkubwa kwa taifa, kwani utawezesha kuwa na taarifa sahihi zitakazoleta tafsiri na utambuzi wa maeneo ya ardhi kwa madhumuni ya matumizi mbalimbali ya maendeleo kiuchumi, kijamii, kiutawala na kadhalika.

Kazi hii ni endelevu na inafanywa kupitia mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Uhifadhi wa Mazingira (*SMOLE*).

Kuendeleza Utayarishaji Ramani za Kawaida Kwa Ajili ya Utoaji wa Hati Mbalimbali za Ardhi Pamoja na Uwekaji Kumbukumbu. (*Cadastral Maps, Site Plans*):

Mhe. Mwenyekiti, idara imeendeleza uchoraji ramani za kiupimaji na za mipaka ya maeneo kwa ajili ya kutoa hati mbalimbali za Matumizi ya Ardhi. Hadi kufikia Machi 2012, uchoraji ramani mpya 303 za kutolea hati "*Site Plan*" ulikwishakamilika na "*Site Plans*" 26 za zamani zimefanyiwa marekebisho.

Kuendeleza Utunzaji Kumbukumbu za Ramani na Taarifa Mbali mbali za Ardhi Kupitia Kitengo cha *ZALIS*:

Mhe. Mwenyekiti, idara imeanza kuweka taarifa za Upimaji na kumbukumbu za ramani katika Kompyuta, "*CD*, *DVD* na *Ext-HD*" kwa maeneo yote yaliyopimwa rasmi. Changamoto iliyopo ni maeneo mengi nchini kuendelezwa bila ya kupimwa kwa mujibu wa taratibu. Kwa kutumia mfumo huu, idara imeanza kuweka pamoja taarifa za maeneo ambayo yanahitaji kupimwa rasmi.

Kuendelea na Ukusanyaji na Utunzaji wa Taarifa za Kupwa na Kujaa Kwa Maji ya Bahari:

Mhe. Mwenyekiti, kazi hii ni miongoni mwa kazi zinazoendelezwa na idara kwa mashirikiano makubwa na Chuo kikuu cha Hawaii. Hadi kufikia Machi 2012, taarifa zote za kupwa na kujaa kwa maji ya bahari zilipatikana kwa mwaka mzima.

Utekelezaji wa Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Uhifadhi wa Mazingira (*SMOLE*).

Mhe. Mwenyekiti, awamu ya pili ya mradi huu (*SMOLE II*) imeanza Januari, 2010 na itakamilika 2013, kwa ushirikiano na Serikali ya Finland.
Lengo kuu la mradi ni kuipunguzia jamii umasikini kupitia usimamizi mzuri wa rasilimali ardhi kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya 2020, na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA II).

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2011/2012, mradi huu ulitekelezwa na Idara tano za Wizara tatu za SMZ ambazo ni Wizara ya Kilimo na Mali Asili, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na Wizara yangu. Msimamizi mkuu wa shughuli za wizara yangu ni Idara ya Upimaji na Ramani.
Mhe. Mwenyekiti, kazi zilizofanywa na mradi huu kwa wizara yangu ni kama ifuatavyo:-

i. Kuchangia baadhi ya gharama za utekelezaji wa kazi za Idara kama Upimaji wa viwanja katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba.
ii. Kuendeleza uwekaji wa kumbukumbu za taarifa za ardhi (*Land Information*) na Kumbukumbu za milki za ardhi kwa madhumuni ya usajili wa ardhi (*Land Registration*) na uhifadhi wa kumbukumbu za Mazingira (*Environmental Information*).
iii. Kugharamia ununuzi wa vifaa vya ofisi vya Idara hizi kama vile kompyuta, gari za kufanyia kazi, vifaa vya upimaji ardhi na vifaa vya uchunguzi wa mambo ya mazingira.
iv. Kuandaa Mpango Mkakati wa Upashaji Habari wa kutoa elimu kwa wananchi katika matumizi ya ardhi, uhifadhi wa mazingira kwa kuandaa semina na kutumia vyombo vya habari –TV, Radio na Magazeti.
v. Kuendeleza tafiti mbalimbali za usimamizi wa ardhi na uhifadhi wa mazingira, ambazo matokeo yake yatatumika katika kuandaa Sera mpya ya Ardhi nchini itakayosaidia usimamizi na matumizi bora ya ardhi.
vi. Wafanyakazi wa idara hizi wanaendelea kupatiwa mafunzo ya ndani katika kazi za utayarishaji ramani, utumiaji wa vifaa

mbalimbali vya kisasa vinavyotumika katika kazi za upimaji wa ardhi.

vii. Kusaidia uanzishwaji wa Afisi ya Msajili wa Ardhi Pemba pamoja na kuanzishwa kwa uhakiki ardhi (*land adjudication*).

viii. Uhakiki wa eka tatu kwa Unguja unaendelea katika kuandaa *Data base*.

ix. Kusaidia kuandaa mpango na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu nchini Tanzania wafanyakazi wa idara hizi.

MALENGO:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara hii ya Upimaji na Ramani inakusudia kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kushirikiana na Idara nyengine za Ardhi na taasisi mbalimbali katika kupima maeneo yaliyopangwa.

ii. Kuweka na kupima mipaka ya Wilaya na Mikoa, Unguja na Pemba.

iii. Kuendelea kuzifanyia mapitio ramani za Zanzibar kila inapohitajika.

iv. Kuendeleza utunzaji wa kumbukumbu za ramani na taarifa mbalimbali za ardhi kupitia Kitengo cha *ZALIS*.

v. Kuendelea na ukusanyaji na utunzaji wa taarifa za kupwa na kujaa kwa maji ya bahari kupitia kituo chetu kilichopo katika Bandari ya Malindi Zanzibar pamoja na matumizi ya Alama Kuu ya Upimaji iliyopo Mbweni.

Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Uhifadhi wa Mazingira (*SMOLE*):

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013 mradi huu unakusudia kutekeleza kazi zifuatazo:-

1. Kuendeleza uwekaji wa kumbukumbu za taarifa za ardhi (*Land Information*) na Kumbukumbu za milki za ardhi kwa madhumuni ya usajili wa ardhi (*Land Registration*) na uhifadhi wa kumbukumbu za Mazingira (*Environmental Information*) za Unguja na Pemba.
2. Kugharamia ununuzi wa vifaa vya ofisi vya Idara hizi kama vile kompyuta, gari za kufanyia kazi, vifaa vya upimaji ardhi na vifaa vya uchunguzi wa mambo ya mazingira.

3. Kutoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi bora ya ardhi na uhifadhi wa mazingira kwa kuandaa semina na kutumia vyombo vya habari –TV, Radio na Magazeti.
4. Kuendeleza tafiti mbalimbali za usimamizi wa ardhi na uhifadhi wa mazingira, ambazo matokeo yake yatatumika katika kuandaa sera mpya ya ardhi nchini itakayosaidia katika usimamizi na matumizi bora na endelevu ya ardhi.
5. Kuwapatia wafanyakazi wa idara mafunzo ya ndani katika fani za utayarishaji ramani, utumiaji wa vifaa mbalimbali vya kisasa vinavyotumika katika kazi za upimaji wa ardhi.
6. Kuendeleza zoezi la kumtambua mwenye haki ya matumizi ya ardhi Unguja na Pemba (*land adjudication*).
7. Kuandaa mpango na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu nchini Tanzania wafanyakazi wa dara hizi.

Mhe. Mwenyekiti, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya shilingi 358,000,000/= kwa ajili ya kazi za kawaida, na shilingi 170,000,000/= kwa ajili ya kazi za maendeleo katika Idara ya Upimaji na Ramani.

IDARA YA UJENZI:
UTEKELEZAJI:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara imetekeleza yafuatayo:-

Ujenzi wa Nyumba ya Maendeleo Mpapa:

Idara imekamilisha kazi muhimu zifuatazo:-

a. Upigaji wa plasta nje na ndani,
b. Uwekaji sakafu ya jengo zima,
c. Uwekaji wa fremu za milango na madirisha,
d. Ujenzi wa mashimo ya karo pamoja na chemba (*drainage*).

Bodi ya Kusajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo:
Mhe. Mwenyekiti, bodi hii inaendelea na kusajili na uratibu wa shughuli za Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo. Hadi kufikia mwezi Machi 2012, Bodi imeweza kusajili Wataalamu kama inavyoonekana katika Jaduweli ifuatayo:-

Jaduweli nambari 2

Na.	AINA YA WATAALAMU	IDADI
1	Wasanifu Majengo (Professional Architects)	12
2	Wasanifu Majengo (Graduates Architects)	3
3	Wahandisi (Professional Engineers)	26
4	Wahandisi (Graduates Engineers)	8
5	Wakadiriaji Ujenzi (Quantity Surveyors)	8
6	Kampuni za Uhandisi (Engineering Firms)	1
7	Kampuni za Usanifu Majengo (Architectural Firms)	3
8	Kampuni za Ukadiriaji Ujenzi (Quantity Surveyors Firms)	1
9	Wasanifu Wataalamu wa Muda (Temporary Professional Engineers)	7
10	Wakadiriaji Ujenzi wa Muda (Temporary Quantity Surveyors)	1
11	Wenye Vyeti vya Ufundi (Civil Engineering Technician (FTC/NTA4)	3
JUMLA		**73**

Bodi ya Kusajili Wakandarasi:
Mhe. Mwenyekiti, Bodi hii kwa mwaka wa fedha 2011/2012 imetekeleza yafuatayo:-

i. Kufungua Tawi la Bodi Pemba.
ii. Kufanya semina kwa wadau mbalimbali Unguja na Pemba kwa lengo la kujitambulisha na kuwashajiisha Wakandarasi kujisajili nchini.
iii. Kuunda Kikosi cha Wataalamu wa Ukaguzi kwenye sehemu za ujenzi.

Hadi kufikia mwezi wa Machi 2012, Bodi imesajili wakandarasi 20, wakiwemo watano wa kigeni na kumi na tano wazalendo.

MALENGO:
Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 idara inakusudia kutekeleza kazi zifuatazo:-

1. Kuendeleza ujenzi wa fleti 24 za Mpapa.
2. Kubuni Miradi ya Ujenzi wa Nyumba Mpya za Makaazi kwa Unguja na Pemba, ili kusaidia upatikanaji wa makaazi bora na nafuu kwa wananchi.
3. Kushirikiana na Idara mbalimbali kama vile Idara ya Ardhi na Usajili, Idara ya Mipango Miji na kadhalika, kuangalia maeneo bora kwa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi, kwa ajili ya kutekeleza Miradi mbalimbali ya ujenzi wa Nyumba za makaazi.

4. Kuendelea Kuziimarisha na kuzijengea uwezo wa kiutaalamu Bodi ya kusajili Wakandarasi (*Zanzibar Contractors Registration Board - ZCRB*) na kusajili Wataalamu wa Ujenzi (*Architects, Engineers and Quantity Surveyors Registration Board - AEQSRB*).
5. Kuviimarisha na Kuongeza Vyanzo vya Mapato ya Serikali kwa:-
    a. Kutoa huduma za Ushauri Elekezi kwenye Sekta ya Ujenzi (*Consultancy Services*) kwa Taasisi za Serikali na Watu Binafsi.
    b. Kufanya kazi za Ujenzi (*Construction Works*) kwa Majengo ya Taasisi mbalimbali za Serikali na za watu Binafsi.
    c. Kuimarisha Kiwanda cha Uchongaji cha Saateni (Saateni *Workshop*) kwa kufanya kazi mbalimbali kama Uchongaji wa Milango na Madirisha pamoja na Samani mbalimbali za Serikali na Watu Binafsi.
    d. Kuimarisha Kiwanda cha Kusaga Kokoto kilichopo Makunduchi.
6. Kuwapatia Mafuzo mbalimbali ya muda mfupi wafanyakazi wake pamoja na semina ndani na nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Ujenzi iweze kutekeleza malengo yake kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 622,000,000/= kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 100,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAAZI:

UTEKELEZAJI:
Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 idara iliweza kusimamia na kutekeleza mambo yafuatayo:

Mapendekezo ya Marekebisho ya Kodi Mpya za Nyumba za Serikali:
Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo ya kodi mpya za Nyumba za Serikali tayari yameshatayarishwa. Kazi inayofanyika hivi sasa ni kuyafanyia mapitio, ili hatimae yaweze kufikishwa katika vikao vya juu.

Kuandaa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Nyumba:
Mhe. Mwenyekiti, hatua za awali za utayarishaji wa Rasimu ya Sheria ya uanzishaji wa Shirika la Nyumba Zanzibar zimeanza kuchukuliwa. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2012, jumla ya *section* 21 zimeshatayarishwa kati ya *section* 42 zinazotarajiwa kuwemo katika Sheria hiyo. Sheria hiyo inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha wa 2012/2013.

Kuwashajiisha Wawekezaji Kwa Ajili ya Ujenzi wa Nyumba za Makaazi:
Mhe. Mwenyekiti, Mazungumzo yameendelea kufanyika na Wawekezaji mbalimbali kama vile *TECHNO GROUP* ya Dubai, *People's Home* ya Ujerumani, *Chonging* ya Uchina kwa lengo la kufikia makubaliano ya kuwezesha kujenga Nyumba za Makaazi katika maeneo mbalimbali kama vile Maeneo ya *EPZ* Unguja na Pemba, ambayo ni Fumba na Maziwa Ng'ombe na pia maeneo ya Chuini na Binguni.

Matengenezo ya Nyumba za Serikali:

Mhe. Mwenyekiti, matengenezo madogo madogo yameendelea kufanyika katika Nyumba za Maendeleo za Michenzani, Mombasa na Kikwajuni kwa Unguja na Mkoani, Wete na Chake Chake kwa Pemba.
Matengenezo hayo yalihusisha ubadilishaji wa mabomba yaliyochakaa ya mfumo wa maji machafu na kuweka mapya na pia usafishaji wa karo ndogo na kubwa za maji machafu.

Kamati ya Kuwatambua Wanaodai Kupewa Nyumba na Marehemu Mzee Karume:

Mhe. Mwenyekiti, ripoti iliyokuwa ikisubiriwa, ili kujua hatma ya Wananchi wanaodai kupewa nyumba na Marehemu Mzee Karume, tayari imekabidhiwa Wizarani na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi na hivi sasa ripoti hiyo inapelekwa serikalini, ili kuweza kupata maelekezo juu ya hatua za kufaa kuhusiana na suala hili. *(Makofi)*
Ni mategemeo yetu kuwa ufumbuzi wa kudumu utapatikana kwa wale wananchi wanaodai kupewa nyumba na Marehemu Mzee Karume.

Kudhibiti Kodi za Nyumba:

Mhe. Mwenyekiti, Bodi imeendelea kupokea, kusikiliza na kuyatolea maamuzi mashauri mbalimbali yaliyowasilishwa katika Bodi. Hadi kufikia Machi, 2012 mashauri 35 yamewasilishwa katika Bodi na kati ya hayo mashauri 8 yametolewa uamuzi.

MALENGO:
Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, idara inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea na utayarishaji wa Rasimu ya Sheria ya uanzishaji wa Shirika la Nyumba.

ii. Kuendelea kuzifanyia matengenezo Nyumba za Serikali.

iii. Kuendelea kuwashajiisha wawekezaji kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba za Makaazi.

iv. Kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na kodi za nyumba za serikali.

v. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwaendeleza kimasomo.

Mhe. Spika, ili Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 269,000,000/= kwa ajili ya kazi za kawaida.

MAMLAKA YA HIFADHI NA UENDELEZAJI MJI MKONGWE: UTEKELEZAJI:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Mamlaka ilitekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

Kuendelea Kutoa Ushauri wa Kitaalamu na Kusimamia Miradi ya Uhifadhi wa Majengo:

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka imepokea maombi ya kusimamia na kufanya matengenezo ya majengo ya Ikulu na Baraza la Mapinduzi (BLM), Skuli za Benbella, Forodhani na Tumekuja na kufanya matengenezo ya Daraja ndogo mbele ya Mnara mmoja ndani ya jengo la Ngome Kongwe.

Aidha Mamlaka imeshatayarisha makisio ya gharama za matengenezo ya ufa mkubwa, ukuta ulioharibika na boriti zilizooza za Afisi ya Askofu wa Kanisa la Mkunazini. Kwa sasa mamlaka yanasubiri fedha kutoka kwa uongozi wa Kanisa hili kuendelea kufanya kazi husika.

Aidha wafanyakazi wanne wa mamlaka (mafundi watatu wakiongozwa na mkuu wa kitengo cha ufundi) walikwenda Comoro kuanzia Septemba hadi Novemba 2011 kwa ajili ya matengenezo ya jengo la Kihistoria Mutsamudu - Comoro kwa hatua za awali na kwa sasa wanasubiri matayarisho ya awamu ya pili yakamilike ili waendelee na kazi hiyo.

Ushiriki wa Mamlaka Katika Mikutano ya Kihistoria na Urithi wa Kidunia

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Mji Mkongwe iliendesha mkutano unaohusiana na muonekano wa miji ya kihistoria *(historical urban land scape)* kwa kushirikiana na kituo cha Urithi wa Kimataifa cha UNESCO *(World Heritage Centre).* Mkutano huo ulijadili changamoto mbali mbali zinazoikabili Miji ya Urithi wa Dunia ukiwemo Mji Mkongwe wa Zanzibar na kuangalia mbinu zitakazosaidia kukabiliana na changamoto hizo kwa madhumuni ya kuitunza na kuihifadhi.

Ripoti hizo zimeshawasilishwa UNESCO kwa kuunganishwa na ripoti za miji mengine, kwa madhumuni ya kuandaa waraka mmoja wa kufanyia kazi za kiuhifadhi kwa miji yetu. Vile vile Mamlaka ilishiriki Mkutano wa Umoja wa Miji ya Urithi wa Dunia uliofanyika Mjini Sintra nchini Ureno (Portugal).

Ubadilishaji wa Milango ya Chuma ndani ya Mji Mkongwe

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ilifanya zoezi la kuwahamasisha na kuwaelimisha wamiliki wa majengo mbali mbali ndani ya Mji Mkongwe namna bora ya kuweka milango ya chuma majumbani mwao bila ya kuathiri haiba ya Mji Mkongwe. Wananchi wengi wamefanya mabadiliko hayo, ingawa baadhi wamekuwa wagumu kwa kuhofia gharama.

Sherehe za Mshikamano kwa Miji ya Urithi wa Dunia.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka iliadhimisha siku ya Mshikamano kwa miji ya Urithi wa Dunia tarehe 08 Septemba 2011, katika sherehe hiyo, wanafunzi walishiriki Mashindano ya Uchoraji Majengo ya Kihistoria ya Mji Mkongwe *(Story Body Competition)* na kazi zao kuwasilishwa UNESCO. Wanafunzi wanne wa Zanzibar walifanikiwa kushinda na walikabidhiwa vyeti siku ya sherehe hiyo.

Kuendeleza Mashirikiano na Vyuo Pamoja na Taasisi za Nje ya Nchi.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka imepokea wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha *Pretoria* wakiongozwa na walimu wao wawili waliofika kwa awamu tofauti kuja kufanya mafunzo yao kwa vitendo katika fani za uhifadhi kwa kushirikiana na wafanyakazi wa Mamlaka. Wanafunzi hao walijikita zaidi katika uimarishaji wa maeneo ya wazi pamoja na uhifadhi wa majengo ndani ya Mji Mkongwe, eneo kubwa la Malindi limefanyiwa kazi kwa asilimia 80 kwa kutayarishiwa ramani kwa matumizi yanayohitajika.

Kudhibiti Ujenzi.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka katika kuulinda na kuuhifadhi Mji Mkongwe ili ubaki katika hadhi yake ya urithi wa asili, imekuwa ikitoa vibali kwa kufanya matengenezo makubwa na madogo pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria wanaokwenda kinyume na taratibu zilizowekwa. Kwa ufafanuzi zaidi naomba muangalie kiambatanisho "**D".**

Kusimamia Utaratibu wa Kupunguza Msongamano wa Vyombo Mbali mbali Ndani ya Mji Mkongwe "*TRAFFIC PLAN"*

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa suala hili haukufanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na watu kutohamasika na pia kukosa mashirikiano yaliyo mazuri kutoka kwa baadhi ya wadau husika, ukubwa wa tatizo hili zaidi unatokana na kuwepo kwa bandari ya Forodha Mchanga ambayo husababisha msongamano wa magari makubwa yanayokuja kuleta au kuchukua mizigo.

Aidha sehemu ya kuteremkia abiria *(passenger terminal)* nayo husababisha msongamano wa magari nyakati za kuondoka ama kufika kwa boti. Mamlaka kwa upande wake itaendelea na jitihada zake za kulipatia ufumbuzi tatizo hili.

Mradi wa Ujenzi wa Ukuta wa Ukingo Wa Bahari.
Mhe. Mwenyekiti, Benki ya Dunia tayari imeshawakubali washauri waelekezi *"Aurecon and Planning Partners"* waliopendekezwa. Mamlaka tayari imepokea barua ya uthibitisho pamoja na kuwasilisha Hadudi Rejea *(ToR)* Benki ya Dunia kwa kuangaliwa na kupata maoni yao.

<u>Malengo</u>

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu.

ii. Kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo vya habari juu ya Umuhimu wa kuuhifadhi Mji Mkongwe wa Zanzibar kama ni urithi wa Dunia.

iii. Kuimarisha, kusimamia na kutunza Mandhari ya maeneo ya wazi kwa matumizi mbali mbali ya jamii ili yawe kivutio kwa wageni na wenyeji.

iv. Kuchukua hatua za hadhari kwa kuyahami majengo yaliyo katika hali mbaya ya kuanguka.

v. Kuendeleza kutoa ushauri wa kitaalamu na kusimamia miradi ya Uhifadhi wa majengo.

vi. Kuendelea na usimamizi wa ujenzi wa ukuta wa Ukingo wa bahari ya Forodhani.

vii. Kuandaa maadhimisho ya siku mashuhuri za kimataifa kama vile siku ya Urithi Duniani na siku ya Mshikamano kwa Miji ya Urithi wa Kimataifa.

viii. Kuendeleza mashirikiano na vyuo vikuu, pamoja na taasisi za ndani na nje ya nchi.

ix. Kuendelea na utaratibu wa kupunguza msongamano wa vyombo mbali mbali katika njia za Mji Mkongwe *(Traffic Plan).*

x. Kuhakikisha kwamba Mji Mkongwe wa Zanzibar unabaki katika Orodha ya Urithi wa Dunia.

Mhe. Mwenyekiti, ili Mamlaka iweze kutekeleza malengo yake katika Mwaka wa Fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Tsh. 330,000,000 kwa ajili ya kazi za kawaida.

MAMLAYA YA MAJI

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, Maji ni rasilimali muhimu kwa maisha ya wanaadamu na viumbe wote. Azma ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wote inaendelea kutekelezwa. Lengo ni kuwawezesha wananchi kupata huduma hiyo muhimu muda wote kwa gharama nafuu na kwa masafa mafupi kadri iwezekanavyo ifikapo mwaka 2015 ambao ni utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020 (Vision 2020), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA II) na Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs).

Mhe. Mwenyekiti, mahitaji ya maji yanazidi kukuwa kutokana na kutanuka kwa maeneo ya miji na kuimarika kwa maeneo ya vijijini. Aidha, mabadiliko ya tabianchi, uvamizi wa vianzio vya maji, uchakavu wa miundo mbinu ya maji, mwitikio mdogo wa wananchi katika kuchangia huduma ya maji vinaipa changamoto kubwa Wizara yangu katika utekelezaji wa malengo hayo.

Licha ya changamoto hizo serikali kupitia Wizara yangu ilifanya jitihada mbalimbali kwa kutumia uwezo wake wa ndani na misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na nguvu za wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 Mamlaka ya Maji ilijipangia kutekeleza mambo yafuatayo:-

Usambazaji wa Maji Vijijini
Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ina Programu endelevu ya usambazaji wa maji katika maeneo ya vijijini Unguja na Pemba. Programu hii imegawika kwenye miradi midogo midogo katika maeneo yasiyo na huduma nzuri au yaliyoshindwa kukamilishwa ujenzi wake katika mwaka wa fedha uliopita. Kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 Mamlaka imetekeleza programu hii kama kiambatanisho **"E"** kinavyoonesha.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka pia inashirikiana na Jumuiya ya *Ivo de Carneri Foundation (IdCF)* katika kuimarisha huduma za maji hapa Zanzibar kupitia Mradi wa Maji unaoitwa *"SAFE WATER PROJECT PHASE III*" unaojumuisha maeneo mawili makuu.

Eneo la kwanza ni uimarishaji wa miundombinu ya maji ambapo kwa mwaka wa fedha 2011/2012 jumuiya hiyo imesaidia kuimarisha mtandao wa maji katika kisiwa cha Kojani Pemba. Miongoni mwa kazi zinazoendelea ni uchimbaji wa kisima, ujenzi wa kituo, ulazaji wa mabomba ya inchi 5 na 4, utengenezaji wa nanga za kuzuwilia mabomba eneo la baharini, kujenga uzio pamoja na kununua pampu.

Eneo la pili ni uimarishaji wa huduma za uchunguzi wa ubora wa maji yanayozalishwa na Mamlaka ya Maji Zanzibar katika Wilaya zote za Pemba. Kazi hizi zinafanywa kwa mashirikiano ya pamoja na watendaji wa Maabara ya Afya ya Jamii iliyopo Wawi Chake Chake Pemba.

Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini
Mhe. Mwenyekiti, sambamba na kukamilika Mradi wa Maji wa Mkoa wa Mjini Magharibi chini ya ufadhili wa Serikali ya Japan katika Mwaka huu wa Fedha Wizara kupitia Mamlaka ya Maji inaendelea na utekelezaji wa miradi midogo midogo kwa ulazaji wa mabomba mapya, uchimbaji wa visima, ununuzi na utiaji wa pampu mpya, ujenzi wa vituo na upelekaji wa umeme katika maeneo ya miradi. Aidha, kati ya visima tisa vilivyolengwa, vinne tayari vilikwishachimbwa hadi kufikia Machi 2012. Kwa ufafanuzi zaidi wa utekelezaji ni kama inavyoonekana katika Jaduweli ifuatayo:

Jaduweli Nambari 3

Eneo	Kazi iliyofanyika
Kinuni, Kijichi, Magomeni, Mpendae, Chuini, Kihinani,	Ununuzi na Ulazaji wa mabomba.
Kianga N9-2 na Mwembe Mchomeke na Chunga	Ununuzi na Ufungaji wa pampu/Mota.
Chumbuni (3), Saateni pumping Station na Sebleni,	Uchimbaji wa visima.
Mombasa, Kijito Upele, Koani na Afisi kuu.	Ujenzi wa vituo vya makusanyo ya mauzo ya maji pamoja na huduma kwa wateja.

Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji Awamu ya Pili.

Mhe. Mwenyekiti, Mradi huu unaofadhiliwa na Serikali ya Japan (JICA) unalenga kuijengea uwezo ZAWA Kiutendaji ili watendaji wake wamudu majukumu yao ipasavyo. Mradi unawapatia wafanyakazi mafunzo ya muda mfupi ya ndani na nje ya nchi, kutoa misaada ya vitendea kazi kama vile gari na ufungaji wa mita za maji.

Hadi kufikia Machi 2012, kazi zilizofanyika ni uhakiki wa maeneo ya majaribio *(pilot areas)* ya mradi huo, kufanya uhakiki wa wateja wa Biashara na kufanya taratibu za manunuzi ya mita kwa wateja wa Majumbani.

Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2012, Mradi wa Usambazaji Maji Safi na Usafi wa Mazingira unaotekelezwa kwa mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika na ruzuku ya Shirika la Makaazi Duniani la UN- HABITAT utakaohudumia vijiji 9 vya Unguja na Pemba na miji 3 ya Pemba ulikuwa katika hatua ya kupokea taarifa za ujenzi kutoka kwa washauri waelekezi. Pia kuendelea na tathmini ya mazao katika eneo la Mradi kwa ajili ya fidia.

Aidha, mradi umehusika na kutoa zabuni kwa wakandarasi pamoja na kufanya tathmini ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa vyoo kwa ajili ya shughuli za usafi wa mazingira katika skuli za Pemba Mijini. Shughuli nyengine zilizofanyika ni kutangaza zabuni na kufanya tathmini ya kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya uhifadhi na utunzaji wa rasilimali maji.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka imeshapata Mshauri Mwelekezi wa Kampuni ya NIRAS ya Denmark katika kuijengea uwezo ZAWA. Wataalamu hawa tayari wameshahakiki maeneo ya majaribio *(Pilot areas),* kuupitia muundo wa Mamlaka ya Maji kiutendaji *(Organization structure)* na kuvifanyia mapitio viwango vya ulipaji wa huduma ya maji *(water tarrifs).*

Mradi wa Kuimarisha Miundo Mbinu ya Maji na Kuijengea Uwezo Mamlaka Kifedha (Adf 12)

Mhe. Mwenyekiti, Mradi huu ni kwa ajili ya kubadilisha mabomba makongwe na kuweka mapya katika Mkoa wa Mjini Magharibi chini ya ufadhili wa Benki ya maendeleo ya Afrika (AfDB) uliotenga kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 21 katika utekelezaji wake. Hadi kufikia Machi 2012 ZAWA kwa kushirikiana na Washauri Elekezi wa Kampuni ya NIRAS ya Denmark ilikwisha kamilisha upembuzi yakinifu *(feasibility study)* wa hali ya kijamii na kiuchumi pamoja na taarifa ya mitandao ya maji.

Aidha, timu ya wataalamu kutoka AfDB tayari imekuja kwa kuainisha maeneo yaliyopangwa kwa mradi huo na hatua inayofata ni kufanya tathmini ya Mradi na hatimaye kusaini mkataba wa utekelezaji.

Kuvilinda na Kuviwekea Uzio Vianzio Vya Maji

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na ongezeko la uvamizi wa maeneo ya vianzio vya maji, ZAWA inalisimamia na kulifuatilia kwa karibu suala la kuvilinda na kuvitunza vianzio vya maji ikiwa ni miongoni mwa majukumu yake ya msingi. Mamlaka ya Maji tayari imeshalipatia hati miliki eneo la Mtoni, imeshafanya ukaguzi na kuyapima maeneo ya Bonde la Nyakurungwi, Kijitoupele, Kwarara, Shakani, Dimani na Mwanyanya. Hatua inayofuata ni upimaji wa maeneo hayo.

Aidha, Mamlaka imeshaweka uzio katika vyanzo na vituo vya maji vya Tangi la Kizimkazi, Gongoni na Ziwani pamoja na visima vya Selem, Kituo cha Maji Saateni na Kianga.

KAZI ZA KAWAIDA

Mafunzo kwa Wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake kwa kuzingatia fani na viwango mbali mbali, hadi kufikia Machi 2012, ZAWA imewapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika vyuo na fani mbali mbali wafanyakazi 12, ndani na nje ya nchi.

Matengenezo

Mhe. Mwenyekiti, Katika kipindi hichi Mamlaka imeendelea na kazi zake za kawaida za matengenezo mbali mbali kwa maeneo tofauti kama yanavyoonekana katika kiambatanisho **“F”**

Ukusanyaji wa Mapato

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2012 Mamlaka ilijipangia kukusanya Tsh. **Bilioni 3.06** kutokana na mauzo ya maji na mauzo mengineyo. Hadi kufikia Machi 2012, Mamlaka imekusanya jumla ya Tsh. Bilioni 1.04 ambazo ni sawa na asilimia 34 tu ya makadirio.

Mhe. Mwenyekiti, licha ya kuwapa Wananchi taaluma ya kutosha kuhusu kuchangia gharama za huduma ya maji, bado mwamko ni mdogo, hivyo tunawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wawe Mabalozi wetu katika kuwashajiisha Wananchi kuchangia gharama za maji hapa nchini.

Malengo

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 imepanga kutekeleza miradi ifuatayo:-

Usambazaji wa Maji Vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu inatarajia kuendelea na mradi unaofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ambayo inatarajia kuchangia jumla ya Dola za Kimarekani **Milioni 1.5** kwa kazi za uchimbaji wa visima zaidi ya 30 Vijijini Unguja na Pemba, ujenzi wa matangi, utiaji pampu na ulazaji wa mabomba ya inchi 6 na 4.

Aidha, Mamlaka imepanga kutekeleza miradi mbali mbali ambayo ujenzi wake haukukamilika, pamoja na kutanua huduma hiyo kwa maeneo ambayo huduma hii haijafika. Maeneo hayo ni pamoja na Mtende, Muyuni, Tumbatu, Bandamaji, Miwani, Fuoni, Kidoti, Kibuteni-Makunduchi, Cheju, Kinduni, Mfenesini Bumbwini, Kilindi, Matuleni, Muambe, Shumbaviamboni, Wingwi Mtemani, Wingwi Mjanaza na Mtambwe Kaskazini. Wizara yangu inaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **Tsh Milioni 600** kwa ajili ya utekelezeji wa mradi huu.

Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na uchakavu wa miundo mbinu ya usambazaji wa maji katika maeneo mengi ya Mjini, Wizara inatarajia kuendeleza kutanua huduma ya maji katika maeneo yasiyo na huduma nzuri, ulazaji wa mabomba mapya, uchimbaji wa visima, ununuzi na uingizaji wa pampu mpya katika maeneo ya mradi huu na kuimarisha mitandao. Wizara yangu inaomba kuidhinishiwa jumla ya Tsh milioni 700 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu.

Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira.

109. Mhe. Mwenyekiti, Mradi huu ni kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa maeneo ya Nungwi, Matemwe, Machui na Dunga Tunguu kwa Unguja na Ndagoni, Mizingani, Wambaa, Kambini-Mchangamdogo na Vitongoji kwa Pemba. Aidha, katika maeneo ya miji, mradi unatekelezwa kwa ajili ya kuhudumia wakaazi wa maeneo ya Chake Chake, Mkoani na Wete. Katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 Wizara yangu inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Tsh Bilioni 2.6** ukiwa ni mchango wa Serikali katika ujenzi wa Mradi huo.

Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji Awamu ya Pili

110. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokwishaeleza, Mradi huu unaofadhiliwa na Serikali ya Japan (JICA) unalenga kuijengea uwezo Mamlaka ili watendaji wamudu majukumu yao ipasavyo.

Mradi wa Kuimarisha Miundo Mbinu ya Maji na Kuijengea Uwezo Mamlaka Kifedha (Adf 12).

111. Mhe. Mwenyekiti, Mradi huu ambao ni mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) unalenga kuimarisha miundombinu ya maji na kuijengea uwezo Mamlaka kifedha. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 hatua inayotarajia kuendelea ni utayarishaji taarifa ya kusaini utaratibu wa uendelezaji wa miundombinu ya maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mapato na Matumizi

112. Mhe. Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 ZAWA inatarajia kukusanya **Tsh**. **Bilioni 3.8** kutokana na shughuli za mauzo ya maji na mapato mengineyo.

Kwa upande wa matumizi, Mamlaka ya Maji inatarajia kutumia **Tsh Bilioni 5.8** kwa kazi za kawaida ikiwemo mishahara na maposho, na **Tsh Bilioni 3.9** kwa kazi za maendeleo. Hivyo kufanya jumla ya makadirio ya matumizi yote ya Mwaka wa Fedha 2012/2013 kufikia **Tsh. Bilioni 9.7.**

Uchangiaji wa Huduma ya Maji

113. Mhe. Mwenyekiti, katika kutoa elimu kwa wananchi Mamlaka ya Maji inatarajia kuelekeza nguvu zake zaidi katika kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuchangia huduma ya maji na kutoa taaluma kwa wananchi juu ya uhifadhi na ulinzi wa miundo mbinu ya maji sambamba na vyanzo vya Maji nchini.

IDARA YA NISHATI NA MADINI

UTEKELEZAJI

114. Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara ya Nishati na Madini ilisimamia na kutekeleza mambo yafuatayo:-

Utekelezaji wa Mpango wa Sera ya Nishati ya Zanzibar

115. Mhe. Mwenyekiti, Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Nishati **"** *Implementation Plan of Energy Policy***"** unaotekelezwa chini ya ufadhili wa **Sida** umeshindwa kuanza kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 kutokana na **Sida** kuanzisha utaratibu mpya wa kusaidia miradi ya maendeleo mbalimbali duniani ambao utaongoza utekelezaji wa miradi hio. Mazungumzo na **Sida** yamefanyika hivi karibuni ili mradi huo uanze katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 baada ya kukamilika kwa utaratibu huo mpya.

Pamoja na mambo mengine, awamu ya pili ya mradi wa **Sida** itatoa fursa ya elimu *(Awareness Compaign)* kwa wananchi juu ya matumizi bora ya nishati *(Energy Efficiency).* Mradi pia utaandaa Rasimu ya Sheria ya Nishati ya Zanzibar *(Draft of Zanzibar Energy Act)* pamoja na kukusanya takwimu za matumizi ya Nishati nchini *(Energy Statistics Data Base).*

Kuendelea Kufuatilia Upatikanaji wa Bidhaa ya Petroli Nchini (Dizeli, Petroli na Mafuta ya taa).

116. Mhe. Mwenyekiti, Nishati ya mafuta kwa ujumla imeendelea kupatikana kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 ingawa kumekuwa na changamoto katika siku za karibuni kwa baadhi ya Makampuni kutokutoa huduma ipasavyo kwa kisingizio cha kutaka kupandisha bei ya bidhaa hiyo.
Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha imekuwa ikilipatia ufumbuzi suala hili kwa njia ya mazungumzo na Makampuni yanayohusika.
Idara inaendelea kufuatilia takwimu za mafuta ya petroli yanayoingia katika *Depot* za Mtoni kila wiki ili kuhakikisha nishati hiyo ipo ya kutosha hapa nchini.

Takwimu ya bidhaa hiyo ni kama zinavyoonekana katika kiambatisho **"G"**

Kuandaa Sheria ya Usambazaji Mafuta na Sheria ya Udhibiti wa Nishati (Mafuta Gesi asilia na Umeme).

117. Mhe. Mwenyekiti, kwa ajili ya kutekeleza Sera ya Nishati ya Zanzibar, Wizara inaendelea na uandaaji wa Sheria inayohusiana na usambazaji wa mafuta na bidhaa zinazohusiana na mafuta ya petroli hapa Zanzibar *(Zanzibar Petroleum Supply Act)* ili bidhaa hiyo iweze kusimamiwa na Sekta husika kwa ufanisi zaidi. Utayarishaji wa Sheria hiyo unaenda sambamba na

utayarishaji wa Sheria ya Udhibiti wa huduma ya Nishati na Maji Zanzibar *(Zanzibar Utilities Regulatory Authority - ZURA)* itakayosimamia biashara inayotokana na rasilimali ya nishati na maji kwa ufanisi zaidi.

Rasimu za Sheria zote mbili zimekamilika, na zinasubiri kuridhiwa na Kamati ya Uongozi ya Wizara.

Kuijengea uwezo Idara ya Nishati na Madini.
118. Mhe. Mwenyekiti, Wizara inaendelea kufanya juhudi ya kuwapatia Mafunzo wafanyakazi wa Idara hii ili kuweza kukabiliana na upungufu wa wataalamu wa fani ya Nishati ikiwemo ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta hapa Zanzibar.

Hata hivyo Kampuni ya Ras El Khaimah Tanzania Ltd. yenye Makao yake Makuu UAE ilikubali kugharamia mafunzo kwa Wazanzibari wenye sifa na tayari Wazanzibari 2 wanaendelea na masomo yao na wengine wanatarajiwa kwenda masomoni mara tu taratibu za safari zitakapokamilika.

Kushirikiana na Serikali ya Norway katika Utekelezaji wa kazi ya kutathmini Mazingira ya Zanzibar.

119. Mhe. Mwenyekiti, Tathmini ya kimazingira itokanayo na muelekeo wa utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia katika visiwa vya Unguja na Pemba ni suala muhimu sana hasa ukitilia maanani udogo wa visiwa vyenyewe na rasilmali kuu za kiuchumi kuwa zinatokana na bahari na ardhi. Maeneo hayo yote mawili hutumika katika harakati za utafutaji na uchimbaji wa mafuta.

Serikali ya Norway kwa kushirikiana na Wizara yangu iliahidi kufanya semina na kongamano zenye lengo la kutoa taaluma kuhusu athari za mazingira zinazotokana na utafutaji na uchimbaji wa mafuta hapa Zanzibar ikiwa ni sehemu ya kuelimishana na matayarisho ya harakati za utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar. Wizara yangu inaendelea na mazungumzo ya karibu na Norway ili kufanikisha mpango huo.

MALENGO

120. Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Nishati Na Madini katika Mwaka wa Fedha 2012/2013 imepanga kutekeleza yafuatayo:-

1) Kuandaa mpango kazi wa Utekelezaji wa Sera ya Nishati ya Zanzibar *(Preparation of Action Plan of Energy Policy).*

2) Kuendelea na juhudi za kuwapatia wananchi wa Zanzíbar elimu juu ya matumizi ya nishati mbadala kama vile umeme wa jua na upepo.

3) Kushiriki katika masuala yote ya nishati ya kitaifa, kikanda, na kimataifa.

4) Kuendelea kusimamia upatikanaji wa mafuta Zanzibar (Dizeli, Petroli na Mafuta ya taa).
5) Kukamilisha Sheria ya kusimamia usambazaji wa mafuta na ile ya mdhibiti wa nishati.

6) Kushirikiana na Washirika wa Maendeleo katika kuimarisha na kutekeleza programu ya mafunzo ya Mafuta na Gesi Asilia.

7) Kushirikiana na Serikali ya Norway katika utekelezaji wa kazi ya tathmini ya mazingira ya Zanzibar *(Strategic Environmental Impact Assesment)* ambayo itatoa mwelekeo wetu kwenye sekta ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

8) Kuanzisha mikakati ya kujiimarisha na utafiti na matumizi ya teknolojia za Nishati mbadala kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za nje na ndani ya nchi ikiwa ni pamoja na kujenga mashirikiano na uwezo wa taasisi za ufundi hapa Zanzibar katika kutimiza lengo la upatikanaji wa nishati ya uhakika kwa visiwa vya Zanzibar*(Energy Security).*

121. Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Nishati iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2012/2013 naliomba Baraza lako Tuku kuidhinisha matumizi ya Tsh. 216,000,000 kwa kazi za kawaida na Tsh. 200,000,000 kwa kazi za maendeleo.

SHIRIKA LA UMEME
Mapato.

122. Mhe. Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2011/2012, Shirika lilikadiria kukusanya Tsh. 34,065,259,920 badala ya Tsh. 57,694,406,200 kutokana na biashara ya kuuza Umeme na huduma zinazotolewa kwa wateja. Hadi kufikia Machi 2012, Shirika limekusanya jumla ya Tsh. 29,434,821,280 sawa na asilimia 86.4 ya makadirio.

123. Mhe. Mwenyekiti, mabadiliko hayo ya ukusanyaji wa mapato yametokana na kutopata idhini ya kufanya mabadiliko ya bei za kuuzia

umeme kwa wateja kutoka Serikalini, ambapo Shirika lilitakiwa kuuza Umeme kwa bei ya Tsh. 120 badala ya Tsh. 170 kwa uniti moja.

Matumizi.

124. Mhe. Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2011/2012, Shirika lilikadiria kutumia Tsh. 50,589,172,311 badala ya Tsh. 56,903,733,123 kwa mchanganuo wa matumizi kama inavyoonekana katika Jaduweli ifuatayo:

Jaduweli Nambari 4

Maelezo	**Gharama husika (Tsh.)**
Gharama ya Ununuzi wa Umeme na Mafuta ya kuzalishia Umeme.	26,589,225,504
Gharama za Uendeshaji wa kazi za Shirika.	16,932,367,474
Gharama za Uchakavu wa Miundo mbinu ya Umeme	7,067,579,333
JUMLA	**50,589,172,311**

Hadi kufikia Machi, 2012 matumizi ya Shirika yalifikia Tsh. 37,202,399,931.00 sawa na asilimia 73.5 ya makadirio. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama unavyoonekana katika jaduweli ifuatayo:

Jaduweli Nambari 5

Maelezo	**Tsh.**
Malipo ya Ununuzi wa Umeme TANESCO	12,070,321,719
Deni La Ununuzi Umeme TANESCO	8,796,486,410
Ununuzi wa Mafuta ya Kuzalisha Umeme (Unguja)	353,426,000
Kazi za Kawaida	12,250,340,501
Kazi za Maendeleo	3,731,825,302
JUMLA	**37,202,399,932**

Utekelezaji wa Kazi za Miradi ya Maendeleo:

125. Mhe. Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2011/2012 Shirika lilijipanga kuitekeleza miradi mitano ifuatayo:

Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Pili ya Umeme Unguja.

126. Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa njia ya pili ya umeme kutoka Ubungo hadi Mtoni Unguja ulianza Julai, 2008 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Disemba 2012. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la Changamoto za Milenia (MCC) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti**,** lengo kuu la mradi huu ni kuongeza uwezo wa upatikanaji wa umeme wa uhakika katika kisiwa cha Unguja. Hadi kufikia Machi 2012 kazi zifuatazo zilikwisha tekelezwa:

i. Upimaji wa njia mpya ya umeme ya ardhini umekamilika.

ii. Utengenezaji wa waya wa baharini wenye urefu wa kilomita 39.5 uliokabidhiwa kwa kampuni ya VISCAS CORPORATION ya Japani umekamilika. Majaribio ya mwisho yameshafanywa kwa mafanikio. Ulazaji wa waya baharini kutoka Ras Kiromoni hadi Ras Fumba unatarajiwa kufanywa hivi karibuni.

iii. Kazi ya ujenzi wa njia mpya ya umeme wa juu kutoka Ubungo hadi Ras Kiromoni na Ras Fumba hadi Mtoni imeshaanza chini ya kampuni ya KALPATARU kutoka India. Miongoni mwa kazi zilizotekelezwa ni:

   a. Kupima eneo linalojengwa njia mpya ya umeme wa juu *(Overhead Line).*

   b. Kufanya uchunguzi wa udongo "**Soil test**" sehemu itakapojengwa mihimili ya Minara ya umeme wa juu wa mkondo wa 132kV.

iv. Kazi ya ujenzi wa vituo vipya vya kusafirisha na vya kupokea umeme iliokabidhiwa kwa kampuni ya "***SYMBION ALSTOM****"* ya Marekani tayari imeshaanza na kazi zilizotekelezwa ni:-

   a. Ufungaji wa transfoma mbili kubwa zenye uwezo wa 60MVA kila moja na kuziweka kwenye mihimili yake, tayari kwa ufungaji wa vifaa vya umeme katika kituo cha umeme Mtoni.

Aidha, hatua za ujenzi wa vituo vipya vya kupokelea na kusambazia umeme zinaendelea vizuri.

Uimarishaji wa njia za kusambazia Umeme Unguja.

128. Mhe. Mwenyekiti, uimarishaji wa njia za kusambazia umeme kwenye maeneo ni jambo muhimu kwa usalama wa watumiaji umeme. Lengo ni kuimarisha miundombinu ili kwenda sambamba na ongezeko la megawati 100 zinatarajiwa kupatikana kupitia mradi wa ujenzi wa njia ya pili ya Umeme.

Miradi inayotekelezwa katika uimarishaji wa njia za kusambazia umeme ni kama ifuatayo:-

i. **Kuimarisha Kituo cha Umeme - Mpendae.**

Ujenzi wa kituo cha Mpendae umefadhiliwa na Serikali ya Ubelgiji kwa msaada wa mkopo nafuu wa Euro 790,550, sawa na Tsh. bilioni 1.6 pamoja na mchango wa Shirika la Umeme Tsh. milioni 160. Fedha hizo zimetumika kwa kugharamia shughuli zifuatazo:-

a. Kujenga jengo jipya la kuhifadhia vifaa vya umeme katika kituo.

b. Kununua na kufunga transfoma mbili kubwa pamoja na vifaa vyake zenye uwezo wa 7.5MVA kila moja.

Mradi huu unalenga kuimarisha upatikanaji wa huduma ya umeme kwenye maeneo ya Mpendae, Mombasa kwa Mchina, Mbweni, Mazizini, Tomondo, Mombasa, Kiembesamaki kijijini, Uwanja wa ndege Kisauni na Chukwani.

ii. **Uimarishaji wa Njia na Ujenzi wa Vituo Vipya Vitatu (3) Vya Umeme Unguja.**

Mhe. Mwenyekiti, Mradi umelenga kuimarisha njia za kusambaza umeme kwenye maeneo ya Kusini, Kaskazini na Fumba Unguja, hasa baada ya Mradi wa Njia ya Pili ya Umeme kukamilika. Ujenzi wa njia za umeme unaendelea sambamba na ujenzi wa vituo vipya vya umeme vya Mtoni, Mwanyanya na Welezo na kwa sasa upo katika hatua ya kukamilisha ujenzi wake.

130. Mhe. Mwenyekiti, Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la JICA iliyosaidia Yeni Bilioni 3.0 sawa na Tsh. Bilioni 55.0 za Tanzania. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imechangia Tsh. Bilioni 2.0 kwa kufidia mali na mazao ya wananchi walioathiriwa kwa njia moja au nyengine. Mradi huu unatarajiwa kumalizika mapema mwaka 2013.

Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini.

131. Mhe. Mwenyekiti, kazi ya usambazaji umeme vijijini imeendelea kutekelezwa kwa mfuko wa Shirika la Umeme pamoja na mchango wa wanavijiji. Hadi kufikia Machi 2012 vijiji 25 vimebahatika kusambaziwa umeme. Baadhi ya vijiji hivyo bado kazi ya ujenzi zinaendelea. Vijiji vyenyewe ni kama inavyoonekana katika jaduweli ifuatayo:-

Jaduweli Nambari 6

	UNGUJA		**PEMBA**
1.	Kwarara	17.	Uganda
2.	Kiboje Mwembeshauri	18.	Magombani
3.	Kazole	19.	Shangini
4.	Kizimkazi Dimbani	20.	Ngezi kuyuni
5.	Kizimkazi uswizi	21.	Machengwe- Mtambwe
6.	Kijichi	22	Kimbuni
7.	Kwambani	23.	Pujini kijili
8.	Fuoni meli tano	24.	Mgogoni
9.	Fuoni kidarajani	25.	Msengele
10.	Donge Mbiji		
11.	Donge Muwanda		
12.	Manyame- Machui		
13.	Mchangani Shamba		
14.	Bumbwisudi		
15.	Dole		
16.	Tunguu mji mpya		

Mhe. Mwenyekiti, vijiji tulivyovitaja hapo juu vinatarajiwa kukamilishwa kazi zote ifikapo mwishoni mwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Jumla ya Tsh. milioni 625 zimetumika. Kati ya fedha hizo Tsh. milioni 560 kutoka kwa Shirika lenyewe na Tsh. milioni 65 zimechangwa na wanavijiji.

Mradi wa Ufungaji Mita 10,000 za Tukuza.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2012, Shirika limenunua mita Elfu Tisa (9,000) za TUKUZA kwa gharama ya Tsh. 944,766,628 ambazo zimefungwa kwa wateja wapya pamoja na kuwabadilishia wateja wanaotumia mita za kawaida.

Kuendeleza Mpango wa Nishati Mbadala.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Shirika imefanya mazungumzo na Wawekezaji kutoka nchi mbali mbali, ambao wameonesha nia ya kutaka kuwekeza katika uzalishaji umeme humu nchini.

MALENGO.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la umeme kwa mwaka wa fedha 2012/2013 limepanga kuendeleza na kutekeleza miradi ya maendeleo kama ifuatayo:-

1. **Mradi wa Njia ya Pili ya Umeme Unguja.**

Wizara itashirikiana na Shirika la Umeme ili kuhakikisha kwamba ujenzi wa njia ya pili ya umeme – Unguja inakamilika kwa wakati.

2. **Mradi wa Uimarishaji wa Njia za Kusambazia Umeme .**

Wizara itahakikisha kuwa lengo la mradi huu wa kuimarisha njia za umeme sambamba na ujenzi wa vituo vipya vya umeme katika maeneo ya Mwanyanya, Mtoni na Welezo unakamilishwa kwa wakati.
`

3. **Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini.**

Mhe. Mwenyekiti, Shirika linatarajia kuendeleza usambazaji wa umeme katika vijiji vya Mtwango- Pongwe , Kibonde Maji - Koani na Mkanyageni kwa Unguja na Kivungo, Kilindi, Simaongwe na Kisiwa Panza kwa Pemba. Wizara itahakikisha kwamba mradi utatekelezwa kwa manufaa ya Wananchi na Taifa kwa jumla.

4. **Mradi wa Ufungaji wa Mita za TUKUZA.**

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya ufungaji wa mita za Tukuza inatarajiwa kuendelezwa kwa kufungwa mita 50,000 katika maeneo yote ya Visiwa hivi na pia kuanzisha huduma ya kununua umeme wa Tukuza kwa kutumia simu za mkononi.

5. **Kuendeleza kazi ya upatikanaji wa nishati mbadala ya kuzalisha umeme.**

Mhe. Mwenyekiti, Wizara itaendelea kushirikiana na wataalamu ili kuwapata Wawekezaji wenye uwezo wa kuekeza katika nyanja ya uzalishaji umeme kwa kutumia nishati mbadala. Lengo ni kuwa na vianzio vya kuzalisha umeme nchini.

Mapato na Matumizi.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika linakadiria kukusanya Tsh. 68,971,586,560. Kati ya fedha hizo, Tsh. 60,517,741,120 ni mauzo ya umeme, Tsh. 8,453,845,440 zitakusanywa kutokana na mapato mengineyo.

Aidha, Shirika linatarajia kutumia jumla ya Tsh. 76,512,926,772 kwa kazi za Kawaida na za Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Tsh. 41,519,577,144 kwa

Ununuzi na Uzalishaji Umeme, Tsh. 17,867,170,208 kwa kazi za Kawaida na Tsh. 17,126,179,420 kwa kazi za Maendeleo.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuchukua nafasi hii kwa mara nyingine tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kuwatumikia Wananchi wenzangu kupitia Wizara hii, ambayo inawagusa wananchi wenyewe ama mmoja mmoja au kwa ujumla wao.

Mhe. Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba utekelezaji wa Wizara yangu ndani ya Mwaka uliomalizika ulikabiliwa na changamoto kadhaa kama ilivyoelezwa. Hata hivyo, Wizara yangu ilijitahidi kuzikabili kadri ilivyoweza, na naamini wananchi wameona matunda ya juhudi zetu. Ninawashukuru sana wananchi kwa uelewa wao, sambamba na ushirikiano wao katika kupata huduma bora zaidi kutoka katika Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa Mwaka ujao wa Fedha 2012/2013, wananchi wategemee ongezeko kubwa la ubora wa huduma na ufanisi wa utendaji kutoka Wizarani kwangu. Upatikanaji wa umeme utaongezeka sambamba na kupungua sana kwa ukatikaji umeme, miradi ya maji katika miji ya Pemba na vijijini nchi nzima itakuwa imetoa sura ya matumaini. Usimamizi ardhi na udhibiti ujenzi utakuwa bora zaidi kutokana na mikakati iliyokwishaelezwa, sambamba na ongezeko la kasi ya utatuzi wa migogoro ya ardhi. Aidha, udhibiti wa nishati na upatikanaji wake utakuwa fanisi zaidi baada ya Sheria zilizotajwa kufanya kazi, sambamba na ongezeko la uwezo wa watendaji katika nyanja husika.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa niaba ya Wizara yangu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, naomba kuchukua nafasi hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mashirika ya Kimataifa na yasiyo ya Kimataifa, Sekta binafsi, NGO"s, CBO"s na wananchi kwa jumla kwa mashirikiano makubwa waliyoyaonesha kwa Wizara yangu kwa misaada yao ya hali na mali waliyoitoa na wanayoendelea kutoa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara yangu. Washirika hao ni pamoja na JAPAN, NORWAY, SWEDEN, MAREKANI, CHINA, EGYPT, FINLAND, UNICEF, UNESCO, UNDP, DFID, JICA, Sida, UN HABITAT, ADB, TASAF, ZATI, IFA, NORAD, RED CROSS, ACRA, BENKI YA DUNIA, IVO DE CARNERI FOUNDATION, UBELGIJI, RAK GAS TANZANIA, EU, PETRAD, MCC ya Marekani, pamoja na wale wote ambao kwa bahati mbaya hatukuweza kuwataja . Tumepata faraja kubwa sana kwa michango yao kwa maendeleo ya nchi yetu, tunaahidi kuienzi na kuiendeleza na kuithamini michango hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena naomba kukushukuru wewe mwenyewe Mhe. Mwenyekiti, Naibu Spika na Waheshimiwa wote kwa kunisikiliza kwa utulivu na umakini wa hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, kwa imani yake kwangu na kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuitumikia nchi yangu. Aidha namshukuru Mheshimiwa Makamo wa Kwanza wa Rais na Mheshimiwa Makamo wa Pili wa Rais kwa misaada na maelekezo yao kwangu wote ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu uadilifu zaidi katika kazi zao, afya njema na maisha marefu pamoja na familia zao.

Tunaomba pia kuwashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zilizotembelea na kufanya vikao na Wizara yangu. Maoni, ushauri na maelekezo yao kwetu yamesaidia sana sio tu katika utekelezaji wa kazi bali pia katika uandikaji wa hotuba hii. Shukurani maalum kwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa msaada wao mkubwa kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia kumshukuru sana Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na Wafanyakazi wenzake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuwezesha vitabu vya Bajeti za Wizara zote kupatikana kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, shukurani maalum ziwaendee wafanyakazi wenzangu wote wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa msaada wao mkubwa kwangu Mwenyezi Mungu awajaalie wote afya njema na maisha marefu bila ya msaada na mashirikiano yao bajeti hii isingeweza kuwasilishwa.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wayapokee, wayajadili kwa kina, watushauri na kutuelekeza na hatimae wayapitishe Makadirio haya. Tuna imani kubwa kuwa michango ya Waheshimiwa Wajumbe itatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ya kazi vizuri zaidi katika kipindi kijacho cha mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, ili Wizara yangu iweze kutekeleza kazi, majukumu na malengo niliyoyaeleza, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Tsh 6,708,000,000 kwa kazi za kawaida na Tsh 73,374,728,000 kwa kazi za maendeleo. Kati ya hizo Tsh 5,301,928,000 ni mchango wa Serikali na Tsh 68,072,800,000 ni mchango wa wahisani kwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naliomba Baraza lako Tukufu likubali matumizi ya Wizara yangu jumla ya Tsh 80,082,728,000 na pia naomba idhini ya kukusanya mapato ya Tsh 4,092,000,000 kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo yangu yote ya hotuba hii vile vile nawasilisha maelezo ya bajeti inayozingatia programu. Wizara yangu ikiwa mojawapo ya Wizara za majaribio mawasilisho ya maelezo hayo inazingatia program ni kwa ajili ya taarifa kwa Baraza lako na sio sehemu ya majadiliano.

Kwa ufafanuzi zaidi ninaomba muangalie kiambatanisho "H1 na H2".

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Rashid Seif Suleiman (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi) Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii. Naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu hotuba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kunijaalia afya njema na uzima na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu katika kutekeleza majukumu ya kulijenga taifa letu. Aidha, napenda kwa moyo wa dhati nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kutoa maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi Maji na Nishati kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumshukuru kwa dhati Waziri wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Mhe. Ramadhani Abdalla Shaaban pamoja na watendaji wa Wizara hii wote kwa mashirkiano yao ya dhati wanayoipatia Kamati yetu katika kutekeleza kazi zake za msingi kama ilivyoelekezwa katika kanuni za Baraza la Wawakilishi. Aidha, napenda kumpongeza tena Mhe. Waziri kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Wizara hii, tunaamini kwamba uzowefu na jitihada zake zitasaidia ufanisi wa Wizara hii ngumu, aliyokabidhiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa moyo thabiti kabisa napenda pia kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati hii kwa mashirikiano yao wanayonipatia katika kuhakikisha kwamba Kamati yetu inaweza kukamilisha

kutekeleza kazi zake za kuliwakilisha Baraza katika kusimamia na kufuatilia shughuli mbali mbali za wizara inazozisimamia.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuongeza msisitizo wa shukurani zangu naomba uniruhusu niwatambue wajumbe wa waliounda Kamati hii kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Mwenyekiti
2.	Mhe. Rashid Seif Suleiman	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Hassan Hamad Omar	Mjumbe
4.	Mhe. Subeit Khamis Faki	Mjumbe
5.	Mhe. Salma Mussa Bilali	Mjumbe
6.	Mhe. Shawana Bukhet Hassan	Mjumbe
7	Mhe. Marina Joel Thomas	Mjumbe
8.	Ndg. Aziza Wazir Kheir	Katibu
9.	Ndg. Abdalla Ali Shauri	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi ni miongoni mwa Wizara muhimu sana kwa maendeleo na mustakabali wa nchi na wananchi wa nchi yetu, hii ni kutokana na ukweli kwamba wizara hii imebeba sekta muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu pamoja na maisha ya wananchi kwa ujumla, miongoni mwa sekta hizo ni pamoja na Sekta ya Ardhi, Maji na Umeme. Umuhimu wa sekta hizi umepelekea kuwepo kwa changamoto nyingi katika Wizara ya Ardhi Makaazi Maji na Nishati.

Kutokana na hali hiyo yamekuwepo malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuhusiana na uendeshaji wa taasisi zinazohusika na sekta hizo katika kuwahudumia wananchi. Hivyo ni wajibu wa watendaji wa wizara hii kufanya kazi kwa uadilifu na umakini mkubwa katika kutekeleza majukumu yao ya kuwatumikia wananchi pamoja na taifa kwa ujumla. Aidha, kwa upande wa serikali ni vyema ikahakikisha kwamba inazijengea mazingira mazuri taasisi zilizomo katika wizara hii, ikiwemo suala zima la kuwajengea uwezo watendaji wake, pamoja na kufanya tathmini ya mara kwa mara ili waweze kuona kasoro na kuchukua hatua zinazofaa katika kurekebisha kasoro zinazojitokeza katika utekelezaji wa shughuli za kawaida za wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo machache sasa naomba kutoa maoni ya Kamati ya mawasiliano na Ujenzi kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi Maji na Nishati kwa mwaka wa fedha

2012/2013. Hotuba hii ya maoni ya Kamati, itagusa baadhi ya maeneo ambayo Kamati yetu imehisi kuwa hatuna budi kuyatolea maelezo. Maeneo hayo ni kama yafuatayo;

UWAJIBIKAJI WA WAFANYAKAZI

Mhe. Mwenyekiti, kufanya kazi kwa kujituma na kwa ubunifu ni suala muhimu sana katika kufikia malengo ya tasisi yoyote ile, kwa muda mrefu tumekuwa tukishuhudia wafanya kazi wengi wa taasisi za umma wakifanya kazi kwa mazoea bila ya kujali ni kwa kiasi gani wanaweza kufikia malengo ya kazi zao kwa mujibu wa muongozo na mwelekeo wa taasisi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, hali hii inajitokeza kutokana na ukweli kwamba wafanyakazi wengi wa taasisi za umma hufanya kazi katika hali ya utaratibu wa kawaida tu yaani '*daily rootine*' bila ya kuwa wabunifu na kuzingatia mipango na miongozo maalum ya kazi kama vile mipango kazi (*action plans*), sera (*policies*), na dira (*vision*) za taasisi za Wizara wanazozifanyia kazi, hali hii hupelekea kutokuwepo kwa ufanisi wa kazi hizo. Aidha, wafanyakazi hushindwa kujitathmini wao wenyewe namna wanavyozisaidia taasisi zao ili ziweze kufikia malengo yaliyokusudiwa ya taasisi hizo. Aidha, Kamati yetu inazidi kusisitiza kuwa ni wajibu wa kila mtumishi wa umma kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa na serikali na inaunga mkono juhudi za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi za kukemea tabia hizo na kuwataka watumishi wa umma wabadilike na waache kufanya kazi kwa mazowea ili kuleta mabadiliko katika sekta zote na wananchi waweze kunufaika na huduma za taasisi hizo.

MAFUNZO KWA WAFANYA KAZI

Mhe. Mwenyekiti, suala la kuwajengea uwezo wafanyakazi ni muhimu sana katika kukuza ufanisi na uwezo wa watendaji. Kamati yetu inapenda kuiomba Wizara izidishe juhudi zaidi za kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake, mafunzo ambayo ni muhimu sana katika kukuza uelewa na kuwajengea uwezo wa kufanyakazi zao kwa ufanisi mkubwa. Aidha, Kamati yetu inaipongeza Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa kuweza kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wapatao 84 kwa mwaka 2011/2012 katika vyuo mbali mbali, ndani na nje ya nchi pamoja na kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanya kazi wapatao 91 .

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa serikali inasomesha wafanyakazi wake kwa lengo la kupata wataalamu katika sekta husika, ni vyema kukawekwa mikakati maalum kuhakikisha kuwa wafanya kazi hao wanapomaliza masomo yao wanarejea kuitumikia serikali hasa katika taasisi zao walizotoka. Ili kuwabana watendaji hao wanaosomeshwa na serikali kurudi kufanya kazi katika taasisi zao za awali ni vyema serikali ikazingatia kuwapatia wafanyakazi maslahi yanayoendana na utaalamu wao baada ya kumaliza masomo yao.

IDARA YA MIPANGO, SERA, NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na malengo iliyojiwekea wizara, Kamati inasisitia haja ya kuwepo kwa chombo cha kusimamia ubora wa mafuta yanayoingizwa nchini na kitakachoratibu uhalali wa bei za umeme na maji. Pia Kamati inaitaka wizara kuharakisha nia yake ya kuweka sheria ya tathmini ya ardhi na majengo na kupatikana kwa taasisi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, sheria inayohusu uhaulishaji ardhi au mali isiyohamishika bado ina mapungufu na ni moja kati ya chanzo cha migogoro. Wizara inapaswa iliangalie upya na kuona haja ya kufanya marekebisho ili kuepusha migogoro na kupatikana kwa uadilifu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuandikwa lengo la kufikisha umeme katika vijiji vilivyokosa huduma hiyo, Idara inapaswa isimamie ufikishaji umeme huo vijijini badala ya suala hilo kubakia kwenye maandishi tuu.

IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile idara hii ndiyo inayoshughulika na maslahi ya wafanyakazi, Kamati inaitaka Wizara kupitia Idara hii kuendeleza mawasiliano na Wizara ya Utumishi na Utawala Bora kutatua tatizo lililojitokeza hivi sasa la baadhi ya watumishi wa ngazi ya chini wa wizara hii kutofaidika na nyongeza ya mishahara iliyoanza kulipwa mwezi wa Oktoba, 2011.

IDARA YA ARDHI NA USAJILI, MIPANGO MIJI NA VIJIJI NA IDARA YA UPIMAJI NA RAMANI.

CHANGAMOTO ZA IDARA

MIGOGORO YA ARDHI

Mhe. Mwenyekiti, moja kati ya matatizo sugu katika nchi yetu ni suala la migogoro ya ardhi ambapo mara kwa mara imekuwa ikiibuka katika sehemu mbali mbali. Miongoni mwa migogoro hiyo ni pamoja na kuchukuliwa kwa baadhi ya maeneo ya wananchi kwa mabavu, kufutiwa hati kwa baadhi ya wawekezaji bila ya kufuata taratibu za sheria ya umiliki wa ardhi. Vilele vile kuna baadhi ya wawekezaji hufutiwa hati za ardhi na kupewa wawekezaji wengine bila kuzingatia taratibu za kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, iwapo hali hii itaendelea inaweza kupelekea wawekezaji kutokuja nchini kuwekeza na hivyo kutuletea athari kubwa za kiuchumi. Aidha, kwa upande mwengine kumekuwa na shutuma kwa baadhi ya Masheha, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuhusika kwa namna moja ama nyengine katika migogoro hii, pia inawezekana kuna baadhi ya watendaji wa Serikali wachache wasio waaminifu kuhusika katika kadhia hii. Hali hii inajitokeza kutokana na ukweli kwamba ardhi imekuwa ni rasilmali muhimu na ambayo thamani yake inaongezeka siku hadi siku, hivyo baadhi yao wamekuwa wakijenga tamaa ya fedha na kukiuka maadili ya kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inasisitiza kuwa pamoja na ahadi nyingi zinazotolewa na Serikali kuhusiana na utatuzi wa suala la migogoro ya ardhi, ipo haja kwa Serikali yetu kuwawajibisha wahusika wote wanaotumia nafasi zao kinyume na ilivyokusudiwa wakiwemo baadhi ya viongozi wa Serikali na watendaji wote wanaohusika na kadhia hiyo. Hatua hiyo italeta matumaini kwa wananchi walio wengi ambao wamekumbwa na suala la migogoro ya ardhi na wamekata tamaa kwa kiasi kikubwa.

UJENZI HOLELA

Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukishuhudia kuendelea kwa ujenzi holela ambao hauzingatii mipango maalum na mahitaji ya baadae *“Master Plan”* Kumekuwa na wimbi kubwa la uvamizi wa maeneo ya kilimo na maeneo mengine ya wazi, ambayo yanavamiwa na kujengwa majengo ya biashara na

makaazi. Kamati yetu inatoa wito kwa Serikali kuhakikisha kwamba maeneo ya wazi hayatolewi kwa ajili ya shuguli za biashara na makaazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu ni kisiwa na haina eneo kubwa sana la ardhi, ni vyema kwa Serikali ikalizingati hilo kwa kuweka mipango mizuri ya matumizi ya ardhi. Ardhi ni raslimali muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi iwapo itatumika vizuri, hivyo ipo haja kwa Serikali kujiwekea mipango mizuri katika kuhakikisha inatenga maeneno maalum kwa ajili ya kilimo, maeneno ya uwekezaji na maeneno ya makaazi ya wananchi, kinyume na hali ilivyo hivi sasa ambapo hakuna utaratibu maalum wa kudhibiti hali hiyo. Iwapo ardhi haitotumika vizuri inaweza ikawa ni sababu ya kuliingiza taifa letu katika umasikini kwa kukosa kuweka maeneno maalum kwa ajili ya shughuli za kilimo na uwekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa kupima maeneo na kugawanywa kwa wananchi na taasisi bila kupeleka miundombinu siyo tu inazorotesha maendeleo ya ujenzi bali pia inachangia katika uvamizi wa maeneo ya njia na sehemu za wazi.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na ukaribu wa kazi zinazofanywa na Idara tatu hizi ambazo ni Idara ya Ardhi na Usajili, Idara ya Mipango Miji na Vijiji na Idara ya Upimaji na Ramani, Kamati inatoa msisitizo kuwa ile fikra ya kuziweka chini ya mwamvuli mmoja Idara hizi zikawa kama “Kamisheni” au vyenginevyo iharakishwe ili ziweze kufanya kazi kwa mashirikiano na kurahisisha kazi za idara hizo kwa kuwahudumia wananchi kwa wakati na hatimaye kupunguza migogoro ambayo imekua ikiibuka na kuongezeka kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pale inapoamua kukutana na Idara zote tatu kwa pamoja umuhimu wa kufanya hivyo huonekana ambapo maafisa kutoka katika Idara hizo walishirikiana kujibu hoja za Wajumbe na kutoa rai zao ambazo ni za msingi katika kuziimarisha taasisi hizo, na kupelekea Kikao hicho kwenda kwa ufanisi wa hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile Wizara hii kupitia idara tatu hizi ndiyo inayogawa maeneo ya ujenzi wa nyumba, viwanda, mahoteli na mengineyo, na kuwa ni dhamana wa kufuatilia ripoti ya tathmini ya mazingira (*Environmental Impact Assessment- E I A*) ni dhahiri kuwa Idara ya Mazingira mahali pake ni hapa.

Kwa vile Idara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Kilimo wanafuatilia mazingira ya baharini na maeneo ya kilimo, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ingepewa jukumu la uratibu wa mazingira yote kwa ujumla.

MAHAKAMA YA ARDHI

Mhe. Mwenyekiti, bado tunakabiliwa na tatizo la mrundikano wa kesi za ardhi hususan katika kisiwa cha Unguja.Wakati Kamati yetu ikipitia bajeti ya Wizara ilielezwa kuwa kati ya kesi 95 zilizofunguliwa Unguja kati ya Julai hadi Machi 2012 ni kesi 15 tu ndizo zilizotolewa hukumu, hali hii inatokana na uchache wa Mahakimu katika mahakama hizo, ili kuondokana na tatizo hilo Kamati yetu inashauri Wizara ichukue hatua za dharura kwa kuiombea Mahakama ya Ardhi iongezewe Mahakimu pamoja na kufungua Mahakama za Ardhi za Mikoa.

Aidha, Kamati yetu inaiomba Wizara katika Bajeti ya 2012/2013 iangalie uwezekano wa kuwajengea mazingira bora ya kimaslahi watendaji wa Mahakama ya Ardhi kutokana na unyeti wa majukumu yao, ni vyema watendaji hawa wakajengewa mazingira bora ya kimaslahi ili kuepusha uwezekano wa kuchukua rushwa wakati wa kutekeleza kazi zao.

IDARA YA NISHATI

Mhe. Mwenyekiti, ili kukuza uchumi wa nchi yetu suala la kuwepo kwa nishati ya uhakika ya umeme ni suala la lazima, na hatuwezi kuendelea bila ya kuwa na nishati ya uhakika, moja kati ya vitu vya msingi ambavyo wawekezaji huangalia kabla ya kuekeza ni kuwepo kwa nishati ya uhakika. Kwa muda mrefu sasa nchi yetu imekosa umeme wa uhakika na ambao hautoshelezi mahitaji yetu ya kawaida. Katika hali kama hii athari yake ni kupoteza fursa nyingi za wawekezaji kuja kuekeza katika nchi yetu, hususan katika sekta za viwanda sekta ambayo kimsingi huhitaji kuwepo kwa nishati ya umeme ya uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imefarajika kusikia kwamba, ripoti ya wataalamu wa Jumuiya ya Ulaya '*European Union'* (*EU*) kuhusu uwezekano wa Zanzibar kuzalisha nishati mbadala, inayoonesha kwamba, Zanzibar inaweza kuzalisha umeme mbadala kwa kutumia upepo, takataka na jua. Kamati yetu inaishauri Serikali kuifanyia kazi ripoti hiyo ya wataalamu

kuhusu njia muafaka kwa uzalishaji wa umeme ili kuharakisha mchakato wake wa kupatikana kwa nishati mbadala ya uhakika na ambayo itakuwa ina gharama nafuu ili kuwapunguzia ugumu wa maisha wananchi kwa kuwa hali ya hivi sasa sio nzuri ambapo bei ya nishati hiyo iko juu na inazidi kupanda siku hadi siku.

NISHATI YA MAFUTA

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imefarajika na taarifa ya Idara ya Nishati kwamba kwa hivi sasa masuala yanayohusu nishati yatasimamiwa moja kwa moja na Idara hiyo badala ya kusimamiwa na Wizara ya Fedha. Aidha, tumefarijika kupata taarifa kwamba Wizara inaandaa Rasimu ya Sheria ya usamabazaji wa Mafuta (*Zanizbar Petroleum Supply Act)*, pamoja na Sheria ya udhibiti wa mafuta, ili bidhaa ya mafuta iweze kusimamiwa na sekta husika kwa ufanisi zaidi na kuwa na mdhibiti mahususi wa bidhaa ya mafuta. Kamati yetu inaisisitiza Serikali kuzingatia kuwaandaa watendaji wa Idara ya Nishati kwa kuwapatia mafunzo yanayohusiana na masuala ya Nishati ili kuwaweka tayari na mabadiliko ambayo tunayatarajia likiwemo suala la kuanzisha nishati mbadala pamoja na suala la uchimbaji wa mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na utegemezi mkubwa wa nishati ya umeme hapa Zanzibar kutoka Tanzania bara, Idara hii ina jukumu kubwa la kutafuta mbinu za nishati mbadala. Kutokana na jukumu hilo ambalo lingehitaji utafiti, taaluma na mikakati ya hali ya juu ambayo itaweza kuipeleka nchi katika nishati inayotumia nyenzo tulizonazo na ambayo haiharibu mazingira (*Environmental friendly*).

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na bajeti ndogo ya Idara hii, Kamati inaona kuwa dalili za kufikiwa mapema malengo hayo hayapo, hivyo Kamati inaishauri Serikali inapopanga bajeti iangalie na unyeti wa malengo yake kwa kuziwekea bajeti ya kutosha Idara zake ili ziweze kufikia malengo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Idara hii ikabidhiwe mambo yote yanayohusu nishati ikiwemo udhamini juu ya uingizaji wa mafuta nchini, pamoja na upangaji wa bei na uhalali wa kuyashughulikia makampuni yanayoingiza na kuuza mafuta ya petroli na mengineyo.

SHIRIKA LA UMEME

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Umeme lingehitaji kufanya marekebisho makubwa katika uendeshaji wake. Ongezeko la bei ya umeme kwa asilimia 40 kwa mkupuo si utaratibu mzuri bali kama gharama zimeongezeka za uendeshaji ni vyema kwa Shirika na Serikali kwa ujumla kupandisha bei ya umeme kidogo kidogo kulingana na hali za wananchi zilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Umeme (*ZECO*) halina budi kujifanyia tathmini ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuwapunguzia wananchi gharama za kuunganisha na kulipia umeme. Aidha, udhibiti wa mapato ya Serikali siyo tu ungeliletea faida Shirika bali pia ungepunguza mzigo kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, shirika halina budi kuweka transfoma za akiba za ukubwa tofauti Unguja na Pemba, ili kuwapunguzia usumbufu wananchi wakati transfoma inapoharibika.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Umeme lina azma nzuri ya kuleta vifaa vya kutosha kwa ajili ya kuwaungia umeme wananchi, hata hivyo Kamati inasisitiza kuwa jambo hilo lifanywe kwa vitendo na Kamati inafuatilia kwa kina ahadi hiyo ili kuona utekelezaji wake unafanikiwa.

MAMLAKA YA MAJI

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya maji (*ZAWA*) ni taasisi muhimu sana iliyobeba jukumu la uhai kwa maelfu ya wananchiwa Zanzibar, kwani “MAJI NI UHAI”.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaikumbusha Mamlaka kuchukua tahadhari zote za kiutawala na kiufundi kuhakikisha kuwa maji yanapatikana katika maeneo ya mijini na vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, upatikanaji wa *pump* za akiba, mabomba na mafundi stadi ni sehemu muhimu za kutoa huduma hii. Ujenzi wa matangi yanayohimili hali ya hewa yetu kunasaidia sana usambazaji wa maji badala ya kutumia njia ya moja kwa moja. Hata tathmini ya uwezo wa *pump* zetu unaweza kufanyika.

Mhe. Mwenyekiti, ili kufuatilia kwa karibu upatikanaji na ukosefu wa huduma ya maji, Kamati inasisitiza ufungaji wa mabomba ya maji kwa zone

maalum katika sehemu za miji na kuunganishwa katika maeneo ya dharura. Utaratibu huu utatoa taarifa mapema *"Early warning system"* katika maeneo ambayo maji yanakosekana na kujua mapungufu yaliyopo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuipa uwezo Mamlaka ya Maji, Kamati inawaomba wananchi wote wanaopata huduma hii ya maji kulipia huduma hiyo bila ya kuchelewa.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, ili wizara iweze kutekeleza malengo yake na kutoa huduma safi kwa wananchi nawaomba wajumbe wenzangu tuipokee, kuichangia na baadae kuipitisha bajeti ya wizara hii yenye Shilingi 80,082,728,000 zikiwemo Shilingi 6,708,000,000 kwa kazi za kawaida na Shilingi 73,374,728,000 kwa kazi za Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha ripoti ya Kamati na kuwaomba Wajumbe kuipitisha, naomba nichukue nafasi yangu kama Mwakilishi kutoa mawili matatu kwa niaba ya Jimbo la Ziwani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Jimbo la Ziwani hasa katika hiyo sehemu ya Ziwani ni sehemu ambayo imenufaika kwa kujengewa tangi la maji na karibuni Mhe. Rais alikwenda kulizindua. Kwa niaba ya wananchi wote wanaonufaika na tangi lile na wananchi wa jimbo la Ziwani, napenda nitoe pongezi zangu za dhati kwa wizara kwa kukamilisha mradi ule ambao hivi sasa unaendelea kuhudumia na kusaidia wananchi katika maeneo tofauti yaliyozungumza Ziwani.

Lakini la pili kwa kuwa inaonekana wazi kwamba ujenzi wa matangi unasaidia usambazaji wa maji kirahisi, naiomba basi wizara izingatie ujenzi wa tangi katika eneo la Gombani ambalo sio tu litasaidia katika Jimbo la Ziwani, hata sehemu ya Gombani ya Jimbo la Wawi itakuwemo na wananchi watanufaika.

Mwisho ni ujenzi wa tangi katika eneo la Ndagoni. Ndagoni ni sehemu ndogo lakini ni sehemu refu kwa sababu udogo wake ni kwa eneo lakini masafa yake ni marefu. Kwa hivyo, uwekaji wa pampu bila ya tangi unawasumbua sana wananchi wanaokaa katika vijiji vya mbali. Kwa hivyo naiomba sana wizara

katika utaratibu wake wa ujenzi wa matangi basi Ndagoni waiwekee nafasi ya pekee ya kwamba kule nako kujengwe tangi kutokana na masafa yake marefu.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, naomba niulize swali la wizara kwamba kuna malalamiko kuhusu upatikanaji wa hatimiliki. Je, suala hili wizara inalijua na ni sababu gani watu ambao wameshapimiwa maeneo wengine ya nyumba, wengine ya mashamba wakawa wanachelewa kupata hatimiliki zao.

Lakini suala la mwisho kwa mchango wangu kwa leo wa binafsi nini hatma ya majenereta yaliyopo Mtoni ikiwa hivi sasa serikali haina uwezo wa kuyaendesha na umeme wanagaiwa kwa mgao, nini hatma ya majenereta yale.

Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na naomba kuwasilisha ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe baada ya kuwasilisha ripoti ya Kamati lakini kabla sijaanza kuwakaribisha wachangiaji wengine ningependa kutoa taarifa ifuatayo.

Kwa siku ya leo kwa bahati nzuri tulibahatika kutembelewa na vijana wetu ambao ni wanafunzi kutoka Skuli ya Mbuyuni Kinondoni Dar es Salaam, lakini kutokana na hali ya shughuli zetu kwa leo na wingi wa watu wa wizara basi imebidi walikuwepo na baadae wamerejea lakini tulitaka kutoa utambulisho tu ili muelewe hivyo.

Baada ya maelezo hayo sasa nimkaribishe Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuanza kutoa mchango wake na baadae atafuatia Mhe. Mohammedraza Hassanali. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Awali kabla ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) aliyeniwezesha kusimama hapa na akanipa pumzi zake na kuweza kupumua vizuri. Kwa neema hiyo namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kusema, *Alhamdullilahi*. Vile vile nitakuwa si mwingi wa fadhila Mhe. Mwenyekiti, kama sikukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kuchangia mawili matatu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza nichangie utangulizi katika bajeti hii iliyoko mbele yetu. Pamoja na ugeni wangu hii bajeti haikukidhi kina hasa katika miradi muhimu kama ile ya maji na utafiti wa uchimbaji wa mafuta.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchangia Idara ya Nishati na Madini katika ukurasa wa 50 kuhusu upatikanaji wa bidhaa ya mafuta ya petroli na dizeli. Idara hii imeshindwa kusimamia majukumu yake kwa sababu mafuta yanayoingizwa hapa nchini hayana kiwango, kuna magari ya watu mengi tu yameharibika Mhe. Mwenyekiti, na kama nongwa na chuki basi mimi naomba radhi zao tukienda kwa Juma Buda tukaangalia kuna gari ngapi hivi sasa zilizoharibika kwa mafuta haya. Kuna daladala ngapi za wanyonge zimelala, kuna *taxi* ngapi za babu zetu hazifanyi kazi hivi sasa kutokana na mafuta haya. Mhe. Mwenyekiti, hapa nitakuwa mkali kuhusiana na mafuta machafu yanayoingizwa na ninaweza nikalia, na mtu mzima akilia ujue kuna jambo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, niingie katika ukurasa wa 15 Mamlaka ya Maji ambapo kila binadamu au kiumbe aliyekuwa hai anahitaji maji. Kuhusu kujenga uwezo Mamlaka ya Maji awamu ya pili mradi huu ni awamu ya pili umefadhiliwa na Wajapani kupitia Shirika la Maendeleo *JICA*, lakini hadi hii leo maji ni tatizo kubwa ambalo halisemeki pamoja na pesa nyingi zilizotolewa na wahisani hawa. Mimi nitahitaji maelezo, hapa mjini tunatumia lita ngapi za maji na uwezo wake serikali ni lita ngapi hata tushindwe kuhudumia suala la maji hapa Zanzibar. Hapa nitahitaji maelezo ya kina Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri katueleza tangu utoaji wa huduma za maji Mkoa wa Mjini Magharibi ni wateja wangapi wameshasajiliwa na kiwango gani kinachowanyima wananchi kukosa maji. Pamoja na huduma hiyo kuchangiwa bado limekuwa tatizo, cha kushangaza zaidi na kinachonitia huruma wananchi wa Mbweni hasa maeneo ya Matrekta miezi mitano wanakosa maji na ukiuliza *pump* yake ni shilingi milioni tano gharama yake leo miezi mitano wananchi wa maeneo ya Mbweni eneo la Matrekta wanakosa huduma hiyo, kweli serikali ishindwe na *pump* ya shilingi milioni tano? Hii ni sawa na kwenda dukani ukaenda ukanunua choroko ukaenda ukapewa bizari, huduma haziridhishi za maji na hapa tulipo Mhe. Mwenyekiti, mimi ukiniruhusu kuchimba naweza kupata maji hapa hapa nilipo, neema kubwa katujaalia Mwenyezi Mungu katika visiwa hivi lakini bado kilio kimekuwa kikubwa.

Majumba ya Michenzani miaka mingapi wamejenga viongozi wetu mpaka hivi leo kitu cha kusikitisha, leo Dr. Mwinyihaji kafanya jitihada ya kufungua bwawa tu pale siku kumi maji kayapata katika *round about* leo kweli serikali ikashindwe na suala hili? Kwa hivyo, serikali haijajidhatiti kwa hili.

Kwa kuhakikisha hilo Mhe. Mwenyekiti, leo Mamlaka ya Maji gari ya kutembelea vile visima na *crane* haina, shilingi ngapi gari hilo, gari inaazimwa Wizara ya Kilimo na Maliasili hapa hapajawa *serious* kufanywa

hili suala ni kuja tukiwadanganya wananchi wetu hakuna jengine, si kisiwa cha kukosa maji hiki. Leo mafundi wanataka kwenda shamba kutoa *pump* wanaisubiri *pump* hiyo itoke Donge imalize na pengine huku wananchi wanazidi kuteseka hii serikali sio ya kuwakomoa wananchi kwa sababu wananchi ndio serikali na binadamu akose yote lakini asikose maji.

Mimi gari hii nishathubutu si mara mbili wala tatu wakinipa shilingi laki moja hamsini mpaka laki mbili kwenda kutoa *pump* kwenye visima eneo la Unguja Ukuu kwa wananchi wa Pete. Pamoja na jitihada zilizofanywa na Wawakilishi sisi lakini Mamlaka ya Maji haijawa *serious* kwa suala hili. Mimi mmoja ninayepata shida Mamlaka ya Maji pale utafiti nakwenda kuomba kwa Mkurugenzi ananambia suala hili nisimuulize la watu wa Pete, nisimuulize watu wa Pete kawaleta nani hapa, mimi sikupata jicho la rehema kusaidiwa wamenileta wananchi. Mimi ndio namwambia naweza kuendelea na nitaendelea na bado wananchi wa Pete hivi sasa wanajiona wa vipi sijui kwa shida inayopatikana. Sisi tumechukua jukumu, "*kullukum rai wakullukum masuul ala raiyatihi*" kila mmoja ni mchunga na kila mmoja aweze kujichunga.

Suala la maji hili linatusumbua sana leo vitendea kazi hapana pale, utaambiwa asubuhi ukakodi gari Mwakilishi watu wakafanye kazi. Tunatoka wapi, tunakwenda wapi. Mhe. Mwenyekiti mimi hapa nitahitaji maelezo kwanza serikali inunue gari, moja iwekwe Pemba na moja iweko Unguja kwa ajili ya visima sio gari ya Wizara ya Kilimo hiyo gari ya Wizara ya Kilimo ukitaka kwenda kushoto inakwenda kulia upinde hali iko halifai kabisa halina kiwango chochote.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji ilipanga kukusanya shilingi bilioni 3 kutokana na hiki kitabu kilivyo, lakini imekusanya shilingi bilioni moja. Mimi nataka Waziri hapa anieleze kwa sababu gani hata wakakusanya shilingi bilioni moja, ukweli siufichi bwana watu hawapati huduma ya maji huo ndio ukweli ulivyo,Mhe Mwenyekiti, wananchi wetu wameshafanya vipara sasa hivi kwa ndoo za maji, leo tunakuja hapa tukawadanganya wananchi ni kampuni ngapi zishakuja hapa kutengeneza mambo ya maji hakuna kilichofikiwa hadi hii leo.

Gari ya kwendea shamba leo hamna unakaa usubiri labda gari ya Mkurugenzi iazimwe au mtu mweninge , wananchi wetu wanateseka na kitu maji.

Mhe. Mwenyekiti nije katika ukurasa wa kuhusu serikali kushirikiana na watu wanaoleta tija katika utekelezaji wa tathmini ya mazingira ya Zanzibar ukiwemo ufuatiliaji na uchimbaji wa mafuta. Kwa kweli serikali haijawa na nia nzuri kuhusu kitengo hiki, mimi nilifikiri Waziri atakuja atatuletea bajeti

nyengine kuhusu kuanzishwa kampuni ya mafuta Zanzibar, maelezo ya mwaka huu na mwaka jana ni hayo hayo. Hili suala nimeshalijadili lakini kupata maelezo ya kina. Leo umelileta hapa ili ukija unipe maelezo ya kina.
Sasa Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala la Mji Mkongwe, kwanza nataka nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uungwana wake, ukweli wake, kwa ubinadamu wake na kwa huduma zake anaziozifanya kuondoa mawe kule Mji Mkongwe. Sasa hapa Mhe. Waziri mimi nitahitaji maelezo kama Mji Mkongwe kweli ndio unaosababisha msongamano huu?

Mhe. Waziri hiki kitu hakipingiki, pana nyumba pale mimi nishauliza mara mbili au tatu katika Baraza hili imetiwa mabati miaka mitatu tokea Mhe. Amani Abeid Karume yuko madarakani, hii nyumba sijui kama inajengwa au vipi, ingekuwa nyumba tongo basi huchukua jiti moja moja na ingekuwa ishamalizika. Sasa hapa tunakuja kuwalaumu wananchi tunazidisha sisi wenyewe viongozi sio wananchi. Kuna barabara ngapi leo kila kitu Mji Mkongwe Mamlaka gani iliyopewa Mji Mkongwe kukata miti ndani ya Mji Mkongwe? Mji Mkongwe sasa Wizara ya Kilimo na Maliasili ina kazi gani, yeye hata aondoshe zile Forodha Mchanga pale hebu iangalie serikali itakosa mapato gani pale. Hebu atueleze hasa Waziri toka kuanza kwa Mji Mkongwe tumepata faida gani sisi wananchi, sikioni labda kimoja tu baada ya kutiwa *tiles* kwa msaada kutoka Ujerumani wananchi hawajui chochote kilichopatikana mji wenyewe umejaa makaro machafu ni aibu kwetu sisi kwa watalii.

Mimi ningewashauri hasa hizi nyumba za Mji Mkongwe wakatia japo chokaa kama uwezo wa kutia rangi hakuna, leo wanakuja kufunga barabara ile ya Mji Mkongwe kwa kisingizio gani, mbona ile njia ya kati kati hawakuifunga pale Wizara ya Mawasiliano kwendea kule mbele na ipo Mji Mkongwe. Leo wanakuja kuleta usumbufu.

Hapa Mhe. Waziri nitahitaji maelezo ya kina kwa barabara ile. Mimi ninampongeza Dk. Mwinyihaji kwa hatua alizochukua. Hizi ni hatua za kiungwana. Mimi leo hapa nitazuia fungu wala hakuna cha kunitisha mtu, mimi ninayemuogopa ni mmoja tu ambaye ni Mwenyezi Mungu. (*Makofi*).

Sababu gani kama kutengeneza Mji Mkongwe ungetengenezwa ule ufukwe wa bahari uliopo mbele yao, ile njia hivi sasa ina kifusi, ile njia kati kati pale imechimbika na inatiwa kifusi. Ndio tunatengeneza Mji Mkongwe kweli hivyo.

Mhe. Waziri hapa nitahitaji maelezo tena ninarudia mara ya tatu, hili suala lilikuwa nimeshalipigia kelele si mara ya kwanza, pili au tatu na mimi Mhe.

Mwenyekiti, ni mkaidi kidogo. Hapa itafika pahali tutapiga kura basi tupige kura lakini njia ikafunguliwe, msongamano umekuwa mkubwa sana. Wananchi wanateseka, haya si mamlaka ya Mji Mkongwe, kila kitu Mji Mkongwe.

Mji Mkongwe wenyewe hivi sasa unanuka hivi sasa, makaro yanavuja, hakuna chochote kinachofanywa, tunafukuzia kama nyoka mdimu. Nyoka wa mdimu kitu hana kazi nacho, ukenda kukichuma anakurukia na yeye hana kazi nacho. Hebu atueleze pale kwa kina kuhusu barabara ya Mji Mkongwe.

Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi nitahitaji maelezo na tena nitakuwa mkali kwa hili. Kama wakati wa kupiga kura basi tutapiga kura lakini hii barabara ikafunguliwe, imekuwa usumbufu wa hali ya juu kwa wananchi. (*Makofi*).

Kuna nyumba pale ninarudia tena imepewa kibali leo miaka mitatu, wengine wanaambiwa baada ya mwezi mmoja hujakamilisha ujenzi wako basi kimefutika. Ile nyumba inajengwa kitu gani. Mhe. Naibu Waziri mimi nimeshakuuliza maswali mara tatu ukawa unanijibu. Hapa ndio wakati wake umefika.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, nitazuia vifungu mpaka nitakapopata maelezo ya kina na yatakayoniridhisha. (*Makofi*).

Mhe. Mohamedraza Hassanali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa heshima na taadhima kwa niaba ya wananchi wangu kwa kupata nafasi hii ya pili, ninapenda kutoa shukurani za dhati kabisa pamoja na Wawakilishi wenzangu ninaendelea kuwashukuru kwa mashirikiano mazuri wanayonipa.

Mhe. Mwenyekiti, nasema Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia vyombo vyake vya sheria vikiwemo hili Baraza la Wawakilishi, Mahakama na taasisi nyengine za kisheria.

Mimi nikitaka kushauri tu naipongeza bajeti aliyoisoma Waziri, mzee wangu Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, lakini vile vile nimpongeze kwa dhati Mwenyekiti wa kamati hii aliyetolea taarifa fupi kuhusu migogoro ya ardhi na mambo mengine katika wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, kama kawaida yangu. Mimi huwa sitafuni maneno. Jembe nitaita jembe na pauro nitaita pauro. Ninasema tena kwamba kila nitakachokizungumza nina ushahidi nacho na nina vielelezo vyangu ambapo wakati wowote vikihitajika.

Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu pamoja na wananchi ni serikali yenye hekma, busara, usikivu pamoja na kujenga ushirikiano na majirani zetu. Sasa kinachonipa taabu Mhe. Mwenyekiti, kupitia wizara hii husika. Kwa ufahamu wangu mimi mdogo serikali zote hizi zilizokuwa zikija madarakani ni serikali za Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*).

Sasa nina ushahidi wa serikali ya awamu ya tano, ulitoa zawadi kwa mfalme wa UAE kiwanja kiliopo Pwanimchangani. Baada ya kupewa zawadi na kwa kweli mimi ninataka kusema kwamba ile kupokelewa kwa zawadi kwa wenzetu wa UAE ni heshima kwa Zanzibar kusema kwamba Sheikh Sayyid familia yake imepewa kiwanja Zanzibar, ile inatosha tu Mhe. Mwenyekiti.

Lakini kinachosikitisha kwamba ninachotaka kusema kuishauri wizara na serikali, hekma, busara na usikivu tuendelee kuwa nao. Sasa ilipokuja awamu ya sita ikafuta ile zawadi ambayo Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Chama cha Mapinduzi, ikafuta na kuondosha zawadi ile bila ya kumjuulisha muhusika, bila ya kuwa na taarifa yoyote ile inayohusika. (*Makofi*).

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kinachotupa taabu sisi Wazanzibari tunaonekana ni watu wastaarabu, ni watu wenye hekma na busara. Sasa kuja kwa watendaji waandamizi kufuta jambo bila ya kuulizia, kilichokuwa au kufanyika. Hata mfano huyo aliyepewa zawadi kiongozi au familia iliyopewa zawadi hawajakitumia kwa miaka kumi au hata miaka ishirini, ile ni zawadi iliyotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Sasa mimi kwa fikra zangu au kwa busara zangu na kwa maelekezo ya wizara inayohusika, kama wangeliona hili suala hawajalitumia wangeliwauliza jamani hapa hamjapapenda naona sasa ni miaka kumi hamjapagusa labda tukakutafutieni sehemu nyengine. Sasa yule aliyepewa zawadi angeliona kwamba wenzetu wanapenda tuje au wanapenda tuwepo. Lakini kufuta tu halafu akaja akapewa mwekezaji mwengine, ni jambo la aibu kwa Serikali yetu ya Zanzibar.

Sasa kwa kweli haya mambo tunapofanya lazima tutumie busara. Lakini si hiyo tu katika awamu hiyo hiyo, Serikali ya Oman ilipewa kiwanja pale Forodhani. Kwa bahati nzuri inawezekana kwa sababu za msingi uwanja ule ukafutwa awamu ya sita.

Matokeo yake Serikali ya Oman ikapewa sehemu nyengine badala ya pale. Ni jambo zuri na la hekma labda kuna sababu za msingi au labda kuna sababu za usalama. Lakini hapo walipopewa tayari kuna wapangaji mule ndani. Sasa unaiambia Serikali ya Oman, sehemu hii nimekupeni. Sasa ni jambo la aibu

sana. Tungefanya sisi utaratibu wizara inayohusika au serikali tungeliwaondosha wapangaji wale, halafu tukawapa nyaraka Serikali ya Oman kuwaambia kwamba pale tayari kuna eneo halikuwa na mzozo.
Lakini tunakwenda kuwapa sehemu tayari kuna wapangaji. Sasa kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, hapa tunaonekana ni watu ambao wamekuja wanataka kuleta vurugu wapangaji wanataka kutolewa. Sasa mimi ninafikiri katika masuala kama haya maamuzi ya nchi kutokana na urafiki, kwa sababu hata katika bajeti ya Wizara ya Fedha iliyosomwa katika nchi ambazo zilizoshukuriwa na Serikali na Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa na Oman imo kwa mchango wao mkubwa kwa Zanzibar.

Kwa hivyo mimi naona Mhe. Mwenyekiti, mambo mengi katika masuala mazima haya ya ardhi, kuna viwanja ambavyo wawekezaji wana waraka, halafu anakuja Waziri wa kwanza, Waziri wa pili huyo wa CCM naye akatoa waraka wake.

Mimi ninafikiri Mhe. Mwenyekiti, imefika wakati maslahi ya Zanzibari tuwekeni mbele. Jamani hili suala la hapa pangu basi tena kwa Zanzibar. Tuliacheni maslahi ya nchi tuweke mbele kwa faida ya Wazanzibari, ya watoto wetu na wajukuu zetu. (*Makofi*).

Kwa hilo niliona kwamba nitoe mchango wangu na busara zangu kwa wizara inayohusika katika suala zima la usajili wa ardhi kwenye ukurawa 11 na 12.

Lakini vile vile niendelee kwenye suala la Mamlaka ya Maji ambayo ni *page* 42 mpaka 43. Kweli Mhe. Mwenyekiti, kwamba hali ya uchumi bado ni changa kwa Zanzibar lakini vile vile suala la maji ni suala muhimu sana.

Mimi kwa ushauri kwa Mamlaka ya Maji kupitia wizara lazima tuwe tunaamua mambo ambayo yenye msingi na muhimu kwa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba hasa suala la maji. Ninafikiri suala la maji ni suala muhimu sana. Mhe. Mwenyekiti, nime-*experience* katika kipindi kifupi na ningelishauri wizara inayohusika kwamba tumo ndani sote humu kwa sababu ya maslahi ya nchi na maslahi ya wananchi ndio waliotuweka madarakani, tuliokuwemo humu ndani.

Suala la maji lisiwe ni suala ambalo la kawaida. Mhe. Mwenyekiti, nimeshuhudia nilipoteuliwa tu kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini kwa mfano, eneo la Umbuji kulikuwa maji yapo mengi, umeme upo kulikosekana *pump* yenye thamani isiyopungua shilingi milioni nane.

Nilipoingia mimi Mamlaka ya Maji nikawaambia jamani hebu niambieni, wakasema Mhe. Raza hapa kuna matatizo ya maji. Sasa nikawaambia

nikupeni pesa muagizie hiyo *pump*, kwa sababu tunazungumza maslahi ya kero za wananchi. Ninashukuru Mamlaka ya Maji kwa kushirikiana wakaliona hilo na likafanikiwa.

Lakini miaka miwili sasa katika miaka miwili hiyo hiyo inaweza kuwa Waziri au watendaji wameshatumia kwa kusafiri kwenda nje ya nchi zaidi ya shilingi milioni mia, lakini wananchi wamekosa maji kwa milioni saba tu. Ushahidi huu ninao. Wizara inayohusika inaweza kutumia zaidi ya shilingi milioni mia lakini wananchi wanaweza kuwa wa Micheweni, Makunduchi, Nungwi, Waumbuji wamekosa *pump* ya shilingi milioni kumi au nane.

Sasa mimi ninafikiri Mhe. Mwenyekiti, ningeliomba Wizara inayohusika, safari zisizokuwa za lazima, zenye tija ziondoshwe. Kama kuna masuala ambayo yanayohusiana na masuala ya mambo ya maji katika visiwa vyetu na hasa katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani, na mara ndio sote sisi tunatarajia angalau tuwaondoshee shida wananchi katika masuala ya maji. Tujipange tuone jinsi gani suala la maji, kwa sababu ninaamini maji yapo ya kutosha. Ni mipangilio tu na utaratibu mzima katika kusambaza maji.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeshuhudia kwamba wakati panapokuwa na safari za nje kwa viongozi au watendaji, pale Wizara ya Fedha panakuwa hapatoshi, mtu anaweza kufika mpaka usiku saa nane anataka kusafiri tu, apate posho tu tiketi. Lakini katika suala linalogusa wananchi maji hana habari nalo, tena ukimwendea anakwambia sehemu gani, sina taarifa.

Sasa kwa kweli hili na haya yote nina ushahidi nayo. Sasa kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, ningeliomba Wizara hii tumefika hapa sote tumekula yamini kwa jina la Mwenyezi Mungu, kwa imani ya Uislamu na wasiokuwa Waislamu. Waislamu tumekamata msahafu humu ndani kwamba tutaitumikia nchi hii kwa taratibu za nchi. Lakini ninasema lazima tuwe wakweli katika kusaidiana masuala ya maji na masuala ambayo yanagusa wananchi kila siku.

Kwa hivyo mimi fikra zangu, mawazo yangu kwa wizara inayohusika, panapokuwa na matatizo ya maji, wazitolee taarifa katika vyombo vinavyohusika kwamba kuna suala hili la maji. Kama sisi wadau tuiteni. Mimi ninashukuru Mamlaka ya Maji nimekuwa karibu, tuiteni tuelezeni. Lakini huwezi kuniambia kuna tatizo la maji la shilingi milioni nane au kumi au kumi na tano unasema halina bajeti. Lakini viongozi katika mwezi huo huo wakaondoka mara nne. Sasa bajeti ile iondoshwe kule ipelekwe kwenye maji.

Kwa hivyo mimi ningeliomba Mhe. Mwenyekiti, wizara inayohusika ninaipongeza lakini tuwe na hekma na busara katika kuwatumikia wananchi katika suala hili. Lakini vile vile bado tuweze kuwatolea elimu kwa wananchi

katika kulipa vile vile huduma za maji, kwa sababu wizara hii ni changa, tunatakiwa sisi kama Wawakilishi tutoe huduma kwa wananchi, ili wananchi waweze kuchangia pale maji yanapoweza kupatikana.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo ninalokuja nalo ni suala ambalo linahusiana na mafuta au nishati. Tumeshuhudia mara nyingi kumekuwa na upungufu wa mafuta. Sasa kitu kinachonipa taabu Mhe. Mwenyekiti, upungufu wa mafuta unapokuwa haupo Zanzibar na wakaazi wengi wanaishi mbalimbali hasa wafanyakazi wa serikali na wananchi wa kawaida kufuata huduma zao katika mambo mbalimbali ya shughuli ya mafuta, wakulima, wananchi wa shamba na nini.

Sasa kitu kinachonipa taabu, nimeshuhudia mara moja au mbili. Mhe. Mwenyekiti, tunamshuhudia Makamo wa Kwanza wa Rais au wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Alhaji Seif Iddi anakwenda kwenye vituo kushuhudia kuwapa pole wananchi wakati wizara inayohusika wala haina habari na jambo hili. Ni jambo la aibu sana hili, wizara inayohusika haina habari kabisa kama Zanzibar kuna matatizo ya mafuta.

Inatoka afisi ya Makamo wa Pili wa Rais au inatoka Ikulu inatoa tamko suala la mafuta kumekuwa na upungufu mkubwa. Sasa hii wizara ipo wapi, waziri yupo wapi, anatoka Makamo wa Pili anakwenda kwenye vituo. Serikali kupitia Wizara ya Fedha ndio inayotoa kauli kuhusu kuwataka radhi wananchi, upungufu wa mafuta na kuna wizara inayohusika.

Sasa kwa kweli mimi ninafikiri tuwe na majukumu kwa sababu uongozi ni utumishi, uongozi si ubwana katika nchi yetu. Tumekuja kuwatumikia wananchi na sisi sote ni watumishi wa wananchi. Kwa hivyo ningeliomba wizara inayohusika katika masuala haya wawe karibu na wananchi katika suala zima hili la mafuta kwenye kutoa taarifa, na kama kuna upungufu wa kusaidia kwenye vyombo vya habari, mimi nipo tayari kuchangia, angalau wananchi wapewe habari kwenye vyombo vyetu, katika kutangaza kama kuna matatizo.

Lakini tunamuachia Makamo wa Pili wa Rais anatembea, tunaachilia Ikulu itoe tamko. Sasa Wizara imekaa. Mimi ninafikiri tufike wakati uwajibikaji uwepo katika suala zima la nchi yetu. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika 5 za ziada.

Mhe. Mohamedraza Hassanali: Mhe. Mwenyekiti, basi naomba niishukuru wizara, lakini ninachosema jamani ninasisitiza maslahi zaidi ya nchi tuwekeni mbele. Suala hili la maji mimi sijaliona kubwa sana, kweli tuna matatizo mengi katika sehemu yetu lakini tuwe karibu katika kutatua matatizo ya maji.

Mimi ninafikiri kama tutakaa tukajipanga *what's next* tunaweza tukafanikiwa kuwatumia hawa hawa watu wafadhili. Panapokuwa na upungufu tuiteni wizara inayohusika ili kuona tunaweza kusaidiana katika masuala haya.

Lakini vile vile ningeliomba wizara inayohusika haya mambo ambayo yamekuwa yamefanyika wangelipitia kwa njia zao kwa kuwasiliana na nchi zilizohusika kwa usumbufu walioupata, angalau tukaiweka nchi yetu katika njia iliyokuwa ya hekma na busara. Kwa kweli inasikitisha sana, na hili suala la *documents* zikapandiana na Waziri mmoja au wawili Mhe. Mwenyekiti, linatuletea matatizo makubwa sana. Tumeambiwa hapa kwamba kesi zipo nyingi mahakamani, na inafika serikali wakati mwengine ikadaiwa mabilioni kwa mtu mmoja tu. Matokeo yake tukaharibikiwa sote, bado Zanzibar ni yetu sote, Zanzibar ni *cosmopolitan*. Mimi ninafikiri tujenge mashirikiano na bado hatujachelewa ili kuona matatizo na kero za wananchi katika visiwa vya Unguja na Pemba zinaondoka. Ni imani yangu kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu hasa suala hili la maji na mambo mengine yataondoka.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia mimi na nyinyi wenzangu nyote na wewe Mhe. Mwenyekiti, tukiwa hai na wazima wa afya, tukiendelea hapa kujadili masuala yanayohusu nchi yetu na watu wake.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii nimshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri kwa bajeti aliyotuletea leo, haidhuru mzee wangu ninamuheshimu Mhe. Waziri, watendaji wake kidogo wamemuangusha, kwa sababu nikiangalia hiki kitabu kilivyokuja leo cha kwanza ambacho kimejaa vikaratasi ndani. Sasa kidogo hii haileti picha nzuri, kama vile watu waliokuwa hawakujipanga vizuri. Nilikuwa naomba hili walizingatie Mhe. Waziri wa wizara, ni mmoja wa mzoefu sana. Mhe. Mwenyekiti, ninadhani ni mmoja wa Waziri anayeongoza ni Waziri muandamizi ndani ya Baraza hili, kwa hivyo watendaji wasimuangushe. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hatuna muda naomba niseme moja la jumla kwa sababu nikenda katika kifungu kimoja kimoja nitauchukua muda mwingi sana. Lakini nimuombe tu Mhe. Waziri akija anisaidie bado hoja yangu ipo

pale pale. Nikiangalia kifungu vilivyokuwa katika matumizi bado maeneo yale yale katika kila wizara.

Fungu la posho maalum, posho la kamati na vikao, safari za nje, viburudishaji, *stationery*. Ninasema mafungu haya kila pahali yamenona kupita kulinganisha mwaka jana na mwaka huu. Kama walivyosema Waheshimiwa Wajumbe wengine hapa inasikitisha Mhe. Mwenyekiti, kwamba katika yale maeneo ambayo tungetegemea kwamba kuna huduma, badala ya kuona kule ndiko kunakoekwa *priority, cash priority*.

Kila pahali fungu la safari limenona kupita kiasi Mhe. Mwenyekiti. Imekuwa *priority* ya watendaji ni kusafiri tu Mhe. Mwenyekiti, badala ya kuwahudumia wananchi. Hili sisi kama Wawakilishi hatuwezi kulikubali Mhe. Mwenyekiti. Nilikuwa ninamuomba Mhe. Waziri sitaki kwenda kulisema moja moja kwa sababu ni mengi, naomba azipitie kwa jumla hizo idara zake mbali mbali aje anipe maelezo.

Lakini katika vifungu Mhe. Mwenyekiti, lipo moja hili naomba nilitaje *specifically*. Kama nilivyosema vifungu hivi Mhe. Mwenyekiti, mimi nikiwa sikupata maelezo ya kutosha nitavizuia wakati wa kuja kupitisha vifungu, ninatao indhari na mapema Mhe. Mwenyekiti.

Lakini moja imenishitua zaidi Mhe. Mwenyekiti. Katika kitabu hiki cha makadirio ya mapato na matumizi, ukurasa wa 389 kuna Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba, *vote* 0302 imeombewa shilingi milioni saba, chini ya maelezo ruzuku kwa ajili ya uendeshaji.

Lakini halafu ukurasa wa 406 wa buku hili hili, tena kuna *vote* yenye nambari tofauti 1102 bodi ya kudhibiti kodi za nyumba, maelezo ruzuku kwa ajili ya uendeshaji shilingi milioni 30. Sasa nashangaa vipi una taasisi moja ndani ya wizara moja ina *vote* mbili tofauti, zenye maelezo sawa sawa lakini zinaombewa mafungu mawili tofauti Mhe. Mwenyekiti, kuna mchezo gani katika wizara hii hapa, nilikuwa naomba hili Mhe. Waziri akija atusaidie sana. Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kama nilivyosema kupitisha matumizi ambayo hayana maelezo ya kina.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo naomba niingie katika baadhi ya sekta mbali mbali ambazo ziko katika usimamizi wa wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nizungumzie kuhusu mipango miji. Mhe. Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana kwamba miji yetu nafikiri inaongoza kwa kujengwa ovyo katika ukanda huu wa Afrika. Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha kwamba tumetoka katika hali nzuri, badala ya kwenda mbele katika zama za sayansi na teknolojia sisi tunarudi nyuma.

Mhe. Spika, ukitembelea mitaa ya asili hapa iliyojengwa, ukiondoa Mji Mkongwe ambao umekutwa vile vile na hali yake na kuna kitabu kizima, kuna mwandishi mmoja kaandika jinsi Waingereza wenyewe walivyokwama kujaribu kurekebisha kutokana na ujenzi wake. Lakini kuna mitaa ya ng'ambo Mhe. Mwenyekiti ni mizuri tu. Ukenda maeneo ya Kidongochekundu kama unataka kuja Skuli ya Jang'ombe mitaa ile imepangika vizuri kabisa, ukenda Miembeni mitaa imepangwa vizuri kabisa, ukenda Kwahani pia kumepangwa vizuri sana. Lakini hii miji tuloanzisha sisi sasa hivi, njoo Bububu kila mtu katoa mlango kwake, nyumba imemzidi huyu kwa nyuma na hii imemzidi huyu kwa mbele ni *shaghala baghala* Mhe. Mwenyekiti, hali hii haivutii hata kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hali kama hii hata tukenda katika utoaji wa huduma kwa serikali hiyo hiyo kwa wananchi, pakiingia moto inakuwa mashaka, tukitaka kupeleka huduma za maji, tukitaka kutandika waya mule chini mashaka kwa sababu ya ujenzi uliokuwa hauna mpango. Lakini hata haiba ya nchi yetu na miji yake inapotea. Kwa hivyo, nilikuwa naomba niambiwe kwa nini tunaendeleza hali kama hii. Moja limetajwa hapa kwamba kuna taasisi nyingi zinasimamia.

Kwa mfano, maeneo ya mjini Baraza la Manispaa linaingia hapa, ukija Mji Mkongwe kuna mamlaka ya hifadhi ya Mji Mkongwe yako hapo, ukija huku kuna wizara inahusika. Kuna mambo mengi, kuna tawala za mkoa mbali zinaingia upande wake. Kwa hivyo, nilikuwa nasema Mhe. Mwenyekiti, hili ni eneo moja ambalo nilikuwa nataka Mhe. Waziri aje atuambie, tuna tatizo gani katika usimamizi wa suala hili la mipango miji. Tunaweza tukaambiwa *master plan* iliyokuwepo haifai tena imepitwa na wakati, lakini si angalau ipo. Je, hii iliyokuwepo inasimamiwa na kutekelezwa, kuna tatizo gani katika hili Mhe. Waziri naomba akija anisaidie.

Mhe. Mwenyekiti, naomba vile vile nizungumzie suala la mamlaka ya maji, kama walivyozungumza wajumbe wote. Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi nasema kuwa Mji Mkongwe ndio eneo linaloongoza kwa kuchangia mapato nchi hii, kwa sababu biashara zote ziko pale, hoteli kubwa ziko pale na matumizi makubwa ya mji yote yako pale. Lakini baadae hatuoni huduma zikiletwa Mji Mkongwe. Waziri aliyepita Mhe. Ali Juma Shamuhuna kabla ya kuteuliwa mzee wangu Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, nilikuwa nikiwasiliana na wala nilikuwa sipigi kelele hapa, nikiwasiliana naye kimya kimya juu ya suala la vipi kuiongezea nguvu huduma ya maji katika Mji Mkongwe. Akaniambia kuna kisima kipya kinachimbwa kitaongezea kima cha maji ambacho kinakuja Mji Mkongwe. Lakini bado wananchi wa Mji Mkongwe wanapiga kelele sana kwamba kuna tatizo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Jaku Hashim hapa ukija kwenye majumba yale ya maendeleo ndio kabisa, imekuwa maji kupanda juu watu wamesahau kabisa. Mtu anatumia mashine yake na umeme wake na bado anaambiwa alipie huduma ya maji Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo nilikuwa naomba Mhe. Waziri akija anisaidie.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala ambalo limetajwa humu la mpango wa kuanzisha sheria ya Shirika la Nyumba. Mimi nataka nimpongeze hatua hii na nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuja na hatua hii. Lakini nimeona katika maelezo yake zaidi kajikita katika kungojea wawakezaji ambao wanataka kuja kuwekeza katika mradi wa ujenzi wa nyumba na baadae kuziuza kwa utaratibu maalum kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna uzoefu katika nchi nyengine kwamba ukiunda shirika kama hili, lenyewe linatafuta mikopo katika taasisi mbali mbali za kifedha duniani. Linaingia kwenye utaratibu ambao kwanza wanajenga halafu kwa utaratibu ambao umezoeleka, mwananchi anaweza kuuziwa akawa analipa kwa awamu na hatimaye nyumba inakuwa yake, huo ndio utaratibu mzuri wa kuwawezesha wananchi wetu wengi ambao ni maskini kuweza kumiliki nyumba. Hasa kwa upande wa wafanyakazi wa serikali ambao wana mapato yanayoeleweka kupitia katika mishahara yao, inaweza ikatumika ile kama ni ya uhakika ili kuweza kudhamini ulipaji wa kulipa kidogo kidogo na hatimaye kuweza kumiliki nyumba.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka kulizungumza ni hili la bodi ya kudhibiti kodi za nyumba. Mhe. Mwenyekiti moja kati ya mambo ambayo yanaziathiri sana nchi zetu hizi, ni kwamba hakuna utaratibu wa utawala wa sheria kila mtu anafanya lake. Mhe. Mwenyekiti, katika nchi ambazo watu wake ni maskini kama zilivyo nchi zetu, utaratibu uliozoeleka sasa wa kwamba kila anayetaka kukodisha nyumba yake, basi anakuambia umlipe kwa mwaka mzima au umlipe kwa miaka miwili. Kwa kweli unawadhalilisha na kuwanyanyasa sana wananchi wetu maskini. Kwa hivyo, inaonekana hatuna utaratibu wa kisheria wa kuwafunga watu hawa Mhe. Mwenyekiti. Bahati mbaya hata serikalini wamechukua mfumo ule ule, hata nyumba za serikali ni hivyo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, mtu ambaye mshahara wake ni shilingi laki moja na ishirini na tano elfu kwa kima cha chini, unapomwambia alipe kodi kwa mwaka nzima au miaka miwili, je ataweka kiasi gani kuweza kuhudumia familia yake. Lakini pengine ungemuwekea utaratibu mzuri huyu wa sheria ya kumlinda, basi ingekuwa inawezekana kuwa analipa kidogo kidogo, ndio pesa ya maskini Mhe. Mwenyekiti, ili aweze kupata pesa ya kuweza kuhudumia

familia yake. Lakini hatuna utaratibu wa kisheria tuliouweka katika hilo, kwa hivyo, kila mmoja anafanya anavyotaka. Mwengine anakuambia ulipe kodi ya miaka mitatu. Nilikuwa nadhani suala hili hebu serikali iliangalie, je hakuna haja ya kuwa na sheria kwa kupitia hii bodi ya kudhibiti kodi za nyumba. Isiwe kudhibiti gharama tu za kodi, hata hiyo sidhani kama inafanywa ipasavyo, kwa sababu mtu anaweka kodi anavyotaka yeye, lakini hata ule ulipaji wenyewe Mhe. Mwenyekiti. Tuwatizame wananchi wetu ni maskini na wanyonge.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Mamlaka ya Mji Mkongwe, pamoja na changamoto nyingi walizonazo, mimi nataka kuwapongeza wanajitahidi Mji Mkongwe umebakia kuwa vile ulivyo kwa kiasi kikubwa, kwa sababu bado wanajitahidi kusimamia sheria, lakini bado kuna malalamiko ambayo niliwahi kuyasema katika Baraza hili hili Mhe. Mwenyekiti, kwamba kuna baadhi ya watu inaonekana kuna *double standard.* Mwananchi maskini akitaka kufanya marekebisho madogo tu, basi hiyo tabu anayopatishwa katika Mji Mkongwe ni kubwa kweli kweli. Lakini mtu mwenye chake akija, basi sheria ya Mji Mkongwe inasema usijenge zaidi ya ghorofa tatu, lakini yeye anajenga ghorofa nne hoteli *bukheri wa khamsa ishirini* hakuna anayemfuata. Suala hili niliwahi kulizungumza na kuna nyumba pale Shangani, mfano hai upo, pale karibu na ilipokuwa Skuli ya Shangani zamani.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nasema wananchi wanalalamika kwamba sisi wananchi mtu anaweza kutia kiji-*canopy* au kiji-*tiles* tu basi anaweza kuingiliwa, akachukuliwa hatua na pengine hata akavunjiwa, lakini wale wenye mapesa yao wanaweza kufanya wanavyotaka akaachiwa. Kwa hivyo, mimi nasema pamoja na kazi hiyo wanayotufanyia tunawashukuru, lakini haya maeneo Mkurugenzi Mkuu awatazame watendaji wake. Mkurugenzi Mkuu anaweza kuwa anafanya kazi vizuri, lakini watendaji wake awatazame, kunazungumzwa sana suala la rushwa katika ofisi hii Mhe. Mwenyekiti katika utendaji wake, na kwamba hiyo inaathiri utendaji wake na katika kuwahudumia wananchi kwa usawa.

Hao hapo Mhe. Mwenyekiti, nizungumze jambo ambalo lilitajwa katika hotuba ya Mhe. Waziri, suala la milango ya chuma. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli wananchi wengi wa Mji Mkongwe wanapiga kelele katika hili, na mimi kama Mwakilishi wao wamewahi kuniambia. Kwamba kuna tatizo la kuzuka tu sheria, miaka yote watu katika kujihifadhi na uhalifu na sio Mji Mkongwe na takriban nchi nzima sasa tumejifungia kwa mavyuma na mageti hata likitokezea balaa la moto hujui ufanye nini, yote ni kwa sababu ya kutafuta usalama. Unakuwa hata hufikirii ikitokezea dharura itakuwaje, wewe unaangalia suala la uhalifu. Kwa hivyo, kama kungekuwa katika hali ya usalama sidhani kama mwananchi angependa hii gharama ya kufanya milango

na madirisha ya vyuma akajikomelea mule ndani, kwa sababu hata ile haiba ya nyumba yenyewe inapotea. Lakini watu wamegharamika kutia milango ile, halafu ghafla kunakuja agizo kwamba milango ile iondoke na iingie kwa ndani.

Kwa hivyo, kuna gharama pale na wananchi wa Mji Mkongwe wa leo, sio ule Mji Mkongwe wa Ibn Khuzaimat Ibn Mudrikat Ibn Ilias, sio ule. Mji Mkongwe wa leo wale wanaokaa mule ndani maskini za Mungu, sasa unapomwambia kila siku abadilishe ni kweli kuna gharama pale Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, nilikuwa nasema hilo walitazame sana, kama serikali imeamua kuja na utaratibu huu basi ingekuja na ruzuku namna gani ya kuweza kuwasaidia wananchi ili kufanya hayo marekebisho ya kutoa mlango wa chuma nje na kuutia ndani kama unavyotakiwa. Lakini kila siku mkitaka yeye kumfanyia masheria mapya kila siku na kila siku atoe gharama. Mhe. Mwenyekiti, hili sio kuwatendea haki wananchi wetu maskini wanyonge. Namuomba Mhe. Waziri akija katika suala hili anisaidie.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala hili hili la Mji Mkongwe limezungumzwa la maeneo ya wazi, naomba katika hii wizara iwe makini na iwe na msimamo kwenye kusimamia ujenzi katika maeneo ya wazi. Leo miji yetu na maeneo yetu yote yanakosa kila eneo la wazi linachukuliwa, na mtu anajenga kwa sababu tu ana uwezo wa kifedha, na kwa sababu Mji Mkongwe ndio *capital* ya nchi, hivyo kila mtu anakimbilia hapo na kila kichochoro kinataka kujengwa. Matokeo yake leo watoto wetu wataishia kuzunguka majumbani, hakuna hata pahala pa kuweza kupumzika mtu akacheza, kote Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, nilikuwa nasema suala hili tulione kwa vitendo, tusisikie maneno tu kila siku, tuone kama kweli maeneo ya wazi yanahifadhiwa na yanalindwa, sio mtu mwenye uwezo wake anakwenda kuchukua eneo la wazi anajenga.

Mhe. Mwenyekiti, suala la *traffic plan*, Mhe. Jaku Hashim Ayoub alilizungumza vizuri sina haja ya kuliongezea. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nimejitahidi nichangie haraka ili nipate muda wa kutosha, nataka kuzungumza suala moja kubwa kwa muda wangu uliobakia. Suala linalohusu Idara ya Nishati hasa suala la uchimbaji na utafutaji wa mafuta Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana niliamua kutumia muda wangu wote wa kuchangia wizara hii kwenye suala la mafuta na nikawataka radhi wapiga kura wa Mji Mkongwe, kwamba sitoyagusia masuala mengine ambayo yanawahusu maisha yao ya kila siku, ili nizungumze suala kubwa linalohusu nchi yetu. Tukavutana sana hapa Mhe. Mwenyekiti, tangu kwenye bajeti kuu, tukaja mpaka kwenye bajeti ya wizara, ninazo *Hansard* hapa. Lakini hatimaye tukaambiwa tuipe muda serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu lilijitokeza mara kwa mara katika kikao cha mwaka jana, hatimaye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, tukamuuliza je, tuipe muda gani serikali ili itupe maamuzi katika hili. Akatuambia tupeni mwaka mmoja. Mhe. Mwenyekiti, nataka kuipa taarifa serikali mwaka mmoja umekwisha. Ni bajeti ya mwaka jana mpaka bajeti hii.

Lakini zaidi Mhe. Mwenyekiti, ile hekima, busara na uungwana wa Wazanzibari unatumiwa vibaya na ndugu zetu wa damu. Hili mimi sichoki kulisema Mhe. Mwenyekiti, nionekane mbaya, kama kutakuwa na mambo ya ulimboka au mambo ya nini, maana yake siku hizi Tanzania imechafuka, watuletee tu, lakini hatutoacha kusemea mambo yanayohusu haki za nchi yetu na haki za wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama mmeamua suala hili kwamba lisimame, basi tutegemee lisimame kote, mpaka hapo tutakapofanya maamuzi. Lakini sisi tunaambiwa subirini na wenzetu wanaalika kampuni kila siku wanaingia mikataba na kuanza kuchimba. Mhe. Mwenyekiti, katika ukanda wa Mtwara pale kwenye eneo linaloitwa Zafarani wameliita jina hilo, kwanza utafiti wameshaanza kuchimba gesi, ile hatua ya mwanzo katika kisima cha kwanza tu wamepata gesi *one trillion cubic feet*. Futi za ujazo trilioni moja ya gesi. Mpaka juzi zinasomwa ripoti za mwisho wameshafikia mpaka trilioni tatu futi za ujazo gesi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mambo haya yako hapo kwa ndugu zetu wa damu, ukiteremka chini huko Msumbiji wana kitu hicho hicho. Sasa mambo haya yana ushindani wa kibiashara Mhe. Mwenyekiti. Sisi tunaambiwa subirini, lakini wenzetu wanaendelea na katika kuendelea huko wanasomesha watu wao na wanapata fursa chungu nzima. Wanajiandaa na kujijengea uwezo, sisi tunasubiri tu Mhe. Mwenyekiti. Tutakuja kutahamaki wakati tunasema sasa tuanze wenzetu wameshatutangulia huko katika maandalizi, kwa hivyo hata ule ushindani hata mkiruhusiwa nyinyi mmeshaachwa nyuma, hii si haki kwa Zanzibar wala si haki kwa Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwaka jana tuliombwa muda mwaka mzima umeshapita, ule muda ulioomba serikali umeshamalizika. Lakini Mhe. Makamo wa Pili wa Rais aliiongoza timu ya mawaziri wakenda katika hivyo vikao vya mashauriano visivyokwisha, wakaambizana tena kwa lugha kali. Mimi nawakubalia kwamba mawaziri wetu au serikali kwa jumla wanatumia lugha kali kipindi chengine hata kuliko wenzetu. Lakini lugha kama haina utendaji Mheshimiwa, haina maana. Wakauliza wao, imeripotiwa ndani ya magazeti, wakauliza tukupeni muda gani ili suala hili lipate ufumbuzi.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakawajibu tupeni miezi minne. Hiyo miezi minne ilikuwa inamalizika mwezi wa Mei Mhe. Mwenyekiti, na sasa hivi tuko mwezi wa Julai, hakuna kitu.

Wenzetu Mhe. Mwenyekiti, hawana nia njema katika hili. Sasa Mhe. Mwenyekit, nasema na tuliwaambia hapa mara nyengine kuchukua maamuzi magumu kunasaidia, hata huyo aliyekuwa anakuzuilia haki zako akuheshimu na aachie haki yako. Mwaka jana tulisema Mhe. Mwenyekiti, kwamba serikali ilifikia hatua ya kuandaa rasimu, na mimi ninayo hapa ya mwaka 2009. Ilifikia hatua ya kuandaa rasimu ya sheria ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta Zanzibar. Baada ya maamuzi ya Baraza hili, chini ya Mhe. Spika wetu Mhe. Pandu Ameir Kificho, kufanya maamuzi ya msingi wakati wa Serikali ya Awamu ya Sita, nataka nimpongeze sana Mhe. Rais Amani Abeid Karume, katika Rais ambaye kaweka historia ya uzalendo katika nchi hii na kupigania haki za Zanzibar, ataingia katika historia. Walifikia hatua wakaliongoza Baraza hili kwa maamuzi mazito, Baraza hili likapitisha maamuzi kwamba liondolewe. Baraza hili halina mamlaka ya kuondoa, lakini likapitisha maamuzi kwamba liondolewe. Lakini hawakumalizia hapo wakachukua hatua ya kuandaa sera ya nishati ambayo leo Waziri katuambia anataka kuingia katika utekelezaji. Wakafika hatua ya kuandaa rasimu ya mswada wa sheria, lakini baadae mambo yamekwama.

Sasa mwaka jana Mhe. Mwenyekiti, nilikuja nikasema tunasita nini kupitisha sheria yetu, tunayo ile ya mwaka 1951 na mimi naendelea kuitetea mpaka kiama kwamba sheria ile bado inafaa, lakini anasema tuache. Hii ya rasimu iliyoandaliwa tunashindwa nini kuileta hapa Barazani ikapitishwa, tunashindwa nini kutekeleza azimio jengine la Baraza kwamba tulete sheria ya kuanzisha mamlaka ya utafutaji na uchimbaji mafuta Zanzibar, *Zanzibar Petroleum Development and Authority*, tunashindwa nini.

Tuliambiwa mwaka jana Mhe. Mwenyekiti, kwamba ni kwa sababu, hata tukizipitisha kuna kampuni kubwa huko bado zitakuwa hazitambui kutokana na mzozo wa kikatiba. Mimi nakubali. Lakini nasema katika kuweka shinikizo na kama tutaamua kimsingi, wameshakubaliana kwamba suala hili liondolewe. Juzi Mhe. Waziri Mkuu Bungeni kasema kule, basi hatua hizi zianze sasa Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, katika hili mimi nasema kwenye kifungu ambacho nitakizuia mwaka huu na patachimbika Baraza la Wawakilishi, kama hatutakuwa na pa kukaa na tusipate pa kukaa kwa kuchimbika humu ndani. Lakini suala hili Mhe. Mwenyekiti, hili kama kupiga kura tutapiga atahesabiwa mzalendo wa Zanzibar nani hapa na msaliti wa Zanzibar atajulikana nani. Kama kuheshimu kauli ya Mwanasheria Mkuu iliyotolewa

mwaka jana Mhe. Mwenyekiti, kwamba katika kusimamia haki za Zanzibar ni muhimu serikali, Baraza la Wawakilishi na wananchi wa Zanzibar waonekane wako pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili naiomba serikali, mwaka jana tuliikubalia, mwaka huu tukubali Wawakilishi twende pamoja tukubali azimio la kuleta sheria hizi mbili. Kama serikali haikuleta. Mimi tukijaaliwa natoa taarifa rasmi hapa, kama serikali itang'ang'ania msimamo wake, na kama Baraza hili likiwa halikuridhia ninayoyataka, basi mimi tukijaaliwa, kwa sababu kazi nimeshafanyiwa mswada si huu ninao. Kikao cha mwezi Oktoba nitaleta taarifa ya kuleta mswada binafsi wa Mjumbe wa kuipitisha sheria hii Baraza la Wawakilishi lifanye maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi tena kukubali kunyanyaswa, tumeingia katika Muungano kuwa wabia wa Muungano, sio watumwa wa Muungano Mhe. Mwenyekiti. Sisi sio watumwa wa Muungano ni wabia, na leo wananchi wanataka kufanya maamuzi hata katika hili. Sasa nasema hili hatuwezi kukubali tena.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kidogo katika suala hili. Kama nilivyosema nitazuia kifungu. Katika hilo hilo la wenzetu kwamba sisi tusubiri wao wanaendelea. Mhe. Mwenyekiti, kuna ramani mbali mbali kuhusu masuala haya ya mafuta. Hii hapa ramani inayoonesha *blocks* mbali mbali katika ukanda wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hii ndani ya visiwa vya Zanzibar. Hii haina matatizo. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hii ukiipata ramani kisawa sawa vitalu au kwa lugha zilizozoeleka kuitwa *blocks* za Zanzibar ni kuanzia *block* nambari 8, 9,10,11, na 12 viko katika maeneo ya Zanzibar, vinafika mpaka Fungumbaraka ambalo ni eneo la kisiwa hiki.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tumezowea kuaminishwa na sisi kama kawaida kwa sababu ya hekima, busara, uungwana na ustaarabu maana tunapata kusifiwa kwa hayo Wazanzibari huku yetu yanachukuliwa tu. Tumeaminishwa kwamba *blocks* za Zanzibar ni 9, 10, 11 na 12. Lakini *block* nambari 8 katika ramani hii inaonekana wazi wazi kwamba iko katika eneo la Zanzibar. Sasa sisi tunasubirishwa na 9,10,11 na 12 wenzetu wametia saini na kampuni ya *Petrol Brass* kwenye block nambari 8 nani kawapa mamlaka hayo na wakati suala hili linasubiriwa maamuzi. Sisi tumewekwa *chenisi* tusubiri, wenzetu wanakula *kizigo* katika karata. Wacheza karata mnakumbuka kuna kile kizigo, anakuja mwenzako anakuwekea nambari anakichukua chote bila kufanya kazi yoyote, tena hufanyika katika hili Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitongoja tukaliwa kizigo, baada ya kuwa nimeshafanya kazi ya kuvuna mpaka kizigo kimejaa akaja mmoja na karata moja akakichukua kizigo chote, mimi sitokubali Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, nasema hili nahitaji maelezo kutoka kwa waziri na serikali kwa jumla. Kwa nini mpaka leo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko kimya juu ya aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini Mhe. William Ngeleja kusaini kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mkataba juu ya block nambari 8 na Kampuni ya *Petrol Brass*, wakati eneo hili katika ramani hii liko wazi kwamba liko katika Zanzibar.

Je, tuiambie serikali hii Mhe. Mwenyekiti, kwamba inashindwa kusimamia yale maamuzi ya msingi yaliyofanywa na serikali ya awamu ya sita. Mimi sitokubali heshima waliyoiweka kina Mhe. Ali Mzee walipokuwa katika Baraza hili na wengine waliokuwemo katika Baraza lililopita. Heshima waliyoiweka katika kupitisha maamuzi mazito ya Zanzibar, chini ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Mhe. Rais Mstaafu Mhe. Aman Abeid Aman Karume. Leo Baraza hili ambalo sasa mimi ni Mjumbe nionekane kwamba niko dhaifu mbele ya Mhe. Ali Mzee Ali sitokubali hilo. Mimi nataka Baraza hili liweke mfano kwamba linajenga juu ya msingi ambao kina Mhe. Ali Mzee Ali waliuweka katika maamuzi yale.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema katika hili tunataka maelezo ya kina, sheria hizi mbili zitaletwa lini, nasema kama hazitofanya kazi na zisifanye kazi, lakini tuzipitishe humu ndani, ipeleke ujumbe kwamba tumeshaamua sisi na nipate maelezo ya kina kuhusu *block* nambari 8. Kinyume na hayo Mhe. Mwenyekiti, nasema kabisa bajeti ya wizara hii sitoipitisha. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha na kutufikisha siku hii ya leo kwenye bajeti ya wizara ya ambayo ni wizara nyeti sana katika nchi yetu.

Pia nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote, jinsi walivyochambua vizuri katika kitabu hiki kwa *data* mbali mbali, pamoja na uzuri uliokuwepo lakini na makosa hayakosi. Kwa hivyo, nitapitia mule mwahala ambamo nahisi kwamba hapa niisaidie serikali kwa kutoa mawazo yangu au fikra zangu.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka 1964 hadi mwaka 1972 muasisi Marehemu Abeid Aman Karume, alijikita katika mambo mbali mbali katika nchi hii kuwaletea wananchi wake na kuwaondolea usumbufu mkubwa sana, ili kuona kwamba wananchi wale wawe kama wako kwenye *paradise.* Kwa kweli Mwenyezi

Mungu amrehemu huko aliko, Mwenyezi Mungu amechukua roho yake hana makosa, lakini *chema hakidumu*. Ingekuwa marehemu Karume yupo, basi kusingekuwa na uchaguzi miaka 50 kama alivyosema wa vyama vingi na sasa hivi tungekuwa katika *paradise Island*, kwa jinsi mwelekeo wake alivyokuwa anauelekeza marehemu Karume.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini nikalisema hili, kwa sababu Marehemu Karume aliwajengea wananchi wake nyumba kwa Unguja na Pemba, nitataja sehemu ndogo ndogo tu. Alianza kujenga nyumba Kikwajuni, Michenzani, Makunduchi, Bambi na Pemba akajenga Chake Chake, Wete na Kengeja, alizieneza nyumba ili kuhakikisha anawapa wananchi wake baadhi ambao hawajiwezi.

Lakini la kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, nyumba hizi ni *shaghala baghala*, nguvu zimepotea na kuna nyengine zimeuzwa, lakini kuna nyengine ukipita vijijini utazionea huruma kwamba ni nguvu za wananchi na hasa wale wachuma karafuu kutoka Pemba, zilitumika katika kujenga nyumba hizi.

Mhe. Mwenyekiti, tukitoka hapo kulikuwa kuna awamu mbali mbali. Awamu ya Mzee wangu Ali Hassan Mwinyi, awamu ya mzee wangu Marehemu Mzee Idrissa Abdul Wakili, awamu ya ndugu yangu Mhe. Salmin Amour Juma. Nyumba hizi kuna mtu mmoja tu alifanya kidogo katika awamu hizo zilizopita. Lakini hapa nichukue pongezi za pekee za kumpongeza Rais Mstaafu Aman Abeid Karume, kwa kuona kwamba ingekuwa ni dhambi kubwa sana, hata mzazi wake asingelala pahala pazuri, kama nyumba zile za Michenzani hakuzimaliza. Nampa hongera na Mwenyezi Mungu atampa fungu lake.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile wale watu ambao walivunjiwa alihakikisha anawarejeshea, pamoja na kwamba watu wengine wameshakufa, lakini wajukuu na vitukuu walikuwepo wamepata. Lakini sasa mimi nijiulize na nitamuomba Mhe. Waziri akija hapa anisaidie ni nyumba ngapi ambazo amezijenga Marehemu Karume na ngapi zimeuzwa, ngapi zimetengenezwa na ngapi ziko katika hali ngumu, ili niweze kujua.

Nije hapo hapo kwenye nyumba Mhe. Mwenyekiti, katika kisiwa chetu hiki cha Unguja, kuna nyumba zimeanza Daraja ya mbao, nyumba za serikali hizo, mzunguko wa kisiwa chote mpaka huku kwangu Mazizini, Mji Mkongwe, mradi zimeenea nyumba nyingi tu za serikali. Lakini la kushangaza na tumerithi majengo mengi, la kushangaza ni kwamba matengenezo hatuzifanyii, zile tulizorithi na zile zilizojengwa. Matatizo makubwa yamejitokeza katika nyumba hizi.

Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri, kuna swali niliuliza hapa nikamwambia aniorodheshee kila wizara ina nyumba ngapi. Lakini hapa nitalizungumzia suala hili, kwa sababu juzi liliulizwa swali hapa la viongozi watatu wa juu. Mimi leo nazungumza viongozi wetu Mawaziri, sio vyema mawaziri kulala mitaani au kuishi mitaani katika nyumba zao. Kwa sababu serikali inazo nyumba nyingi na uwezo upo, lakini bado viongozi wastaafu waliokuwemo katika madaraka, hatukatai walifanya kazi nzuri sana katika nchi hii, lakini miongoni mwetu sote tulikuwa na uwezo wa kujenga nyumba za kuishi sisi wenyewe.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kwamba atuletee orodha za nyumba, wanaoishi ambao wamestaafu na kubwa zaidi ni kwamba hawakai wao, wengine wamezikodisha, mmoja ana nyumba mbili, mmoja ana nyumba tatu. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri kwa kweli tujipe heshima sisi wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nitaambiwa na wewe Mhe. Asha Bakari umeuziwa nyumba. Ole wao wanaosema hivyo. Mimi nimeuziwa nyumba kweli. Leo nataka kutoa siri ya nyumba ambayo nimeuziwa mimi. Hivi mimi katika maisha yangu katika nchi hii sina haki mimi. Nikwambie Mhe. Mwenyekiti, maana yake mimi nasikia minong'ono hee anasema nini yeye kauziwa nyumba. Nyinyi mna majumba kumi kumi. Mimi nina nyumba hii moja tena kwa kupewa kwa ari, Mwenyezi Mungu amsaidie sana Mhe. Salmin Amour Juma. Ni kwamba toka nije katika nchi hii, kiwanja kanipa Mhe. Ali Juma Shamuhuna juzi, si la kusikitisha hilo. Sijapewa kiwanja huko nyuma, kila Waziri anayekuja ngojea uko namba moja, ngojea uko nambari mbili, ngojea uko namba ngapi. Kiwanja nimepewa juzi nasema kabisa. Serikali ya nchi hii kiwanja nimepewa juzi.

Mimi bado nasema sina fadhila za kumlipa Salmin Amour Juma aliyekuwa Rais wa Zanzibar hapa. Ni yeye aliyesema kazi anazozifanya mwanamke huyu, wanaume 50 hamuwezi kuzifanya, mnashindwa kumpa kiwanja. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nataka ile minong'ono nong'ono iondoke leo, kwamba anasema nini na yeye kauziwa nyumba. Nimeuziwa nyumba kwa ari na mpaka leo nyumba hiyo ninayo, nimeizidisha na mpaka leo imenishinda kuimaliza. Kuna watu wana nyumba kumi kumi, mashamba, magari na maviwanja sita, saba au nane, lakini imewatoa roho nyumba ya Asha Bakari aliyouziwa na Mhe. Salmin Amour Juma.

Mhe. Mwenyekiti, natoa historia ya nyumba ile. Kwa hivyo, vile viromoromo vimalizike. Unapomnyooshea mwenzako kidole, vitizame na vinne, vitatu

vinakuelekea wewe na hiki kimoja kinasema Mwenyezi Mungu yupo. Kwa hivyo, naiomba sana Wizara ijali wananchi wake. Twende kwenye ardhi huko ndio hakusemeki. Ardhi ni mashamba ya bibi, sio mashamba ya serikali mimi naweza kusema. Kama mashamba ni mali ya serikali basi watu wasingejikumbizia tu. Wanajikumbizia wao mpaka yale mashamba ya kurithi wanachukua, maana yake hata Mwenyezi Mungu hawamuogopi, mpaka makaburi sasa yanachukuliwa yanagaiwa na kupewa wawekezaji au mtu anajichukulia yeye binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana na namuomba Mhe. Waziri kwamba ardhi ni mali ya serikali, hivyo tufuate taratibu na sheria na mimi nitakujakuwa mkali kwenye mambo ya ardhi. Tujiulize sisi wenyewe viongozi tuliomo humu humu Barazani tumejikumbizia heka ngapi ngapi. Kila mtu ana haki katika nchi hii, sasa tusijikumbizie sisi, yule mwengine tukamuona hana haki ni dhambi kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, niondoke kwenye mambo ya nyumba na ardhi, maana yake nimesema kidogo kwa hamasa, kwa sababu kama kawaida yangu. Nakuja kwenye maji. Mhe. Waziri nakuonea huruma, haya wewe yamezee tu, japo yamekukuta sio yako, lakini sasa usharithi. Kwa hivyo, *mkamatwa na ngozi ndio mwizi*.

Mhe. Mwenyekiti, tunafanya haya kwa sababu wizara hii, sijui ina bilisi gani, akichukuliwa Waziri akiwekwa pale na yeye anajisahau. Sasa kwa imani tuliyonayo kwako wewe hatutaki uje ujisahau, tunataka utufanyie kazi nzuri Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban. Kwa hivyo, vigongo na mawe tutakupiga leo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani tufanye utafiti maalum katika maji. Nchi yetu hii ina maji mengi sana tuangalie kila eneo kuna matatizo gani ambayo yanasababisha wananchi wasipate maji. Sitaki nilizungumzie sana, kwa sababu wajumbe wenzangu wameshalizungumza.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika umeme. Umeme najua kwamba serikali ina mpango maalum wa kufanya umeme, hivyo niipongeze serikali kwa kisiwa cha Pemba *Alhamdulillah. Mla kuku wa mwenziwe miguu humuelekea*. Maana kule Pemba *Allahu Akbar*, maana hizo shida walizokuwa wakipata wananchi wa kule sijapata kuona, sasa yamerudia hapa. Naiomba sana serikali kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa. Najua kwamba haumaliziki mwaka huu, tunaweza tukapata umeme wa uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tuliuliza swali hapa, wizi waibe wao watu wa umeme nathubutu kusema hivyo. Wameiba wee kwenye umeme, vifaa mbali mbali.

Mimi simo katika kamati teule lakini ni mambo ambayo tunayaona. Hili nitalisema japo inaundwa kamati teule. Lakini musituzidishie sisi umeme kwa wizi wenu. Mnawapa shida wananchi, hawawezi kulipa umeme ambao mmeupandisha sasa hivi Mhe. Waziri, umepanda bila ya kiasi umeme, niliuliza hapa swali Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo akaniambia, dada wewe ni miaka mingapi hamjapandishiwa umeme. Sio sababu hiyo. Wananchi kwa kweli Mhe. Waziri wanapata shida kubwa sana kuhusu ulipaji wa umeme kwa kipindi hiki.

Kwa hivyo, naiomba serikali, najua serikali kila kitu kinawezekana. Fidia ile ya juu ifidiwe na serikali, wananchi waliokuwa hawana uwezo wapate kutumia nishati hii ya umeme. Mhe. Waziri uje utueleze, kwa nini mtu akilipa shilingi elfu kumi anapata unit 30 na wengine unit 60 wengine 5 na wengine 2 na yule akilipa shilingi elfu kumi anapata unit 6 na ngapi. Mhe. Waziri hapa uje utueleze vizuri, kama umeshadanganywa huko, basi usikubali kudanganywa, uje utueleze kwa makini.

Mhe. Mwenyekiti, nije suala la mwisho, niseme kwamba Mhe. Mwenyekiti, hebu tubadilike mji wa Zanzibar umevamiwa sana, hebu tubadilike. Najua kwamba kuna *plan* nzuri sana ya serikali, lakini tubadilike na sisi wenyewe ili ile *plan* itakapokuja basi tuwe tumeshaanza kubadilika, isiwe nyumba hii imeelekea kusini, nyumba hii kaskazini, nyumba hii magharibi na nyumba hii urejua sijui, mji huo ambao ndio tunautumainia. Naomba sana Mhe. Waziri ujitahidi na wizara hii, kwa sababu imani yetu iko kubwa sana na unao watendaji.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, wakati ni mdogo, nilikuwa na mambo mengi. Lakini nitafanya nini. Baada ya kusema hayo nina sehemu yangu mpaka nije nifafanuliwe ndio niunge mkono hoja ya wizara hii. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

TAARIFA

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe, kabla ya kuahirisha Baraza nina maombi naomba kutoa hapa. Wale wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi wanatakiwa mara baada ya kwisha kuahirishwa Baraza hili waelekee katika chumba chao cha mikutano. Baada ya maelekezo hayo nachukua fursa hii kuahirisha Baraza hili hadi jioni saa 11:00 leo, ahsante.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na sasa tumkaribishe Mhe. Omar Ali Shehe, baadae anafuatia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuanza jioni hii, ili niweze kuchangia hoja hii muhimu. Kwanza nikushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi. Pili nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na ugeni wake, lakini kwa uwasilishaji wake wa bajeti katika mwaka huu 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze na utangulizi kwa kueleza kwamba kwa mujibu wa mahesabu hapa tuliopewa, wizara mara hii imepanga kutumia jumla ya shilingi milioni 272/= kwa ajili ya safari za ndani na nje. Kwa uchanganuzi wa shilingi milioni 136.8/= kwa safari za ndani na shilingi milioni 135/= kwa safari za nje.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli kiwango hichi cha shilingi milioni 272/= kwa ajili ya matumizi ya safari ni kiwango kikubwa sana cha fedha, hasa kwa wizara ambayo ina changamoto nyingi ambazo hazijapatiwa ufumbuzi. Sasa katika kuhakikisha kwamba tunatumia fedha kwa mujibu wa thamani halisi ya fedha, naiomba serikali kwa ujumla wake iweke utaratibu mzuri juu ya kuzifanyia uhakiki safari za ndani na nje. *(Makofi)*

Hali hii inawepelekea watendaji mara nyingi kuwa hawakai maofisini, kwa sababu tunapopitisha mafungu makubwa namna hii, yanawafanya watendaji mara nyingi kutumia muda wao badala ya kushughulikia kazi maofisini wao wanashughulikia mambo ya safari, na safari zenyewe ukiuliza tija yake nini, huwezi kupata. Kwa kweli fedha hizi wakati mwengine hutumika kwa ajili ya safari za matembezi tu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naiomba serikali katika hili iwe na utaratibu maalum. Kwanza sisi Wawakilishi tujiridhishe, kwamba safari hizi zina tija kwa wananchi pamoja na wizara husika, lakini hatuwezi kupitisha kiwango hichi kikubwa cha fedha kwa safari ambazo kwa kweli hatujui matunda yake ni yepi kwa wizara, serikali na wananchi. *(Makofi)*

Katika hili Mhe. Mwenyekiti, nataka nikumbushe kwamba kwa kupitisha mafungu makubwa namna hii wakati tunashughulika na Kamati Teule, Katibu Mkuu wa Wizara hii tulimwita si chini ya mara tano hapatikani, na mara zote

tunazomwita yuko nje. Sasa ikiwa Katibu Mkuu mara nyingi anatumia muda wake wa kazi kwa safari za nje, tutaona ni kiasi gani fedha tunazozipitisha hapa huwa zinatuletea matatizo na hasa katika masuala ya utendaji. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho aweze kutufafanulia hizi shilingi milioni 272 kwa safari za ndani na nje atupe uchanganuzi angalau kwa muhtasari, ili tuweze kujiridhisha kwamba zitatumiwa inavyopaswa na badala yake kama itakuwa hazina maelezo, fungu hili tulipunguze tulipeleke katika maji, ambalo tatizo limedumu kwa muda mrefu kwa wananchi wetu. Hilo la kwanza.

Pili Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie tatizo la maji. Kwa kweli nchi yetu ina tatizo kubwa la upatikanaji wa maji safi na salama, hili hasa kwa kipindi ambacho tunachoelekea cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani, linatupa usumbufu mkubwa, wananchi wetu wanahangaika mijini na vijijini kwa suala zima la kukosa maji.

Katika hili serikali imeunda Mamlaka ya Maji, lakini bado mamlaka hii inaonekana inakwenda katika mwendo wa kusuasua. Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme hapa kwamba Mamkala ya Maji ni moja kati ya taasisi ya serikali ambayo inadaiwa deni kubwa sana la umeme, yaani inadaiwa zaidi ya bilioni 7 za umeme, sizungumzii wateja wengine ambao hukopesha vifaa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, mamlaka hiyo ina deni katika kiwango hicho. Lakini mamlaka hii inadaiwa katika sehemu nyengine sasa tuione na changamoto inayoikabili mamlaka hii, kwamba bado haijakaa katika *position* yake.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali na hili inawezekana ni deni ambalo Mamlaka ya Maji haina uwezo wa kulitatua peke yake, kwa sababu kuna baadhi ya vituo ambavyo serikali iliahidi kwamba deni la umeme watalipa kutoka Hazina. Sasa naomba maelezo namna gani serikali kupitia Wizara ya Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wataweza kuisaidia Mamlaka ya Maji kulipia deni lake hili.
Vile vile nirudi kwa Mamlaka ya Maji, niwaombe wajipange zaidi, kwa sababu pamoja na yote, lakini mamlaka nayo haijajipanga katika kukusanya madeni yake kwa wateja pamoja na matatizo yaliopo kwamba maji hayapatikani na ni kweli kabisa kuwa maji hayapatikani.

Mhe. Mwenyekiti, pia huwezi kuwalipisha wananchi kitu ambacho hawapati huduma na hiyo haiwezekani, lakini kwa yale maeneo ambayo angalau wanaweza kupata mara moja au mbili kwa wiki, basi kile kidogo ambacho kinastahiki Mamlaka ina wajibu wa kujipanga vizuri, ili hicho kidogo kiweze

kupatikana kwa ajili ya kufidia mambo ya madeni pamoja na masuala mengine. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia Wizara ya Fedha itoe kauli namna ambavyo watakavyoiwezesha Mamlaka kulipia deni lake la umeme. Pia nipate jawabu namna gani Mamlaka imejipanga kiutendaji hususan katika suala la zima la kukusanya madeni yanayotokana na malipo kwa wateja.

Nikiendelea na mchango wangu, sasa naomba niende kwenye Idara ya Nishati. Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kuzungumzia ujenzi wa uchumi kama hatujazungumzia suala la upatikanaji wa umeme tena wa hakika katika nchi yetu.

Kwa kweli suala la umeme sikuona katika bajeti, yaani haikujikita sana kuelezea ni namna gani Zanzibar itapata umeme wa uhakika, tena umeme ambao wananchi wataweza kuununua sikusikia. Mhe. Mwenyekiti, kama hivyo ndivyo, ikiwa serikali haikuzungumzia chochote, itakuwa ni tatizo kupitisha bajeti hii ambayo haikuzungumzia kitu muhimu sana kinachoweza kuwagusa wananchi. Upatikanaji wa umeme wa uhakika, ambao wananchi wetu wataweza kuununua. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika hili hatuwezi tukaitegemea *TANESCO*. Shirika lenyewe la Umeme linadaiwa fedha nyingi sana na *TANESCO,* na sisi pia tunajiacha miguu na mikono kwa ajili ya kuutegemea umeme wa *TANESCO*.

Sasa mategemeo ya wananchi pamoja na Baraza letu la Wawakilishi ni kuona azma ya serikali inatekelezwa katika kuipatia nchi yetu umeme wa uhakika. Lakini leo sitozungumzia sana suala la umeme, kwa sababu Kamati ya *PAC* inafanya kazi hivi sasa ya kulichunguza Shirika la Umeme na wala sitokwenda mbali sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, katika nukta hii namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atupe maelezo, kuhusu mchakato wa serikali kuelekea kuipatia Zanzibar umeme wake wenyewe tena wa uhakika. *(Makofi)*
Lakini hapo hapo katika kipindi cha karibuni kama wiki moja wananchi walipata matatizo sana walipokwenda kulipia umeme, walikatwa bila ya maelezo yoyote licha ya lile agizo lililotolewa kwamba kodi ile iliyoongezeka kama mwezi mmoja uliopita. Kwa kweli ni juzi tu wiki moja wananchi walikwenda vituoni kulipa na kukatwa bila ya maelezo yoyote, na hadi sasa kwa kweli shirika limeshindwa kutoa maelezo na kuwaambia wananchi kwamba nini kimetokea. *(Makofi)*

Sasa naomba niitumie fursa hii kumuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja awaeleze wananchi kwamba kulitokea kitu gani mpaka wananchi wakakatwa fedha zao bila ya kupata maelezo yoyote.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niingie katika suala zima linalohusiana na mafuta. Mhe. Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu ameturuzuku nishati ya mafuta na kila nchi duniani Mwenyezi Mungu ameiruzuku kuwa na kitu ambacho hicho ni cha kutegemea kwa uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sisi wazanzibari kama alivyoeleza Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba rasilimali kubwa yenye ushahidi kuwa tunayo mafuta. Lakini katika hili kwenye kitabu hichi sijui kama sikukisoma vizuri, nadhani haikuja na mkakati wa namna gani serikali imejipanga katika kuhakikisha kwamba kwa bajeti ya mwaka huu 2012/2013 inajielekeza katika kuandaa mkakati wa kuona tunachimba rasilimali yetu hii, hiyo itakuwa udhaifu mkubwa Mhe. Mwenyekiti.

Sisi kama Baraza la Wawakilishi la wananchi hatuwezi kila siku kuwatoza kodi tu na kuwakamua wananchi wakati tunayo rasilimali muhimu sana katika uchumi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika hili wakati nikichangia Hotuba ya Makamo wa Pili wa Rais, nilisema kwamba kuna mambo ambayo ni ya Muungano na Zanzibar tulipoamua kuyatekeleza basi tuliyatekeleza bila ya matatizo na tunaendelea kuwa nayo. Sasa iweje leo tushindwe na kupitisha Sheria ya Kuunda Shirika letu la Mafuta, ili tuchimbe matufa yetu.

Kwa kweli tulisema hakuna sababu, nadhani sababu inaonekana ni sisi wenyewe bado hatujawa tayari ni sawa na kuambiwa nyumbani mwenu kuna kasiki, lakini kuna shetani ameikalia. Sasa tunataka tuone huyu shetani aliyeikalia kasiki yetu na ikiwezekana tupigane taire sisi kwa sisi humu ndani, ili tuweze kuichimba rasilimali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tulitegemea kwamba bajeti hii itatuelekeza angalau katika mchakato wa awali, leo tumeambiwa kuna sera na huku serikali inasema inazuia kabisa mambo hayo, tusubiri mchakato wa Katiba mwaka 2014, lakini kwa upande mwengine tunaambiwa kuna matayarisho ya sera na huku nyuma tunaambiwa tayari kuna *draft* ya mpaka ya sheria. *(Makofi)*

Kutokana na hali hii, tunafika pahala kwa kweli hatuelewi hasa msimamo wa serikali katika hili ni kitu gani, isipokuwa tunajizonga sisi kwa sisi na wala hatuelewi, mara tusubiri, tukija kwenye bajeti tunaambiwa kuna *amount* hii

imetengwa kwa ajili ya sera, mara kuna sheria tumeziweka kwenye *shelves*, ukweli hasa mnafanya kitu gani? *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema awali katika wizara zilizopita kama vile Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili, kwamba hivi sasa ni wakati wazanzibari tunahitaji kama wenzetu wanavyofanya Bara kule, na sisi tunahitaji kuchimba mafuta yetu, kama ile ni ya Muungano na wala hawatushirikishi basi na sisi hii ni yetu sisi wenyewe ni lazima tuchimbe sisi wenyewe. *(Makofi)*

Katika hilo nirudie tena kwamba azma yangu iko pale pale na leo nimeungana na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwamba katika kikao kinachokuja tutaleta hapa Mswada Binafsi, ili tuone kwamba tunakuwa na shirika letu wenyewe. Hili nadhani na niipongeze serikali kupitia Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kusema kwamba chochote ambacho kitakuwa na maslahi kwa wazanzibari serikali haitopinga. Kwa hiyo, tuna imani kwamba serikali nayo itaunga mkono mswada huo utakapokuja tukijaaliwa. *(Makofi)*

Sasa niende katika Idara ya Nyumba. Mhe. Mwenyekiti, umasikini wetu takriban kwa sehemu kubwa sana unasababishwa na suala zima la nyumba, kama tutafanya utafiti tutaona kwa maisha ya mnyonge wa kawaida katika nchi yetu, basi nusu ya maisha yake anayatumia katika kujipatia kibanda cha kuishi. Nadhani kama tutafanya utafiti mtu tajiri atajenga kwa wiki moja tu na atamaliza, yaani tajiri wiki moja anaangusha kitu kinatulia, lakini kwa mnyonge au mzanzibari wa kawaida nusu ya maisha yake anayatumia katika kujitafutia kijibanda. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hatuwezi tukaondosha umasikini kama serikali yetu haijakuwa na sera maalum ya kuwatafutia makaazi bora wananchi. Suala hili Mwenyezi Mungu amrehemu Marehemu Mzee Abeid Amani Karume aliko, kwamba yeye ambaye hakusoma hili aliliona na akawajengea wanyonge na leo tunaendelea kujisifia kwamba ni Matunda ya Mapinduzi Matukufu. *(Makofi)*

Sasa leo imekuja na hii ni Awamu ya Saba, kwa nini tusiitekeleze kwa vitendo sera hii, mimi nasema inawezekana kwamba duniani na kokote kule kuna utaratibu wa wananchi kujengewa nyumba na kukopeshwa kidogo kidogo na hilo linawezekana, sisi tunashindwa na kitu gani katika hilo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, katika hili tuliona kuendelea kuwa na Idara ya Nyumba haiwezi kutusaidia, lazima tufike pahala tuwe na shirika kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwamba shirika linao uwezo wa kukopa na kukopesha. Kwa hivyo, ni kitu cha kukitungia sheria na tukawa na shirika

lenye mamlaka kamili ya kuweza kutafuta mikopo ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuwajengea wanyonge masikini wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja atupe hasa ni lini sheria hiyo ya kuibadili Idara ya Nyumba kuwa ni shirika lini italetwa katika Baraza hili, kwa sababu siku zote hatuwezi tukazungumzia vitu ambavyo havipo duniani, kwamba kila siku serikali iko mbioni, tuna mchakato hivi na vile. *(Makofi)*

Kwa hivyo, sasa tunataka tarehe maalum, japo kama hutatupa, lakini Kikao angalau cha mwezi wa Oktoba au Januari, ili tujue kwamba kikao fulani tutaletewa sheria hii ya kuwa na Shirika la Nyumba, ambapo wananchi wetu wanyonge watanufaika. *(Makofi)*

Katika hili Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kwa sababu hivi sasa tunazo nyumba na tumeshindwa kuzi-*maintain* kupitia Idara ya Nyumba. Vile vile nakumbuka Waziri aliyekuwepo aliunda tume maalum kwa ajili ya kuzipatia ufumbuzi, kwa sababu inaonekana nyumba hizi za umma ziko mikononi, ambazo nyengine ziko kwenye mikono ambayo haifahamiki, kitu ambacho kimepelekea hata Kodi ya Serikali inakuwa haikusanywi vizuri katika hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, serikali ilikuja mbele ya Baraza hili na ikaahidi kwamba imeunda tume, lakini bahati mbaya sana na huu zaidi ya mwaka wa ngapi sijui, tume hiyo bado haijamaliza kazi yake na wala hatujapata ripoti. *(Makofi)*

Sasa kwa kupitia bajeti hii namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu tume hiyo imeundwa na Mhe. Waziri, tena imetumia fedha nyingi za umma. Kwa hivyo, angalau basi tuelezwe tume imefikia wapi na ripoti iko wapi, ili tuone kwamba suala la mchakato huu wa kuzibaini nyumba zile na uhalali wake na wale waliopewa tuweze kuziona. Mhe. Mwenyekiti, katika hilo lina athari kwamba wengi sana waliomo kwenye nyumba hawalipii kodi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, leo inashangaza kwamba tumeombwa hapa tuidhinishe fedha kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo. Lakini Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, zinaeleza kwamba Idara inadai fedha nyingi sana. Sasa sisi hatuwezi kuidhinisha fedha wakati ambapo kuna kodi iko katika mikono haijaweza kukusanywa. *(Makofi)*

Nadhani jambo la busara kwanza idara ingekwenda kukusanya kodi na ikatuambia mapungufu yako wapi, ili tuweze kutafuta fedha sehemu

nyengine. Kwa hivyo, mimi binafsi napinga kuidhinisha fedha hii ambayo itakwenda kwenye matengenezo ya Nyumba za Maendeleo, kama fedha zilizomo wanaidai hazijaletwa hapa tukaambiwa, na tukaambiwa kwamba fedha hizi zimepatikana na nyengine hazijapatikana, basi hapo ndipo tunapoweza kutafuta au kutoa fedha sehemu nyengine na tukaziingiza katika sehemu hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ninachodai hapa kwanza ile Ripoti ya Tume ya Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Maalim Abdalla Mwinyi Khamis iletwe katika Baraza. Vile vile nazuia fungu hili la kwenda kufanyia matengenezo iwapo kuna fedha mikononi mwa wadaiwa ambazo bado hazijakusanywa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, fanya majumuisho kwa dakika tano za mwisho.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, sawa.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa ya ujenzi wa Nyumba za Michezani pamoja na Mpapa, nataka nikumbushe tu katika Baraza, kwamba ujenzi wa nyumba zile haukufuata taratibu. Sasa pamoja na mafanikio ya kuzisimamisha nyumba zile, lakini inawezekana kama tungelifuata utaratibu au wizara ingelifuata taratibu, basi inawezekana kwamba fedha nyingi zilizotumika pale zingeliokolewa na kwenda sehemu nyengine. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tulipokwenda kuhoji tuliambiwa ilikuwa ni mambo yalikuwa hayafahamiki, vikosi vinatumwa lakini mara wanaambiwa saruji nendeni Ikulu mkachukue, sijui nendeni kwa duka la Bwana Juma mkachukue na wala huo si utaratibu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, pamoja na mafanikio haya, lakini tunasisitiza kwamba utaratibu wa matumizi ya fedha tunazodhiidhinisha ufuatwe. Majengo yaliyojengwa yale Michenzani na Mpapa hayakufuata utaratibu, ni bosi fulani alikuwepo pahala fulani na kuagiza tu kutoa mifuko 100 au 200 na mingine kachukueni JKU mujenge. Fedha zilizokuwa zikiidhinishwa zilikuwa zinakwenda pahala gani, wanatumia nguvu kazi ya vikosi wakati tayari fedha hapa tumeshaidhinisha, kwa hivyo nasema huu ni wizi ambao hatuwezi kuukubali katika bajeti hii. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, ili tuidhinishe fungu hili serikali ije ituambie utaratibu kamili utakaotumika wa kisheria, kwa ajili ya kuzikamilisha nyumba ambazo hatujazikamilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo kwa kuheshimu muda wako naomba niseme tu, kwamba kuna tatizo kubwa la ardhi na imekuwa ni nyimbo ya kawaida Mhe. Rais, Waziri, Wawakilishi na hata wananchi wanalia kwenye ardhi. Kwa hivyo, hivi sasa ni wakati pekee Baraza hili liunde Kamati Teule. *(Makofi)*

Vile vile nakubaliana na wazo lililotoka kwamba Baraza la Wawakilishi liunde Kamati Teule kwa ajili ya kuisaidia serikali katika kubaini matatizo ya ardhi yanayojitokeza, ili kuona kwamba tunafanya haki, kwa sababu ardhi ndio iliyochukua dhima ya Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tukumbuke kwamba moja kati ya kitu kilichosababisha Mapinduzi katika nchi hii ni ardhi. Mhe. Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alitoa ardhi kwa manyang'au wale na kuigawa kwa eka tatu tatu kwa wanyonge wa nchi hii, ambao ni wakulima na wakwezi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tukumbuke suala la ardhi katika nchi hii lina umuhimu wake, na kwa msingi huo hatuwezi kuruhusu watu wachache kuifanyia mchezo ardhi, naunga mkono hoja kwamba iunde Kamati Teule, kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi suala la ardhi. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante sasa tumuite Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na baadae Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kuweza kunipa nafasi ya leo kuwa mtu wa pili kwa ajili ya kutoa baraka na mimi kuichangia wizara.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nimsifu sana Mhe. Waziri wangu, ambayo itakuwa ni mara ya kwanza tokea kuanza kwa bajeti kuweza kumsifu Waziri, kwa sababu mtu mwenye haki yake mpeni pamoja na watendaji wake kutokana na kitabu hichi kizuri na wala sitaki kupoteza muda Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Lakini kwanza Mhe. Mwenyekiti, katika kuchangia nakubaliana na Mhe. Mjumbe aliyekaa kitako kwamba iunde Kamati Teule, kwa kutumia Kanuni yetu ya kifungu 120 ukurasa wa 92, naomba Mhe. Mwenyekiti turidhiwe, ili kwa kuinusuru nchi yetu ikapelekwa katika Mahakama ya *The Hague*. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti, tuweze kufanya hivyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tulipokuwa tukitembea kama Kamati tulikuwa tunahoji mambo mengi katika idara zetu hasa ukurasa wa 11 kuhusu usajili, na tulijaribu kuuliza utaratibu wa sheria. Kwa bahati nzuri nimshukuru sana Mkurugenzi alitusaidia sheria ambayo mimi nilikuwa siijui kama Mwenyekiti, katika masuala ya ufutaji wa ardhi (*Land Lease*).

Kwa hivyo, tulikuwa tunamuuliza hiyo *land lease* inafutwa vipi, kwa utaratibu gani na sheria ipi? Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri siku ile Mhe. Mwanasheria wa Idara ama Wizara alikuwepo, alitueleza kuhusu utaratibu wa kufuta *land lease*, kwanza ni utaratibu mkubwa sana na unataka umakini, kwa hiyo naomba kunukuu sasa Mhe. Mwenyekiti na hata katibu wangu wa kamati alikuwa akiandika *point* hadi *point*.

Kitu cha mwanzo alitwambia, kwamba sheria hizi sasa ni ngumu kuifuta *land lease*, kwa sababu gani na akatueleza. Sababu za kufanya ugumu wake kwanza unatakiwa uende kwenye Mahakama na ukaandike *Special Order*, kule Mahakamani ukaeleze yale madhumuni hasa ya ile *land* yenyewe unayotaka kuifuta, halafu Mahakama kama imeridhika ndio itoe kibali cha kuweza kufuta, hilo moja alituambia.

Vile vile sehemu ambayo iliyokuwa imeshafanyiwa marekebisho na mimi nilimuuliza hata kufyeka, akaniambia sehemu ikifyekwa inakuwa ngumu sana kuweza kuifuta ardhi ile, kwa sababu inaonesha tayari yule mtu anataka kuitumia kwa mujibu wa utaratibu kama alivyopewa.

Mhe. Mwenyekiti, tuliendelea kumuuliza je, unafanya vipi ukitaka kumfutia, alisema ukitaka kumfutia unampa kitu *notice* ya muda wa miezi mitatu na halafu unamuongezea indhari ya muda wa miezi mitatu, na halafu mwisho sasa imesharidhika, ina maana muda wa miezi sita hiyo, kutokana na yule anayetaka kufutiwa amejibu au hakujibu, pale ndipo unapotoa barua ya kumwambia sasa *officially* kabisa ardhi yako imefutwa.

Lakini jambo la kusikitisha Mhe. Mjumbe ambaye ni kaka yangu hapa amezuia mafungu ya kutoka nje, lakini kumbe kwenda kule nje tulikuwa na madhumuni ya kuwaita *investors* waje hapa Zanzibar kwa ajili ya kuwekeza, ili wananchi waondokane na umasikini wa Zanzibar. Kwa hivyo, ndio maana fedha hizo zikawa zinatumika kwa watu kwenda nje kwa ajili ya waje hapa, lakini kinyume chake tumewaita *investors* kuja hapa na kuwatia kabali ndio maana yake na wala hatujawatendea haki. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumaliza shughuli hiyo siku hiyo kwa mara ya mwisho tena siku ya majumuisho nilimuuliza swali mbele ya Mhe. Waziri kama hakumbuki mimi nakumbuka. Kwa hiyo, tulimwambia je, kama mtu

amefutiwa ardhi, lakini mwenyewe hana habari kama amefutiwa kile kitu, je mtu yule vipi na Mkurugenzi akajibu bado hajafutiwa huyo.

Sasa natoa ushahidi kwamba wamefutiwa watu ardhi hawa *notice*, indhari na hata ile *official letter* hawakupelekewa. Je, Mhe. Waziri uko tayari kuwarejeshea haki zao hawa wazungu? *(Makofi)*

Jambo baya zaidi wanalipa kodi *on time* na wala hawakuchelewa hata siku moja kwa mujibu wa sheria na wamefutiwa, hichi ni kitu cha kusikitisha, lakini wengine tumewapa majina mabaya na tumewafurusha nchi hawapo kabisa, waingia uchizi wako Dar-es-Salaam wanahangaika na miji, wanashindwa kurudi kwao na fedha za watu hawazijui watazipata wapi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ushahidi zaidi idara husika wanasimamia mauzo kati ya mwananchi na yule *investor*, anapoteza fedha zake nyingi. Mhe. Mwenyekiti, ninayo *document* hapa, lakini jambo la kuchekeza na sisi kila leo tunapiga kelele hapa kwa ajili ya wafanyakazi wetu jamani fedha kidogo. Kwa mfano, humu nimeona sehemu moja kwenye fungu humu mambo ya ukusanyaji, nyinyi huku mnatuonesha mafungu na kwengine mnatufutia mafungu, jambo hili linanishangaza sana, huku tunapunguza kodi na sehemu nyengine tunaonesha ukusanyaji ambao umewekwa kwa asilimia umekuwa ni mkubwa, si kweli tusidanganyane naonesha ushahidi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna hati hii hapa ambayo huyu mtu anatakiwa alipe *dollars* 5,000 lakini huku mtu aliyefutiwa jambo la kuchekesha anatakiwa alipe serikalini *dollars* 11,565 Kizimkazi hiyo, tunakwenda wapi Mhe. Mwenyekiti? Ameshajenga , anataka kumaliza shughuli zake na ameshapata pesa zake za kujiendesha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: (Anaendelea) anakwenda kulipa fedha za kodi ZRB. Nawasifu sana ZRB Mheshimiwa tena nawasifu, nawasifu. Wanapoona anakwenda kulipa mtu *rate* ndogo wakati mwanzo kuna mtu ambaye amewekewa *special* alipe *rate* kubwa walizikataa zile za *rate* ndogo wakasema sisi hatukujui wewe. Aah, manaake miye ndiyo niliyopewa. Wamepewa vipi? Umepewa kisheria. Lakini kumbe tumegundua kuna kampuni feki, ambazo zinapewa hizi *land* ni feki Mheshimiwa, ukweli tuseme huo. Hebu twende kwenye utaratibu wa sheria, Mwanasheria wangu sasa nakuelekea wewe.

Sheria hii maeneo ukiyafuta unatakiwa ufanye nini? Umpe mtu ama dalali auze? Au arudi kuko serikalini kwa mujibu wa sheria yaweze kugaiwa kwa utaratibu mwengine, atafute invester mwengine kama yule kashindwa. Lakini

je, ipo sheria mtu kumfutia halafu usimpe fidia yake wakati yeye yule ameshakula hasara.

Mheshimiwa mimi ni mwenyekiti lakini naigeuka nyumba yangu kwa tatizo hili. Sitoiacha nyumba yangu, nauza basi niitizame hivi hivi. Naziba ufa na kuziba kwangu ufa nasema hichi kitu kimo ndani ya sheria, hawa watu wameonewa.
Kuna mwengine huyu analipa dola 13,000, anakwenda kulipa mtu dola 3,000, hiiii! Mhe. Mwenyekiti hizi nyengine zinakwenda wapi. Hatutoacha kusema hata kidogo, tunaiokoa Zanzibar tusiingie kaumu mbaya katika nchi za wenzetu. Hili tumeshakuletea ripoti kama Kamati Mhe. Waziri wetu. Nilikwambia Mheshimiwa nakupenda sana lakini Wizara iliyopewa mbaya.

Wizara hii inataka watu sugu kama sisi. Wanasema Tume imeshasema na tumemwabia Mhe. Rais. Mimi kitu ninachosikitika jamani Mhe. Rais tunamdanganya katika Bango Kitita tena naendelea tena kumwambia angeyajua haya Mhe. Rais hayo yanayofanywa huko nje. Kwa sababu haiwezekani itakuwa mtu huyo aliyefanya hivi itakuwa lazima mtu huyo aliyefanya hivi keshatengeneza mabilioni ya fcdha, hatujaokoa hapa. Mheshimia tuko *serious* na suala hili, tunaomba kamati teule. Kwanza Mhe. Makamo wa Pili ameshairidhia hiyo, amaikubali zamani. Hatupitishi vifungu mpaka tuhakikishe Kamati teule imeundwa na hiyo ndiyo itakuwa muokozi.
Mheshimiwa la pili la kusikitisha kuna mwananchi wangu mmoja anakaa Kiwengwa anaitwa Hamadi Mamoja, kanyang'wanywa hati na mfanyakazi wako anaitwa Mohammed mpaka leo hati yake hajapewa, anamadhumuni gani. Hati Mheshimiwa iletwe hiyo. Kwa nini mnyang'anye hati yake, tunyang'anya hivi hivi, tunanyang'anya, haiwezekani hilo. Hiyo hati iletwe tena iletwe mimi nitaunga mkono kwa asilimia zote, lakini nataka hiyo hati iletwe.

Mheshimiwa nikiendelea kwa haraka hara nimemaliza masuala haya ya matatizo yetu, isipokuwa iundwe Kamati ikiundwa Kamati ndio hapo tunamaliza maswali hayo.

Mheshimiwa nende kwenye Mahakama ya Ardhi, bado hapa hatujawatendea haki. Mimi namuhurumia sana Mwenyekiti yule. Yule Mwenyekiti anaumbo lake mnene kama miye lakini kutokana na kazi tulizomtwika kanyweya, hana mua wa kupumzika, tumesema mpaka tumechoka jamani wapo kule watu wanaoweza ngazi hizi tuwapelekani kule.

Mhe. Abubakar tupeni hao watu, mumsaidie yule kijana jamani imekuwa kama kalazimisha, kaomba. Ndio kaomba lakini kwa mujibu wa kutafuta rizki. Lakini imefika pahali tumemtwisha anafikiri, anamawazo nitafanya

nini. Ufanye nini ndio mambo ndio kuomba kazi. Tunaomba Mheshimiwa hili nalo uje kutusaidia. Na Ofisi yenyewe hebu itizame kijifinyu. Kwa kweli hatujamtendea haki kijana wetu. Wameomba watu ofisi wamepewa mara moja lakini yeye kaomba mkapa kachoka hajapewa. Mimi naomba Mheshimiwa hiyo afisi aliyoomba tunaomba apewe aweze kufanya shughuli zake kwa mujibu wa utaratibu.

Mheshimiwa kuna suala hili la Mwenyekiti, mpaka leo hajachaguliwa wa uhaulishaji. Waheshimiwa mtawpapa neema sasa hivi watu wa Mambomsige, watatengeneza hati wakati nyinyi mmeshashindwa. Mimi nashangaa mpaka leo Mwenyekiti kashindwa, hebu nipelekwe miye utizame Mwenyekiti. Mwenyekiti hatukuweka *condition* kubwa, tumeweka *condition* zetu kwa Katibu, Kabitu ndiyo mtendaji ni lazima afike na kiwango fulani. Lakini Mwenyekiti wa kukaa pale aende akasinzie tu tumalize pale mpaka leo. Hili kwa kweli linasikitisha sana.

Mheshimiwa kuhaulisha pale hatuhaulishi bure, unahaulisha kwa fedha, lakini mpaka leo mwenyekiti hajachaguliwa kulikoni nini Mhe. Waziri? Tunaomba utupelekee salamu zetu kwa Rais tunamuomba baba yetu hatumuingilii kwa mujibu wa sheria na mihimili ilivyo lakini tunamuomba kutokana na hasara inayotukuta sasa hivi watafanya vitu feki watu.
Mheshimiwa upimaji, ndiyo yale yale ninayosema. Upimaji kwa mujibu wa taratibu sasa hivi za kanuni yetu za utumishi sasa hivi imefika haja achaguliwe Mkurugenzi. Mheshimiwa Wakurugenzi wapo waliyokuwa wametoka *Universities* Masuala ya Ardhi tunao. Naona mpaka leo, basi yule yule tumtangaza *hafamanilah* hakuna tatizo lolote. Tumpe haki yake kijana keshatumikia kwa muda wote. *Experience* yake tumeshaiyona, kwa nini asipewe. Ili tuone sasa hivi ipo haja ya kuwa Mkurugenzi *official* kabisa ametangazwa na Mhe. Rais na kupewa kiapo. Mimi naomba sana kwa hilo kuwa huyu mtu, tunamuomba Mhe. Rais tuko pamoja na yeye atusaidie.

Mheshimiwa katika ukurasa wa 31 majenzi. Nimshukuru sana Mheshimiwa wangu wa Majenzi kajitahidi sana na ususan kila ukimpa miradi anajitahidi. Lakini pesa mnazompa kidogo, hasa hivi za majenzi ya Mpapa shilingi milioni 100 ni sawa sawa na milioni 10, ataifanya kazi hiyo vipi. Fungu hili bado dogo, limeng'ang'aniwa pale pale tu . Mheshimiwa wangu Omar Yussuf nitamuomba hizo fungu ulizozikuta kuna wingi wa fedha mpunguzieni huyu. Hayo mambo ya safari, kila leo watu wanasafiri lakini neema yake ndogo, hatimaye tunanyang'anya watu ma- *investor* ardhi, ndio maana yake hiyo.

Mheshimiwa Mkurugenzi huyu hata pesa ya gari hamumpi, basi zile gari anazofanyia mpango wake mwenyewe muachieni jamani msiziweke pale. Sijui kama imeruhusiwa ile gari, inanyiwa na dete tu pale, hebu mruhusini

muachieni. Ule ni ujanja wake kuna mambo mengi tulisema sisi wana Kamati kuwa Wakurugenzi wawe na vigezo ili akiondoka pale akija mkurugenzi mwengine arithi kigezo kile kizuri. Na huyu Mkurugenzi wetu mzuri. Pamoja na kwamba mnamwita mchina lakini uchina wake ni mtendaji kazi.
Mmemzuilia kazi yake aliyopewa *contractor* kujenga kibanda, mkamtaabisha pesa mliyompa, haibi huyu. Apewe pesa zake amalize zile kazi za watu tusimtie dosari kwa kuwa kizuri tena ndi tukitie dosari. Haiwezekani Mheshimiwa.

Nikiingia katika Mamlaka ya Hifadhi ya Maji. Nashukuru sana kwa jitihada zao, kazi ngumu na jitihada zo ni nzuri. Chakufurahisha kabisa wamejaribu sana katika fedha za wahisani kuzitumia kama vile inavyotakiwa. Lakini bado maji jini ya ardhi inakuwa ni kiwango kidogo na hasa tatizo kwamba tunakata vianzio vya maji.

Nawashukuru sana na naishukuru sana Bodi chini ya mwenyekiti wake mwana mama kama ulivyokaa wewe hapo Mwenyekiti. kama unavyoendesha kikao chako kizuri na huyo mwana mama anaendesha Bodi yake vizuri kabisa. Yuko pamoja na wafanyakazi wake, yuko pamoja na wataalamu wake, hiyo ni moja katika sifa nzuri. Ukianza bodi ya kubagua watu huna kazi. Kwa hivyo mimi namsifu sana huyu mwana mama na *cabinet* yake yote. Nimemtaja yeye na kumsifu kwa sababu yeye ndio kiungo kikuu sasa hivi. Kama ulivyo wewe sasa hivi ukinambia nikae kitako, nakaa kitako.

Kwa hivyo akina mama tunakupeni hongera sana. Mimi panapokina mama kukusifuni nakusifuni tu ukweli niuseme ni huo. Mamlaka ya Maji yapo marekebisho madogo madogo, nakubaliana nayo. Kwanza watendaji kidogo hasa mafundi, tuongezewe mafundi. Wataalamu tunao lakini watendaji wa kazi kidogo. Kila siku wale wale, Kesi bomba, Bangi, nani nani, wale wale. Wapewe fursa ili waweze kuongeza mafundi ili tuweze kufika pahali pazuri.

Nikija katika Mji Mkongwe. Tulipokwenda na Kamati alisikitika sana Mkurugenzi wangu suala la kusema kwamba kuna fedha ambazo zilikubalika. Mheshimiwa wangu Mwinyihaji siku hiyo alinambia kuwa zile fedha kweli zipo katika *account* ya peke yake. Mimi nasema si kweli. Kama ni kweli basi namuomba Mhe. Waziri aje kunithibitishia leo ni kiasi gani anapewa huyu ili aweze kuimarisha vizuri Mji Mkongwe wake.

Mimi nachoomba kabisa Mheshimiwa wangu waziri uje kunieleza kuwa Mamlaka hii ya Mji Mkongwe inapewa fedha tangu ianze shughuli hizo ukurasa wa 37, shughuli zake zinaendeshwa kwa kupitia mfuko ule kwa kiasi kadhaa. Lakini kama hawakupewa itakuwa mnatudanganya Baraza hili. Siku moja nilimuuliza kaka angu naomba nimtanie, nilimwambia je, tukenda

tukimgundua Waziri amefanya manyago atakuwa yupo tayari kujiuzulu. Lakini naona hawajiuzulu wanaficha nafasi, nashangaa sana Mhe. Mwenyekiti, hawa hawajiuzulu bwana, madaraka matamu tuache haya na yale tuseme ukweli ulivyo. Hawakujiuzulu mpaka leo tumewang'ang'ania nao hivyo hivyo tu. Lakini Ishalla Salama, twendeni hivyo hivyo lakini nashukuru kuwa wengine hawana nongwa, tunacheka nao, tunafurahika nao, ndiyo ilivyo hivyo Mheshimiwa.

Nende katika Shirila la Umeme nakubaliana nalo Mheshimiwa matatizo yapo, marekebisho yapo na yatakuwepo lazima kidogo hapa niwe mnyonge kwa sababu bei iliyosemwa kubwa na mimi kwama mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, naomba Meneja wangu ni mtu msikibu, ni mtu hana tatizo lolote masikini ya Mungu ni mnyonge. Atakubali na sisi Wawakilishi wake kutupunguzia bei, mimi nina imani hiyo. Wallahi ukenda kule akikusikitikia hiyo bei tunayopewa kule Bara kwa ndugu zetu wa dam utasikitika sana Mheshimiwa. Anafanya hili kutokujua au kudhibitiwa, hasemi ukweli anavyopigwa bei kule kirungu kikubwa cha umeme. Ndio maana tukasema sasa tutafute mbadala.

Mheshimiwa watu wapo tayari kufanya umeme wa takataka, Mhe. Ramadhani kubali suala hilo ili ufanyike umeme wa mbadala. Umeme wa upepo ukubali tunafanya *challenge*, *competition* ndio biashara zenyewe, ili waweze kukubali. Nakuomba sana Mheshimiwa wangu mtu rahimu. Lazima mtuletee umeme mbadala kwa kuisaidia ZECO, vyengine siku zote tutamuona Meneja mwizi, watendaji wizi, kumbe si wizi wanafanya kazi kwa hasara. Hili nalo tulione jamani. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi sana kuwa Wajumbe wenzangu wamenielewa jinsi gani ninavyozungumza. Tatizo linalotupata Zanzibar kuwa umeme mbadala hatuna na ndio maana ukaona wemefurahi kwa hilo Mhe. Mwenyekiti, wamefurahi kuwa Mshimba kasema kitu cha uhakika.

Mheshimiwa nimalizie kwa idara hii ya nishati. Mambo mengi sana yamezungumzwa na mimi nitakuwa si mfadhili nikikosa kulizungumza nitakuwa nimefanya makosa makubwa sana. Idara hii kwanza tuliitupa muda mwingi sana. Lakini kwa kuwa sheria imeridhiwa italetwa kupewa Mamlaka yake husika ya kuweza kupanda bei ya petrol, sikujui za kushughulikia *quality* za petrol ili iwe sawa sawa na kama ile ya wenzetu ya EURA. Mimi nashukuru sana hilo naomba Mwanasheria Sheria utuletee haraka sana ili kuweza kutusaidia angalau sasa itakuwa ina jina zuri.

Bure yote kwa sababu ofisi hawana. Leo ukishamtanulia hiyo sheria nambia maafisa wake atawaweka wapi. Tulimuomba nafasi pale upande wa pili

tukaambiwa ile itakuwa ndio sehemu ya kumbukumbu ya kuweka mafaili ya watu wa umeme. Naomba watu wa umeme maeneo yapo mengi kule Saateni, waweke sehemu nyengine ili wawasaidie wale wenziwao. Najua hilo ni zito lakini tutafanya nini jamani, mkurugenzi huyu anataka kujitanua na yeye kwa mujibu wa taratibu. Anataka kuweka historia ndani ya Idara yake. Naomba sana asaidiwe, apewe ofisi ya kuweza kujiendesha.

Nimshukuru sana Mkurugenzi huyu wa sasa hivi ambaye ni mpya kutokana na jitihada zake na kutafuta wafadhili pande zote ili Zanzibar iweze kupata ufadhili wa kuweza kulekuleta umeme mbadala pia na ufadhili wa kuweza kuchimbwa mafuta yetu. Mafuta tunasema kuwa yachimbwe na wenyewe Wazanzibari tupo tutasimamia. Wataalamu tumeambiwa kwamba wanakwenda kusomeshwa. Hebu njoo unambie Mhe. Waziri ni wataalamu wangapi sasa hivi umeshawapeleka. Naomba hili uje kunieleza na nijue kwa uhakika kama kweli sasa hivi tunataka kuchimba wenyewe mafuta yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kabla hujanambia kuwa Mheshimiwa dakika 5 nakuomba sana kwa kumalizia wananchi wa Kitope kwa kuwa wao ndio wanaodhalilishwa na ardhi zao. Wananchi wa Kiwengwa wamesema hivi karibuni kulikwenda kupimwa sehemu ya kijana mmoja anaitwa jina lake limenitoka kidogo. Huyo ana midimu yake kaandika barua yeye mwenyewe. Nawambia watu wa upimaji, mliokwenda kumpimia kaondoweni, wananchi wa Kiwengwa wamesema hawakubali, hawakubali, mtawafunga wote. Kwa maana hiyo nyinyi mlipopewa ile barua tu na nyinyi mbio mkenda mkapima, mkampa mtu mwengine. Jamaa yule amedhalilishwa, michungwa yake imekatwa, midimu yake imekatwa. Kwa hilo nasema Mhe. Ramadhani Shaaban na mimi mwenyewe niko mstari wa mbele mtatutia risasi, lakini yule bwana hajengi, hajengi, hajengi. Arejeshewe mwenyewe mwananchi wangu.

Kwa hayo machache nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, nitaunga mkono baada ya kukubaliwa Kamati Teule. Hapo naunga mkono hakuna tatizo lolote.

Mhe. Mwenyekiti ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni hii na mimi kuweza kuwa miongoni mwa wachangiaji katika Wizara hii muhimu sana kwa maslahi na ustawi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kazi ngumu na nzito aliyopewa. Nataka niseme Mhe. Waziri kwa kweli ni kiungo lazima tukubali. Mhe. Waziri wa Wizara hii sasa hivi huyu mimi namchukulia kama ndio *midfield* wa Serikali, pahala popote penye matatizo ukimpeleka yeye basi anaweka sawa. Tumeanza kutona jitihada zako baada ya kuingia katika

Wizara hii tayari umeanza kushughulikia baadhi ya mambo mbali mbali ikiwemo migogoro ya ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, ingawa katika migogoro hii nitamuomba Mheshimiwa tusimvunje mgongo mapema. Yeye tumuachia ashughulikie migogoro ya wananchi na serikali lakini sisi achuachie tushughulikie ile migogoro ya unyang'anywaji watu ardhi lakini vile vile na ubadhirifu katika taasisi mbali mbali zilizokuwa chini yake.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimpongeze Katibu Mkuu kwa sababu Katibu Mkuu mimi namuheshimu sana, alikuwa ni kocha wangu. Ingawa mimi nilikuwa ni timu pinzani na timu yake aliyokuwa anaifundisha ya African Keed mimi nilikuwa ni mchezaji wa Pani Keed na mimi nilikuwa ndio mfungaji mkubwa. Kwa hiyo hawa wote ni watu wangu wa karibu na nawaelewa vizuri. Lakini kwa bahati mbaya leo tupo kazini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo sasa nakuja katika mchango wangu wa Wizara hii. Kwanza naanza jimboni nyumbani, kwa kweli nasikitika sana na nimeshasema sana katika bajeti hii ya Wizara hii kwamba angalau nipatie hati miliki ya miradi ambayo imo ndani ya jimbo langu ambayo wananchi tumejitolea, tumejikopesha, tumedaiwa, tumelipa, mpaka leo miradi ile inafanya kazi bado hatujapatiwa hati miliki.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali yangu ya Kwamtipura jana Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) alikuwa anaiambia serikali imkabidhi. Mimi nashangaa mtu kitu chake anaiambia serikali imkabidhi. Mimi sitaki kusema serikali inikabidhi kwa sababu jengo lile ni letu, tumelijenga kwa nguvu za wananchi, tunashukuru tumepata Msaada wa TASAF. Hii nayo ni miradi ya wananchi, tunashukuru sasa hivi serikali imetusaidia kumalizia lakini bado lile ni jengo la Hospitali ya Wananchi wa Kwamtipura. Kwa hivyo tunamuomba Mheshimiwa atupatie hati miliki ili na sisi tuweze kufanya kazi zetu kwa uhakika.

Vile vile jengine kuna kiwanja ambacho tunashukuru tuliwahi kupimiwa katika nyumba ya *Government Press* pale ambapo tunataka kujenga Sekondari. Lakini tunashindwa kujenga mpaka leo hatimiliki bado hatujapewa, ingawa kupimwa kimeshapimwa tayari. Nilikuwa naomba hili. Lakini jengine leo kwa sababu nina mambo mengi na nahisi kutokana na muda sitoweza kuyasema yote hapa nina bahasha naomba muhudumu aje akamkabidhi Mhe. Waziri hawa watu atawashughulikia kwa mujibu wa taratibu wa kiofisi.

Hapa kuna kadhia ya mzee wetu huyu mwalimu kasomesha siku nyingi alikuwa Lumumba pale analo jengo lake alikuwa anaomba serikali iweze kummilikisha ingawa umiliki anao lakini waweze kumthibitishia ili aweze kufanyia shughuli zake. Anaitwa Mhe. Abdalla Mohammed Said Abeid, nadhani anamjua kwa sababu ni mwalimu mwenzake alikuwa.

Vile vile nina ndugu Hamadi Maalim Khamis, huyu ni mtu wa Kizimkazi, Shamba lake limevamiwa na wananchi Tomondo amehangaika sana serikalini amefika kwa Mkuu wa Mkoa sasa hivi anaomba basi katika hayo majengo ya serikali mnayotaka kuyauza au kama mnashamba jengine mumpe ili waweze angalau kufidia. Na yeye vile nakuletea document zake utashughulika naye kama kawaida yako.

Nakushukuru wale watu wanaokuja na malalamiko tukikuletea unawahudumia vizuri. Tunakushukuru sana kwa hilo. Kuna mwengine huyu mwananchi kaleta malalamiko yake, amelipa ardhi amepewa kiwanja lakini viwanja hivyo vimegeuzwa makaburi, anaomba apatiwe kiwanja chengine. Ndugu Mhudumu naomba mpelekee Mhe. Waziri haya sitaki anijibu haya naomba ayachukulie tu mwenyewe kwa wakati wake unaofaa.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja sasa katika utendaji wa Wizara. Tuna taratibu zetu za utumishi na kwa kuwa tumeunda Wizara ya Utumishi na Utawala Bora lakini bado tunaona katiak utekelezaji kuna baadhi ya vifungu tunakuwa tunavikiuka. Katika Wizara yako kuna huyu Mkurugenzi wa Upimaji, huyu sasa hivi anakaimu karibu miezi 16 hivi sasa. Kuna vijana ambao wana uwezo mkubwa ambao sawa sawa na yeye.

Kanuni ya Utumishi ukiangalia kifungu cha 56 kinasema kwamba mtu anaweza kukaimu nafasi si chini ya miezi 12 lakini huyu keshakaa miezi 16. Leo namuomba sana Mwanasheria Mkuu serikali yetu bado kuna nafasi sasa hivi mwaka karibu wa pili na unaendelea wa tatu kuna nafasi bado zinakaimiwa kaimiwa. Watu wanapopewa dhamana kukaimu kaimu bado anakuwa hawezi kusimamia dhamana zake vizuri. Tunaomba Mhe. Mwanasheria Mkuu wewe ndio mshauri Mkuu wa serikali, mpaka miaka miwili bado sehemu zinakaimiwa mimi nafikiri bado tutakuwa hatujajipanga vizuri.

Nikiondoka hapo sasa hivi nakuja katika kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri, naanza na Kanuni 98 (b) ya Baraza la Wawakilishi inasema inaniruhusu kuondoa shilingi 100 katika Idara yoyote ambayo nahisi utendaji wake hauniridhishi. Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba kifungu (c) cha Kanuni ya 89 kinasema kwamba nampunguzia fungu Mhe. Waziri katika

Idara hizi nitakazozitafu ambazo siridhiki na utendaji wao na sababu nitazieleza.

Lakini vile vile kifungu (f) kinamtaka Mhe. Kiongozi wa Shughuli za Serikali aweze kutoa kauli ili tuweze kuridhia haya mambo mengine ambayo kama hatukuridhika tutatumia kifungu cha 98(g) kama hakuna budi kupiga kura. Mimi sioni twende mpaka kwenye kupiga kura. Kwa sababu sote hapa tumeletwa kwa mujibu wa maslahi ya wananchi. Sisi kama ni Wawakilishi kazi yetu kuisimamia serikali katika utekelezaji wa shughuli zake.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba katika Idara ya Ardhi sitopitisha kifungu tena cha mapato. Lakini vile vile katika Mamlaka ya Maji, vile vile nitazuia fungu kutokana na uzembe ambao unafanyika ndani ya Mamlaka kila siku wananchi wanabakia na dhiki ya maji.

Nakuja sasa katika michango yangu kwa nini nikasema nitezuia fungu katika Mamlaka ya ardhi. Nina orodha hapa za wawekezaji mbali mbali ambali wamefutia *lease* zao kinyume cha sheria. Nilipokuwa nikichangia hotuba ya Makamo wa Pili wa Rais nilieleza kwamba tayari hapa Zanzibar watendaji wa Mamlaka hii ya Ardhi kwa kushirikiana na baadhi ya madalali. Kwa bahati nzuri katika *document* moja nimeona mpaka jina lake Shekh Saleh, huyu ndie dalali mkubwa anayetumiwa na Mamlaka ya Ardhi.

Mimi niliwahi kukamata *document* yake ambayo alikuwa kuna maeneo alikuwa anayanadia anatafuta wawekezaji. Kwa bahati mbaya eneo lenyewe ni eneo la Kampuni ambayo ilipewa na serikali hii hii Kampuni ya NAKHEEL ambayo ni Kampuni Tanzu ya wanaita, *LEISURE CORP ya Dubai World Company*. Mheshimiwa hawa jamaa wamewapelekea mpaka malalamiko ZIPA kwa kulalamikia kwamba eneo lao limechukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme eneo hili la Muyuni/Matemwe mpaka leo bado uhalali wake wa kufutwa haujakuwepo. Kwa sababu muwekezaji huyu anamuandikia barua Mhe. Waziri, hakujibiwa na vile vile kifungu alichokitumia Mhe. Waziri naomba vile vile na mimi nataka nikisema kama yeye alivyosema. Anasema kwamba *"The recondition now in place under the revised regulation section 48"* ambacho kifungu hichi Mhe. Waziri, ndio kila mara alikuwa akikitumia kwa ajili ya ufutaji.

Lakini yeye anasema "*Were not in force at the time lease was signed and would need to be specifically included in amendment agreement were there to apply since no time limit was part of lease".*

Kwa hivyo yeye ina maana alipopewa ile *lease* ilikuwa ile *time limit* ilikuwa haipo. Kwa hiyo yeye kitu anachosema *"Further more the same section of the act state that the holder of lease shall be given three months notice to rectify the default before termination of the lease. This has not been done*"
Mhe. Mwenyekiti, huyu ni muekezaji anaiambia serikali kwamba kifungu hicho hicho ambapo cha chini kilikuwa kinasema kwamba muwekezaji yule anapotaka kufutiwa *lease* yake apewe *notes* ya miezi mitatu. Hicho kitu hakikufanyika kwa hiyo huyu bado, tena yeye katika domument yake kwa sababu ni refu na nina mambo mengi sitaki kuitaja sana kwa sababu anasema yeye yupo tahari kukaa na serikali kuangalia ni namna gani ya kuendeleza ule mradi wake. Kwa sababu alikwisha kuanza kuendeleza lakini alisita kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani.

Mhe. Mwenyekiti, eneo hili leo kwa bahati mbaya amepewa muwekezaji mwengine anayeitwa ICAS LIMITED na eneo hili Mhe. Mwenyekiti kitu cha kushangaza, juzi nilisema kwamba hizi kamati zetu zinadharauliwa na watendaji. Tuliwaita na tukawambia sisi tunataarifa kwamba eneo la NAKHEEL Matemwe lilifutwa na yakauziwa Makampuni Hewa. Na makampuni yenyewe ni manane, kwa ukoa muda leo sina haja ya kuyataja tena kwa sababu juzi tukenda kwenye Hansard katika Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais niliyataja.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikukabidhi aje muhudumu ili akukabidhi makampuni hewa hawa yaliyokuwe eneo la NAKHEEL. Makampuni haya Mhe. Mwenyekiti, tumejaribu kufatilia mapaka Mambo Msege hayajakuwa *register*. Haya ni Makampuni hewa kwa hivyo nakubaliana na ile kauli ya kusema iundwe Kamati Teule ili tukayachunguze Makampuni haya manane.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nikija kuna hoteli moja inaitwa *SUNSET PARADISE RESORT* hii walipewa lease mwaka 2010 na hawa wamelipa ZRB tunazo hapa. Kuna *document* hii ya *Sunset Paradise* ambao hawa wamelipa *Zanzibar Revenue Board*, hii wamelipa US$ 39 elfu lakini leo *lease* hii imefutwa imepewa Kampuni ya *Sea rock and Resort* kwa US$ 2,500.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti

Mhe. Mgeni Hassan Juma (Mwenyekiti): Waheshimiwa namna mnavyogonga meza iko hatari hizo meza zikaja zikavunjika. Waheshimiwa taratibuni.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Nakushukuru Mwenyekiti, nipeni raha nizungumze. Mhe. Mwenyekiti, US$ 39,000 tumefuta *lease* hii tumempa mtu kwa US$ 2,500 *are we serious*? Kweli tuko serious katika uchumi..

Lakini sio hii tu Mhe. Mwenyekiti, kuna kampuni nyengine ambayo vile vile inaitwa ***Sagopal Resort*** hawa ninazo *document* zao hapa wamelipa *ZRB* US$ 11,565 na *document* tunazo hapa za *ZRB* ambazo mpaka mwaka 2012 tayari wameshalipa, lakini leo *lease* hii imefutwa amepewa *The Coconut Resort and Villas* kwa US$ 5,000 Mheshimiwa tunakwenda wapi. Halafu hii *The Coconut Resort and Villa* hii ni kampuni hewa vile vile. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hii lazima tukachunguze usahihi wake.

Lakini vile vile kuna Kampuni nyengine inaitwa ***Soverent Sand Resort,*** hawa na risiti hii hapa ya *ZRB* malipo yao, mwenyekiti wewe leo pokea tu hapa tumejiandaa. Mhe. Mwenyekiti, US$ 13,365 hii tayari wameshalipa *ZRB* juzi tena tarehe 15/06/2012 imefutwa imepewa kampuni hewa inaitwa *The Address* tena kampuni hii hawa ndio wale wachakachuaji kwa sababu hizi kampuni bado hazijasajiliwa, kampuni iliyosajiliwa inalipa *ZRB* imefutwa inapewa kampuni hewa inalipa US$ 3,000 kutoka 13,365.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, kuna hoteli inaitwa *Residence Hotel*, hawa ninayo *document* yao hapa vile vile, hawa walikuwa wanalipa serikalini US$ 80,000 kwa mwaka, sasa hivi imepunguziwa wanalipa US$ 48,100 kwa mwaka. Mhe. Mwenyekiti, *are we serious*?

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mimi nikiwa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti tunapitisha Bajeti kuu ya Serikali pale tunahangaika fungu hiki peleka huku, hili peleka huku, serikali hatuna uchumi, Mheshimiwa fedha hizi hapa ndio siku zote tunaposema jamani serikali pesa zipo lakini tatizo letu hatutaki kushughulikia mapato. Leo kwa bahati mbaya Waziri wa Fedha hayupo lakini yeye ndiye aliyetwambia tukatafute mapato yanayovuja, mapato yanayoachiwa ovyo ovyo, hawa ndio wawekezaji wanaofanya biashara walipe kodi, tunawaacha wafanyabiashara ambao wanaingiza fedha ambao walipe kodi tunakuja kuwakamua wananchi, tumewaongezea bili za umeme, tumewaongezea bili za safari hatuwezi tukaruhusu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wenzetu kule Bungeni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Waziri Mkuu yeye hasubiri serikali kuburugushana na Wabunge, kupiga kura yeye wanasema tu, wakati mwengine hata Wabunge hawasemi iundwe tume, yeye anasema kutokana na haya mliyoyaona hebu undeni tume nendeni kachunguzeni. Mimi nafikiri Mhe. Makamu wetu wa Pili wa Rais msikivu, kwa sababu kupiga kura mimi nitashangaa, tena hata mawaziri wakikataa kuunga mkono sisi tukaangalia ufisadi mimi nitashangaa itakuwa hii serikali ya watu au ya nani.

Mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, hapa leo sitaki niseme sana kwa sababu haya mambo kwa kweli yako mengi, lakini Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu, nimesikia taarifa kuna hiki Kisiwa cha Kwale nacho kimeshatoka kimepewa Kampuni inaitwa *The Rihela Limited,* mimi naomba tu katika hiyo kamati itakayoundwa na mimi japo sikuteuliwa lakini siku ya kwenda kukagua hicho kisiwa na mimi mnichukue ili nikaone. Kwa sababu huyu kapewa kisiwani tunajua baadae atakuja kuongeza ongeza huko baadae.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, sisi tunaposema kwamba serikali ina pesa lakini inawakamua wananchi bila ya sababu zozote. Mimi kuna document nimezi-*reserve,* Mhe. Waziri akija akinibisha tutakuja kushindana kwenye vifungu kwa sababu *document* hizi zote za serikali. Sasa ndio maana nikasema tusende kubishana aturuhusu basi undeni hiyo tume nendeni kachunguzeni.

Jengine juzi tulipokuwa wananchi wamekuja kutulalamikia kwa sababu sasa hivi wananchi wanatukubali, mwananchi akinyang'anywa au akidhulumiwa kidogo anakuja, wananchi wa Matemwe walikuja, kuna mmoja anaitwa Ndevu alinipigia simu nikamwambia njoo tukazungumza siku ya tatu yake akaitwa akaambiwa basi tutakulipeni. Mhe. Mwenyekiti, utaratibu umekiukwa kawaida ya *lease* inavyotoka inatakiwa kwanza kama kuna watu walikuwa wanafanya shughuli zao pale wanalipwa *compensation* halafu baadae ndio inatoka hiyo *lease* yenyewe. Lakini leo *lease* imeshatoka eti wananchi wameitwa siku ya Jumamosi kwa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini wende wakalipwe, wakalipwe nini na *lease* keshapewa mtu.

Mhe. Mwenyekiti, *lease* ile ifutwe na kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, *lease* hiyo kapewa huyo dalali wa huko Muyuni, Matemwe yeye ndiye aliyepewa eneo lile, maeneo yale ya Matemwe yalikuwa yananadiwa kwa US$ laki saba na nusu kila eneo moja *plot* inane, sasa fanya mahesabu mwenyekiti dola laki saba na nusu mara nane ngapi? Sasa inaonesha keshauza ndio kamuuzia huyu mwengine sasa hivi anataka kwenda kuwalipa *compensation* wananchi wa Mkoa wa Kaskazini.

Mhe Makamu wa Pili wa Rais naomba lisimamiwe hili, wananchi wa Matemwe siku ya Jumamosi kwanza wasilipwe mpaka kieleweke eneo hili limefutwa vipi, kapewa nani, sasa hivi wananchi nyinyi leteni tu, haki zetu tutazizungumza humu ndani ya Baraza. Siasa zishakwisha sasa kazi tu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nataka nimaliziemalizie tena maana yake unajua muda mwingi. Mhe. Mwenyekiti, nakuja Mamlaka ya Maji. Mwaka jana nilisema bajeti ya Mamlaka ya Maji sitoipitisha, na nilimuomba Mhe. Waziri kipindi kile rafiki yangu mpenzi Mhe. Ali Juma Shamuhuna

nilimuomba kwamba hii Mamlaka ya maji ipewe Brigedia ya Jeshi mwaka mmoja tu maji yatatoka, ninazungumza hivi kwa ushahidi. Mhe. Mwenyekiti, nina *document* ya wao wenyewe Mamlaka ya Maji wanalaumiana namna gani wanavyonunua *pump* mbovu, matangi mabovu, lakini vile vile na haya mabomba ya kusambaza maji mabovu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana hii Mamlaka nayo tukaichunguze kuna uzembe mkubwa. Mimi juzi tulipokuwa tunazungumza Wizara ya Utumishi wa Umma katika ile Idara ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali nilisema ifanyiwe *study* au uchunguzi wa *human resource auditing* na hii Mamlaka ya Maji ikafanyiwe *human resource auditing*. Kuna miradi ya *ADB* nasikia *ibnukhudhaimata* na *ibnukinana* wamejazana tele mambo hayendi, Mheshimiwa hatuwezi tukenda hivi. Sasa hivi tunapitisha sisi vifungu hivi sijui kununua *stationery*, wakurugenzi wote sasa hivi mimi naomba mchunguzane, wakurugenzi wote serikalini kila mmoja ana kijiofisi cha kuuza *stationery* kwa bajeti tunazozipitisha hapa, leo hawa wafanyabiashara watamuuzia nani hizo *stationery* zote mmefungua vijikampuni vyenu.

Mhe Mwenyekiti, hapa tunapitisha shilingi milioni arobaini, thalathini, mtu anatoka anakwenda kufungua *stationery* yake hatuwezi tukenda hivi, hii serikali bwana sasa hivi. Kuna rafiki yangu mmoja mpenzi yeye alikuwa ana msemo mmoja anasema, "mmekula matunda ya mapinduzi mshayamaliza sasa hivi mnaanza kulana wenyewe kwa wenyewe". Mimi nadhani sasa hivi jamani tuyaache.

Vile vile ninaye rafiki yangu mwengine mpenzi nampenda sana na nikisema yeye hupenda kunichekacheka tu, lakini misemo yake huwa naipenda sana. Mhe. Mwenyekiti, matunda ya Mapinduzi tumeshayamaliza sasa hivi tunakulana wenyewe kwa wenyewe, wananchi waachiwe.

Kwa hivyo, mimi siku ya ufunguzi wa kibanda kile cha Mamlaka ya Maji pale Kijitoupele nilisikia kauli pale sijui masikio yangu siku ile yalikuwa mazito au vipi, Mhe. Waziri aje anisaidie. Naambiwa kile kibanda pale kimejengwa kwa shilingi 45 milioni, sasa hii masikio yangu nafikiri siku ile yalikuwa na matege, sasa Mhe. Waziri aje anithibitishie na akinithibitishia kwamba kimejengwa kwa shilingi 45 milioni basi hiyo tume itakayokwenda kuichunguza Mamlaka ya Maji na pale itabidi twende, manaake nyumba ya shilingi 45 milioni mimi nakaa mpaka na wajukuu wangu kile kibanda tu pale ni shilingi 45 milioni labda iwe kuna kauli nyengine pale.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika Mamlaka ya Maji katika huu mradi wa Mkoa wa Mjini na Magharibi pale tume-*invest* pesa nyingi na serikali yetu

inapokopa pesa baadae zile pesa zinarudi inakuwa kama ni deni la taifa, deni la taifa kila siku linaongezeka. Mheshimiwa fedha zile laiti kama tungeligaiwa majimboni kila mmoja akaamua akachimbe visima katika jimbo lake basi tungekuwa tunakungwa maji mengi, lakini kwa bahati mbaya mradi ule mpaka leo na hakuna dalili. Na tuna taarifa kwamba lile *tank* pale halijai, hebu tupeni sababu kwa nini *tank* lile la Welezo halijai?

Mhe. Mwenyekiti, mimi naona uchungu maji yanakwenda kwa Mhe. Ismail Jussa Mji Mkongwe yanapita ndani ya Jimbo la Kwamtipura lakini sisi watu wetu wanaota vipara, mimi mwenyewe hiki kipara changu cha mambo tu, lakini wanawake wa Kwamtipuira hawapati kusuka, siku hizi Kwamtipura huwezi kumjua Mzungu nani, Mchina nani, wote wanatia nywele za kubandika kwa maji. Naomba sana, Mamlaka ya Maji kwa kweli tumekupeni pesa nyingi sana na miradi mingi bado tunaendelea nayo lakini tunahitaji na nyinyi tuje tukuchunguzeni. Unajua Mhe. Mwenyekiti, unapochunguzwa ufurahi kwa sababu kama Mhe. Makame Mshimba katetea Shirika la Umeme, wanachunguzwa huko ripoti itakuja. Sasa na hii Mamlaka ya Maji naionea huruma vile vile pengine pesa wanazopewa hazitoshi.

Mwakajana tuliambiwa ile *network* ya *pump line* ile ya maji bado, tukaambiwa sijui kuna mabomba yana *linkage*. Mhe. Mwenyekiti kama mabomba yangekuwa na *linkage* ingelikuwa humu mitaani hamkaliki nyekenyeke, lakini maeneo makavu haya maji yanakwenda wapi? Visima vimechimbwa pale *tank* mpaka leo halijai, hebu tupate sababu kwa nini halijai mana tunaambiwa kwa kuwa halijai ndio maji hayaingii katika mitaa yetu.

Mhe. Mwenyekiti, najaribu kujitahidi kumalizia, lakini katika hili eneo Mheshimiwa pamoja na jitihada zako lakini eneo la Mchangamle bado kuna malalamiko. Sasa hili sijui katika hiyo kamati yako uliyoiunda huko ya kufuatilia migogoro ya ardhi, lakini naomba hili suala kama limeshakaa muda mrefu wapewe wananchi kwa ajili ya kulifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa nataka nimalizie Shirika la Umeme. Shirika hili sasa hivi limo katika uchunguzi lakini mimi kitu ninachokiomba na hata katika hotuba yangu kama Mwenyekiti wa Wenyeviti nilisema kwamba, bili hii ya umeme iliyoongezwa ilikuwa si pahala pake pa kuongezwa kwanza, ilikuwa kwanza tusubiri ule uchunguzi ukamilike. Kwa sababu mapato mengi tumegundua Shirika la Umeme yanavuja, leo mwananchi wa kawaida anadaiwa shilingi 15,000 anakatiwa umeme, lakini vile vile leo kuna ma-*giant* yanadaiwa mpaka shilingi 25 milioni hayajakatiwa umeme. Sasa kwa kuwa hawa wengiine inaonesha wanawaonea haya kwa hivyo matokeo yake lile bili limegawiwa wateja wa umeme wangapi tukafanyiwa mahesabu tukagawiwa.

Mimi nitakuja kuzuwia fungu hili la mapato, kwa sababu fungu la mapato ndio hizi ada mmeongeza kutoka shilingi bilioni ngapi sijui mpaka ngapi, sio kama tunakataa lakini kwanza tujiridhishe na ule ubadhirifu uliofanywa katika Shirika la Umeme isijekuwa kwamba ndio tuna *compensate* katika kuwalipisha wananchi. Kama tutaridhika kwamba ni huduma ambayo inahitajika basi huko baadae tutaendelea kuridhia, lakini nilikuwa naomba sana katika maeneo ambayo serikali inatakiwa kufidia ni haya maeneo ya umeme, kwa sababu haya tukitaka tusitake wananchi wetu kipato chao cha chini, mshahara wao wanaopata ni mdogo, kwa kuwa mshahara mdogo leo bili ya umeme imeongezeka karibu asilimia 60 mwananchi huyu tunampa hali ngumu ya maisha.

Mhe. Mwenyekiti, ili usije ukaniambia umebakisha dakika tano leo dakika tano zangu nakopesha, kwa sababu tayari nitakuja kusubiri katika vifungu. Lakini naamini Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hatosubiri tukazuwia vifungu atakuja kutoa kauli tu, na waziri wake kwa bahati hayupo atakuja kutwambia Waheshimiwa hiyo kamati yenu nitaiunda basi kafanyeni kazi, leo vifungu vyote vitapita kwa muruwa.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, samahani. Kuna eneo kule Nungwi siku ile tulipokuwa kwenye kambi kuna wananchi walituita tulikwenda kama Waheshimiwa watano nikiwemo mimi na Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Ali Salum na Waheshimiwa wengine. Mhe. Mwenyekiti, kuna eneo wakubwa wamegawana, eneo hili alikuwepo mwekezaji kawalipa wananchi na wananchi wale wamenyamaza kimya yule Mzungu baadae sijui kafukuzwa au kakimbia mwenyewe, unaweza ukakimbia mwenyewe bila ya kufukuzwa, hiyo jawabu nafikiri Mhe. Waziri atakuwa anaijua yeye. Lakini eneo lile baada ya kurudi serikalini wakubwa mmegawana. Sasa nilikuwa naomba kabla kwenye vifungu mimi sitaki kama Mhe. Hija Hassan alisema atawataja mimi simtaji mtu, mimi naomba tu lile eneo Mhe. Waziri kesho urejeshewe mwenyewe lirudi serikalini ili sasa tuje tusubiri hao wawekezaji ambao wataleta tija kwa nchi yetu sio wakubwa.

Mhe. Mwenyekiti, humu sisi tunalipwa pesa hatuji na jembe, hatuji na shoka wala hatuji na panga, humu tunakuja na maneno ya wananchi wetu. Sasa leo tunalipwa mishahara, tunapewa gari, tunapewa na mafuta tunakwenda kuchukua na maeneo ya watu hee! Hao wananchi watatuleta tena humu?

Kwa mara ya kwanza hivi karibuni Kizimkazi Mhe. Rais wetu Mpendwa Dr. Ali Mohammed Shein.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza ulikuwa umeshamaliza.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Aa nilikuwa nimeshamaliza, basi namalizia hapa. Rais wetu mpendwa alipokelewa kwa mabango, mabango yenyewe sio ya kumpongeza watu wanadai ardhi zao. Sasa tusije tukafika pahala waziri wetu mpendwa Waziri wa Ardhi mpya asije akapokelewa kwa mabango, eneo lile tunaliomba katika hii ripoti ya kamati teule katika hii kamati itakayoundwa ikalichunguze ili lirudi serikalini, sisi hatutaki mtu afungwe wala nini mali zote zikisharudi serikalini sisi tusharidhika.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, naomba nikae kitako kama nilivyosema sitopitisha bajeti hii mpaka pale yale mambo ambayo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais akiniridhisha. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma kidogo tu nataka nikupe angalizo katika mchango wako umesema kwamba unanikabidhi baadhi ya *document*, sasa nilikuwa naomba unikabidhi mimi kabla ya kuzipeleka kwa waziri kwa sababu huo ndio utaratibu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa roho upande nitakukabidhi lakini na mimi nitabakia na kopi zangu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii niweze kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makazi, Maji na Nishati. Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake hii mwanana kabisa, hotuba nzuri sana, ina mambo mengi, nimshukuru sana Mhe. Waziri, lakini vile vile nimpe pole kwa kazi ngumu aliyonayo katika wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikianza mchango wangu nitaanzia kwenye ukurasa wa tano wa kitabu hiki cha Mhe. Waziri kwenye Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Mhe. Mwenyekiti, kama utakumbuka Baraza lako hili liliunda kamati teule na ripoti yake ikatoka na kazi kubwa sana ilifanya kamati. Mimi nilikuwa ni mjumbe wa kamati ile, kulikuwa kuna kitu kilijitokeza nimeona leo bora nikizungumze katika bajeti hii, tulipata tabu sana katika wizara hii namna ya kumpata Katibu Mkuu, kila ukimwita yuko safarini, yuko BLM hapatikani, sasa sijui leo hapa kwenye kuombwa fedha yupo mana tunataka tuje tumkabidhi fedha, sijui atakuwepo au ndio yuko safarini vile vile sina uhakika. Sasa mimi nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri hebu tusaidie hizi safari hasa za huyu Katibu Mkuu katika mwaka huu zilikuwa ngapi na alikwenda wapi na wapi na nchi imefaidika vipi kwa safari hizo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niendelee mbele nikishapata jawabu hilo sina tatizo na fungu la idara hii labda kwa huko mbele ninakoendelea. Nije kwenye ukurasa wa 11 Idara ya Ardhi na Usajili. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa

nachangia hotuba yangu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais nilizungumzia sana juu ya migogoro ya ardhi, nikapiga kelele sana, nikasema sana na nikaomba tuunde kamati teule. Lakini kwenye majumuisho ya Mhe. Waziri alipokuja kutoa majumuisho yake hapa akawa mgumu lakini baada ya kuja kukikamata kifungu tukakubaliana kwamba kamati teule basi tuisubiri Wizara ya Ardhi au wizara husika tuje tuiunde pale.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ile siku imewadia leo ndio ile bajeti ya Wizara ya Ardhi, sasa narejesha hoja yangu namuomba sana Mhe. Waziri atukubalie hili ile hoja nimeirejesha hapa leo namuomba sana na mimi namfahamu Mhe. Waziri hana tatizo, kawaida yake tunamfahamu kwenye Baraza hili simgumu wa hivyo, mkishamuelewesha jambo amelielewa hana tatizo. Kwa hivyo, nakuomba sana Mhe. Waziri, mimi sitaki niseme sana katika eneo hili wenzangu wameshalizungumza sana. Sasa nakuomba utakapokuja uje na jawabu la kutukubalia ombi letu hili ili kamati iundwe tufanye uchunguzi juu ya migogoro ya ardhi ipo ya aina nyingi.

Mhe. Hamza Hassan amesema sana hapa juu ya wawekezaji, lakini ipo migogoro ya wananchi kunyang'anywa ardhi zao kila mkoa, kila wilaya utakayokwenda migogoro hiyo imo hata kwenye kitabu chako umetuandikia humu. Kwa hivyo, unakiri kuwa hivi vitu vipo sasa kama vipo basi hili ni Baraza la wananchi hawa ndio wananchi wenyewe, tunaomba tusaidiane kazi isiwe kazi hii inafanywa na serikali tu peke yake. Sasa tutoe nafasi na kwa wananchi nao wafanye hii kazi. Kwa hivyo, nakuomba sana Mhe. Waziri tukaiangalie migogoro katika wilaya zote, mikoa yote iko mingi mno hivyo tuichanganue tuiweke kwa pamoja tukaitatue kwa sababu ile imekuwa donda ndugu haliponi, kila ukija hapa migogoro imo, kila ukija migogoro imo, sasa hebu tutafuteni dawa na dawa ni kuunda kamati tukenda tukatengeneza dawa kule kunakohusika.

Nilisema mchango wangu kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais kwamba tatizo jengine kubwa la migogoro hii kuwa haitatuki hao waliokuwa wa kutatua hiyo migogoro wao wenyewe mgogoro, hawawezi kutatua wanawaonea bure wale wananchi, wanawadhulumu wengine wananchi, watu wamevimba matumbo huko kwa dhulma tu wanawadhulumu wananchi ardhi zao na kwa sababu wananchi wale ni wanyonge hawajui hata pa kuelekea wanatishwa hadithi inakuwa imekwisha. Kwa kweli hiki si kitendo kizuri na kinarejesha nyuma sana maendeleo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa sitaki niseme mengi kwenye idara hii yameshazungumzwa mengi, lakini mimi nimwambie kabisa Mhe. Waziri kama hakuja na jawabu zuri juu ya uundwaji wa kamati teule katika hili fungu la idara hii nitaling'ang'ana sitoridhia kuingiza fedha pahala ambapo pana

migogoro ambayo ni ya wananchi wetu. Sisi ndio waliotuleta hapa tusingekuwepo hapa kama si wananchi, wametuleta hapa tuje tutetee maslahi yao, sasa unaweza kukuta kuna viongozi kabisa wa serikali wanahusika katika migogoro hii. Kwa kawaida ya viongozi huoneana haya hutizamana mara mbili hivi ah, haya lakini hapa hukumtendea haki inakuwa ndio imekwisha, tunataka tupeleke nguvu za wananchi ili wakapewe haki zao.

Mhe. Hamza amezungumza hapa kuna baadhi ya wakubwa wamejilimbikizia mali za ardhi, wamechukua maeneo makubwa makubwa huko wanagawana wanasubiri kuuza, watu wamekaa *standby* we katafute mteja tu huko, ukishapata mteja lete biashara imekwisha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hiyo yote nayo ni migogoro hiyo. Kwa hivyo, katika hili mimi naungana na wenzangu hawa kuhakikisha kwamba Mhe. Waziri atakapokuja akituridhia katika hili hatuna mushkeli, lakini kama atakuwa anahisi hatuko sawa sawa basi fungu hili na mimi sitolipitisha.

Mhe. Mwenyekiti, nisogee mbele kidogo katika ukurasa wa 34 kwenye Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi. Mhe. Mwenyekiti, kuna mchangiaji mmoja alichangia hapa juu ya kuweko na kamati ya kutambua anayedaiwa kupewa nyumba na Mzee Karume. Hii kamati kusema kweli Mhe. Mwenyekiti, imeshakuwa ya siku nyingi, hata ukiangalia kwenye ripoti za kamati za kudumu za Baraza kwenye ukurasa wa 64 imo hii, Kamati ya *PAC* ilipopita na iliagiza kwamba ripoti iletwe tuione, lakini mpaka leo haijaletwa ripoti ile. Sasa sijui kwa nini na ubaya wenyewe kwamba kamati ile inalipwa posho ni fedha za wananchi zile, sasa tunashangaa hii kamati au imekuwa kama idara, maana inaonekana inafanya kazi mfululizo inaendelea tu, haijulikani itamaliza lini, haijulikani inafanya nini, sasa itakuwaje kamati hii miaka mine au mitatu kamati gani hiyo hii si itakuwa idara tunamuongezea mzigo tu Mhe. Waziri huyu, imekuwa idara mpya hii.

Sasa mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja aje atupe ufafanuzi wenye kujitosheleza kabisa juu ya kadhia hii. Kamati hii imemaliza kazi, kwenye kitabu kaandika mle kidogo, lakini kanyofua kidogo tu hatukupata ufafanuzi mzuri. Mimi namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hebu atueleze hasa kinagaubaga juu ya hii kamati ilipofikia na uamuzi ambao umefikiwa. Kwa sababu tunapoambiwa hili suala liko linaendelea mbele kwa hatua za kiserikali tunataka kujua na sisi wananchi huku, kwa sababu hizi fedha zinazotumia kamati hii ni fedha za walipa kodi, hebu tuelezeni mmefikia wapi juu ya hili.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la nyumba 79 ambazo walipewa Wakfu na Mali ya Amana. Wakfu ilipewa nyumba zile za warithi wale ambao wanastahiki

kurithiwa zile nyumba itakuwa nyumba zile katika majengo mapya yale kuwagaia wenyewe mana wao ndio wenye dhamana ya kugawa ile mirathi. Wakfu ilizigawa zile nyumba ikabakisha nyumba 20 kwamba kidogo wenyewe walikuwa wanaonekana wako tabuni kupatikana, lakini kwa mujibu wa sheria Nam. 2 ya mwaka 2007 katibu wa Wakfu pale ndio mwenye dhamana ya nyumba zile, lakini bahati mbaya nyumba zile zilibakishwa kule wizarani au kwenye idara hii hazikurudi tena kwenye wakfu, wakati yeye wakfu ndiye aliyetakiwa kukaa na nyumba zile kama anazikodisha au kuzipangisha mpaka wanapotokea wenyewe anawakabidhi na fedha ambazo kakodisha awakabidhi warithi wale. Lakini leo nyumba zile zimechukuliwa zote hazionekani yaani hazikurudi tena wakfu walipokwenda kuziuliza kule hakuna jawabu la kuridhisha.

Waliwahi kupewa nyumba 79 nafikiri wakagawa 59 zikabaki ishirini, zile zilitakiwa zibakie kwao pale na kama atakuwa hakutokea mwenyewe mali ile inakuwa inaingia kwenye tilka wenyewe wanaita kule mambo ya mirathi hayo kidogo wataalamu wa mambo ya mirathi maalim Makame Mshimba anafahamu hayo, sasa nyumba zile hazikurudi.

Mimi nilikuwa nataka ufafanuzi kidogo Mhe. Waziri, utapokuja hebu tueleze nyumba hizi ziko wapi na amegaiwa nani, fedha zile za warithi wale zinakwenda wapi. Mana msimamizi wa mambo ya mirathi ni Wakfu, sasa kama wizara ndio mmezichukua nyinyi mtueleze hapa kwamba nyinyi ndio wasimamizi wa mirathi siku hizi badala ya Wakfu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikiendelea mbele niende kwenye ukurasa wa 50, naruka kidogo halafu nitarudi huku, maana ndio mchezo wenyewe wa kurukaruka unakuwa hapo, dakika unazotupa kidogo sasa lazima wende huku halafu urudi huku. Ukurasa wa 50 kwenye Idara ya Nishati.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napata shaka na idara hii namna ninavyoiona kwenye vitabu kazi zake na mambo yake, lakini siioni kufanya shughuli zake utafikiri hii idara haipo. Kama utachukua *hansard* yangu mwaka jana nilizungumza juu ya idara hii, hatuioni zile shughuli zake. Kwa sababu hii Idara ya Nishati na Madini, lakini leo hii ukiuliza habari ya kodi za mafuta au biashara ya mafuta upandaji na kushuka hajui, mpangaji wa bei za mafuta *ZRB* wakati *ZRB* ni chombo cha kukusanya kodi si cha kupanga bei za mafuta. Haya ni mambo ya Idara ya Nishati kwa sababu haya ni mambo ya kisera. Sasa mimi napata shaka hii idara haipo ipo jina tu haijaanzishwa rasmi au kitu gani.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo vile vile hapa la hawa watu wanaouza mafuta wanatuletea mafuta mabaya, vyombo vyetu vinaharibika. Sasa hivi kuna kesi nyingi ukipita huko ma-gereji kuna matatizo ya vyombo kuharibika

kutokana na mafuta machafu, hebu Mhe. Waziri twambie nani hasa anayeyasimamia mafuta haya kuyapima kuona kiwango chake, ni Idara yako hii ya Nishati. Kama inapima inatumia kigezo gani, mbona humu sisi tunaofumbua macho tunayaona kama mafuta machafu, kwa sababu unapokwenda ushayajaza ukienda kwa fundi gari haipigi vizuri anakwambia mafuta yana maji akimwaga maji yamo, hivo hawa watu wa Idara ya Nishati wako wapi, wanafanya shughuli gani hasa hawa. Huku wananchi wanakula hasara kwa sababu hivi vyombo vyetu tunanunua kwa fedha zetu, lakini idara hii ni chombo cha serikali, kama ndio kazi zake kusimamia mambo hayo basi hakifanyi kazi zake. Sasa kama hakifanyi kazi zake na sisi hatuna haja ya kuiingizia fedha hii maana itakuwa tunaingiza fedha mahala ambapo hapana matumaini. Mhe. Mwenyekiti, malalamiko ya wananchi ni mengi mno juu ya mafuta machafu.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, juu ya watu hawa hawa wa mafuta, watu hawa mimi wananishangaza sana mafuta yakipanda duniani wao hudai wapandishiwe bei, kama hayakupandishwa hawatoi mafuta maana yanakuwa yashapanda yako ghali. Ingawa yale waliyonayo sio waliyonunua kwa bei ile, lakini yakishuka hapo ndipo penye mchezo.

Juzi tu Mhe. Mwenyekiti, na wewe najua gari unayo bila shaka ulipata tatizo hili na gari yako ni ya petroli ninavyoijua, tulikuwa tuna kishindo cha petroli hapa imebanwabanwa kisa imeshushwa bei. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi napata tabu hawa wasimamizi wa hizi sera wako wapi, kwa nini wananchi wanapata tabu kiasi hiki. Mafuta yamo mbabe tu anakaa anasema mimi sitoi halafu tunamuachia tu, ule usimamizi wa serikali uko wapi juu ya watu hawa si wanawapa leseni hawa, kama unawapa leseni hakuna masharti, basi kuna siku watu wataamua tu leo hatutoi mafuta nchi nzima wakakaa na hatuna vya kuwafanya.

Mhe. Waziri hebu utakapokuja tusaidie, nini hasa idara hii kazi zake, na haya ninayoyazungumza kama ni kazi zake wanayatekeleza vipi mbona sisi hatuoni huku. Hili kwetu ni tatizo Mhe. Mwenyekiti linatusumbua sana wananchi wetu wanapata tabu, wanasababishiwa usumbufu pasi na sababu yaani hii tunaweza kusema bure bure, ikipanda lazima wapandishiwe siku ile ile, lakini ikishuka aa, ibaki pale pale mpaka itakapopanda tena. Sasa hili nalo tusaidiwe kidogo lipatiwe ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, nirudi nyuma kidogo kwenye ukurasa wa 25 kwenye Idara ya Upimaji na Ramani. Idara hii inashughulika na mambo ya kupima na kuchora ramani, mambo ya mipaka haya na nini.

Mhe. Mwenyekiti, katika jimbo langu la Mkwajuni pana ugomvi pale wa mpaka baina ya Kijiji cha Potoa na Muwange, ugomvi huu uko wa siku nyingi mno namuomba sana Mhe. Waziri akija anisaidie, lini hasa patapatikana ufumbuzi katika tatizo hili. Kwa sababu inaonekana ndio yale niliyoyasema wakubwa huwa wanafumbiana macho, hutizamana tizamana hawa. Sasa limekuwa tatizo, patatatuka kidogo baada ya muda unarudi tena vile vile maana yake yale masharti inaonekana watu hawayafuati. Sasa hebu Mhe. Waziri utakapokuja naomba unisaidie ni lini hasa utatatua tatizo lilioko pale. Kwa sababu tukiendelea hivi hivi tunapata tabu.

Hivi juzi tu mimi najua Mhe. Waziri wewe ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa katika Chama chetu cha Mapinduzi, mimi kada wako wa Chama cha Mapinduzi, hata uchaguzi wangu wa viongozi katika tawi la Muwange ulikuwa tatizo kwa sababu ya ugomvi huu. Sasa ninapata tatizo mimi mwenzenu na wewe kada wangu Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa tusaidie tuweze kutatua tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakwenda kidogo kidogo wanasema taratiibu sina haraka, niliguse kidogo kwenye ukurasa wa 55 Shirika la Umeme. Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wamechangia hapa kuna matatizo Shirika la Umeme. Mimi nakubaliana nao kweli yapo tena mengi, sitaki nizungumzie mambo ya kamati nataka nizungumzie kwa ujumla.

Kuna suala zima hapa nafikiri Mhe. Omar Ali Shehe alilitaja juu ya suala la kuwa hivi karibuni kulitokea tatizo la ubandishaji wa bei ya umeme ghafla bila ya wananchi kujua, nafikiri hata wao wenyewe Shirika la Umeme watakiri lilileta msongamano mkubwa, ilikuwa tena hata sisi Waheshimiwa usijekwenda kununua umeme, ndio nyie mnatupandishia aa, mimi mwenyewe nimekuja kununua mimi mteja kama nyinyi hapa, nikajiteteatetea lakini bado kidogo nipigwe. Umeme ulipandishwa ghafla sijui kama tatizo hili lishatatuka au vipi, lakini hili lilianza kuanzia tarehe 6 ya mwezi wa saba mpaka juzi lilikuwa bado sijui sasa hivi namuomba Mhe. Waziri atapokuja atakuja kutueleza.

Umeme ulitoka bei ya *unit* shilingi 168 mpaka shilingi 322, ajabu mana kila mmoja tafrani kuna watu pale walishituka aka! Vipi, lakini wale wauzaji wenyewe pale vituoni walikuwa hawana maelezo ya kuwaeleza wateja nini tatizo. Sasa kama mwananchi anakwenda pale na shilingi yake elfu kumi au ishirini anakuta kile kiwango alichokuwa anakipata hakipati anapata robo au nusu ya kile lazima ashituke. Sasa ukiuliza muuzaji naye hajui anachosema umeme umepanda tu, mbona mnapandisha hamtwambii, na hapa nje ndo pana makaratasi wameweka bei ya umeme matumizi yanayozidi *unit* 50 shilingi 168, *unit* moja hadi 50 shilingi 66, wamebandika pale nje lakini ukipiga

hesabu ya ile bei ya *unit* uliyouziwa pale unakuta umeinunua *unit* moja kwa shilingi 322. Mimi nilikuwa namuomba Mhe. Waziri aje atusaidie ufafanuzi katika hili ili wananchi wetu weweze kujua.

Lakini isitoshe kama ni makosa yamefanywa na shirika je, hawa ambao waliuziwa kwa bei hii zile fedha zao zitapatikana vipi. Naomba hapa Mhe. Waziri atapokuja asiwe na haraka, taratibu ili wananchi waweze kumuelewa kwamba fedha zile ambazo zimekosewa zitarejesheka vipi, kwa njia ya kuwarejeshea umeme wao au kuwalipa fidia au utaratibu gani; uje hapa utueleze ili wananchi wetu waweze kupata busara zako na kuelewa nini serikali yao imekosea na inafanya marekebisho kivipi. Hilo nataka Mhe. Waziri utapokuja utusaidie sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika shirika hili hili kuna tatizo pale namuomba sana Mhe. Waziri atusaidie hili kwenye utendaji. Kamati ya Baraza ilikwenda Pemba kufanya kazi zake katika Shirika hili, walikuja viongozi wa shirika tukafanya kazi nao pamoja kule Pemba kwa muda wa wiki moja tukarudi Unguja. Tukachukua na maofisa wengine kutoka Pemba kuja Unguja kufanya nao kazi pamoja, tukafanya nao kazi lakini Unguja nafikiri ikawa wiki mbili au karibu ya tatu hivi. Lakini cha kusikitisha katika kulipwa mafao wamepeana wote, lakini kuna afisa mmoja wakamuacha, kisa aa huyu alikuwa akiisaidia kamati sana kinachoulizwa na kamati yeye anajibu moja kwa moja hakuwa akipindapinda, hilo lilikuwa ndio tatizo. Sasa Mhe. Waziri utusaidie juu ya watendaji wako kwa kadhia kama hizi. Tunaomba sana mimi ningekuomba Mhe. Waziri utapokuja juu ya hili unieleze kwamba yule mtu ameshalipwa haki zake zote, na kama hajalipwa kwa nini yeye halipwi na wale walipwe wakati wote ni wafanyakazi wa shirika.

Hivi si vitendo vizuri kufanywa na watendaji wetu, kisa cha kwamba ameisaidia kamati ndio liwe tatizo kwa mfanyakazi yule. Lakini ningewaomba watendaji wako hawa wakasoma hizi kanuni za Baraza, wangeangalia ile Kinga, Haki na Fursa za Wajumbe wangekwenda kwenye kanuni ile wakaiangalia wakaweza kuona. Kama kutolipwa walikuwa wasilipane wote basi, kwa nini walipane wote abakishwe mmoja. Hili Mhe. Waziri kwa kweli hatukuridhika na afisa yule alishalalamika kwenye kamati yetu ameandika barua kwa Mwenyekiti, lakini Mwenyekiti aliniambia suala hili nije nilizungumze mimi, Mwenyekiti yeye amekaa pembeni anatuma kijana wake, kwa hivyo nakuomba sana Mhe. Waziri utapokuja kutupa maelezo yako unisaidie vizuri, au na mimi kwenye hili basi kule kwenye lile fungu la mapato tena la Shirika la Umeme sitoliacha, nitalikamata mpaka nijue mwisho wa hadithi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nirudi nyuma kidogo kwenye ukurasa wa 31 Idara ya Ujenzi. Idara hii tumesoma kwenye kitabu hapa inaonekana itaendelea na ujenzi wa majengo yake katika maeneo ya Mpapa ambapo hakujakamilika. Lakini mimi niungane na Mhe. Mwenyekiti wangu wa Kamati ya *PAC* juu ya malalamiko yetu, juu ya ujenzi wote wa nyumba hizi kuanzia za Michenzani na Mpapa, kwamba ujenzi wa nyumba hizi haukufuata taratibu ambazo ni sheria za manunuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kitabu hiki *Public Procurement Act and It's Regulation* hiki hakikufuatwa. Sasa hebu tusaidiwe kidogo tatizo ni nini? Wakati leo unatuomba tena fedha tuidhinishe kwa ajili ya ujenzi huu wa kuendeleza majengo ya Mpapa, kama hizi za mwanzo hukuzitumia vizuri unatuomba nyengine tukupe hapa Mhe. Waziri pagumu. Mimi Mhe. Waziri sina wasiwasi na wewe nakufahamu uchapaji wako wa kazi, wasi wasi wangu hawa huku, mimi ninaujua usimamizi wako ni mzuri kweli, utendaji wako wa kazi sina wasiwasi nao, lakini Mhe. Waziri hapa ipo kazi. Sasa sijui utakuja kutwambiaje, maana haya ndo yashapita lakini bado hizi ni fedha za walipa kodi, kama hazikutumika kwa mujibu wa utaratibu maana yake hizo fedha batili, sasa kama fedha iliyotumika batili unaiomba na nyengine tutaitoaje hii nyengine kama ile ya mwanzo haikufuata utaratibu tutaamini vipi sisi. Hapa Mhe. Waziri naomba utapokuja utusaidie maelezo ya kina, namna gani utavyoweza kuzidhibiti fedha hizi ili zifuate ule utaratibu unaotakiwa kisheria.

Mhe. Waziri ili nikubaliane na wewe basi labda uniahidi vizuri kwamba hawa ambao walitumia sivyo hatua ambazo utachukua.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika tano za kumalizia.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakubali Mhe. Mwenyekiti, hata tano nyingi mimi nitatumia labda tatu tu nimalizie ili niwape na wenzangu nafasi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri mimi hili nitalitakia maelezo ya kina kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwenye Idara ya Nyumba ukurasa wa 34 ambako niliacha neno kidogo. Niishukuru sana serikali kwa kuanza kuandaa sheria ya nyumba ya kuanzisha hili Shirika la Nyumba. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo zuri sana, nitalisaidia shirika hili kama litaanzishwa basi litaisaidia sana ili kuweza kupata mapato. Kwa sababu sasa hivi idara hii haikusanyi mapato ipasavyo, ukiangalia hata zile kodi za nyumba inavyokodisha, idara hii mtu yeyote ukimwambia anaweza hata asiamini. Kwa hivyo, kuanzishwa kwa Shirika mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri akaharakisha sana kuileta hii sheria, aiharakishe kuileta tuipitishe hapa ili Shirika hili lianze kazi yake haraka iwezekanavyo.

Nakuomba sana Mhe. Waziri utapokaa huko na watendaji wako mjihimize sana, ikiwezekana hata mwezi wa Oktoba kikao kinachokuja mkaileta sheria hii mimi nakuhakikishia tutakusaidia, tutaijadili na tutaisaidia kuichanganua ili uweze kuanzisha hili Shirika. Kwa sababu utapoanzisha shirika hili basi nahakikisha matatizo mengi sana ambayo kwa sasa hivi yapo juu ya idara hii yatapungua, sisemi yatakwisha lakini imani yangu yatapungua. Kwa hivyo, nakupongeza sana Mhe. Waziri kuwa na mchakato wa kuanzisha sheria hii.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, nimkumbushe sana Mhe. Waziri mimi namjua Waziri wetu huyu hana tatizo msikivu sana, tushamuona katika mambo yake hayo huwa jambo likishakuwa la ukweli hapingipingi, nakuomba sana Mhe. Waziri utakapokuja usiwe na kupingapinga, ruhusu tuunde kamati tuweze kukusaidia katika migogoro ya ardhi na mambo mengine ambayo yamejitokeza. Katika wizara yako kuna mambo mengi Mhe. Waziri basi pengine kuundwa kwa kamati ile kutakusaidia wewe na wizara yako kuweza kuyajua matatizo yaliyokuwepo katika wizara ile.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kunipa nafasi hii, sitounga mkono hoja hii mpaka nitakapopata ufumbuzi wa kutosha juu ya yale ambayo nimeyaeleza. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia na mimi bajeti hii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 kuwasilishwa mbele ya Baraza lako tukufu.

Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Waziri kwa kuleta bajeti yake hii ambayo ina mambo mengi, kutokana na maoni ya kamati basi na mimi niungane na kamati kwa yale mengi ambayo walitoa kama ni ushauri wao. Sekta ya Maji ni sekta muhimu sana na ina matatizo mengi.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 5 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Idara hii inawajibika katika kusimamia na kuratibu kazi zote za kawaida na za maendeleo, na nimeweka hapa miradi ambayo nimeielezea hapa ni miradi ya usambazaji wa maji vijijini. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sijui ni tathmini gani wanayoifanya wenzetu wa Idara hii ya Mipango na Sera na Utafiti, kwa sababu maji bado ni kikwazo katika miji mbali mbali. Maji ni kikwazo na mimi nachukua fursa hii kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani ambao kwa kweli wana changamoto kubwa juu ya upatikanaji wa maji, juu ya kwamba tumejisaidia kwa kuchimba visima maeneo mbali mbali, lakini bado watu wanalalamika kwamba maji si safi na salama. Sasa tunahitaji kwamba maji ambayo yatazalishwa na kupatikana katika visima hivi vya

maeneo mbali mbali ambayo wamekusudia serikali basi tunahitaji tupate maji yale kwa ufanisi.

Kwa kweli mimi niseme kwamba nilie kilio changu kwenye mradi wangu wa SEMUSO, ambao mpaka leo hii maji hatuyapati na sababu ni kwamba mradi ule sasa hivi tunaambiwa tatizo ni umeme. Lakini hata hiyo *water pump* yenyewe ambayo tulifadhiliwa, kwa sababu mradi ule ni wa wananchi pamoja na ufadhili wa Marekani, lakini mpaka leo hii imekuwa ni tatizo na tumejitahidi sisi kama Wawakilishi kwa mradi ule mpaka leo hatukupata mafanikio.

Mimi kinachonipa hofu hasa ile miradi ambayo tumefadhiliwa, ni jambo litakuwa la kushangaza na hata wale wafadhili kwamba baadae haupatikani ule ufanisi wenyewe. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hili ni tatizo na tatizo kubwa. Kwa hivyo, kama idara hii kazi yake ni kutathmini basi ifanye tathmini zilizokuwa na ukweli ndani yake.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende na ukurasa nambari 37 Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe. Mji Mkonge ni hifadhi ambayo imekubalika kimataifa, kwa hivyo mimi nasema tukipata ile misaada mbali mbali basi tujitahidi kwenye Mamlaka hii isimamie vizuri ili isipoteze sifa zile ambazo zimekubalika kimataifa. Kwa kweli zile nyumba zinazobomoka kwa kujengwa kwa matofali inakuwa tumeshapoteza zile sifa za Mji Mkongwe.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije Mafunzo. Kwa kweli mafunzo ni muhimu kama walivyosema Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwamba ni lazima tunapowapeleka wafanyakazi wetu masomoni, wakirudi basi yale maslahi waweze kuyapata ili wawe *active* katika kazi zao na vile vile tutapunguza ule usumbufu wa wafanyakazi kutorejea tena na wakachukuliwa sehemu nyengine.

Vile vile niende kwenye ukusanyaji wa mapato. Kama mapato yatakuwa hayakusanywi ipasavyo hapa itatokea kutowajibika. Kwa sababu kila mtu kwenye nafasi yake ya kazi basi atambue kwamba kuna uwajibikaji na uwazi ndani yake uwepo, hasa tukijua kwamba sote ni wananchi wa nchi hii, kuna mambo mengi ambayo tunayahitaji ya mafanikio na maendeleo ambayo hayapatikani. Wenzetu wanaotoka nje mara nyingi huwa wanatusema kwamba kuna nchi ambazo zilianza mchakato wa maisha katika mambo mbali mbali na wao walikuwa nyuma kuliko sisi, lakini sasa hivi sisi tumeshakuwa nyuma kuliko wao. Tatizo ni nini, ni kwamba hatuna uwajibikaji, uwajibikaji na uwazi na hasa ile misingi ya utawala bora. Ni lazima tuifuate misingi ile kuwa wawazi, kuwa wawajibikaji kila mtu ajue dhamana yake ni nini, lakini

mapato ni mengi baadae yale mapato hayo yanapenya au yanaingia mikononi mwa wajanja wachache.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele niende na mapungufu haya yaliyoonekana kwenye umiliki wa ardhi. Kwa kweli umiliki wa ardhi vile vile kama walivyosema wenzangu kuna matatizo mengi, ni kwamba migogoro hii ya hapa na pale na hasa nikizingatia kwamba yameshazungumzwa mara nyingi na Waheshimiwa wengi ili sasa tuone ni jukumu letu sisi kama viongozi. Mhe. Waziri akija hapa ayafafanue na atueleze kwa uwazi kabisa, ili na sisi tutoshelezeke kama ni viongozi Wawakilishi wa wananchi, inakuwaje hii migogoro na ukizingatia kwamba migogoro hii wanaoanzisha ni viongozi wenyewe.

Kama ilivyosemwa kuwa Masheha, Wakuu wa Wilaya, na viongozi wengine kwamba mtu anajikatia maeneo mengi kwa kujitosheleza yeye, anajisahau kwamba hizi ni mali zetu sote wananchi na ni rasilimali za taifa letu na kwa hivyo sote tugawane kidogo kidogo, kuliko mtu kujibebea peke yake.

Niende kwenye Idara hii ya Mipango Miji. Kwa kweli watu hawa niseme ni watu wenye kufuatilia mambo yao kwa hapa nitawasifu sana. Lakini vile vile nitakuwa na majonzi yangu kwamba ni wafuatiliaji kwamba ni yale ambayo wanayaona wao hayana maslahi kwao. Kuna maeneo ya wazi ambayo yanajengwa kiholela lakini kwa sababu ya ubinafsi, lakini pale inapotaka kujengwa kitu ambacho kwa wao wanakiona hakina maslahi kwao basi ni watu ambao wanakuwa wagumu. Mimi kwa masikitiko sana niseme kwamba tulitoa ahadi na Mbunge wangu kujenga kituo cha Polisi. Lakini walisimama kidete na ninasema wako *active* sana, siku ile ile niliyoanza kujenga tu basi walikuja pale na wakatizama na tukapewa sababu, mimi nitasema ni sababu ambazo si za msingi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kitu ambacho nilikijali zaidi ni kuwepo *cable* ya umeme, lile ndio nililoliona, lakini lile halikuwa tatizo kwa sababu watu wa umeme walisema nyinyi kama mutakwenda mbele huko sisi hatuna tatizo, na kama nyinyi huu waya mutauvuta nyuma basi sisi vile vile hatuna tatizo.

Lakini la kushangaza ni vile kuambiwa kwamba kuna programu toka mwaka 1982 ya kujenga barabara kutoka Makunduchi mpaka mjini, maana yake hiyo njia Mhe Mwenyekiti, inaonekana itapita hewani. Huko nyuma haitoathiri chochote itakuja kuathiri kituo cha Polisi.

Mimi ninamshukuru sana Makamo wa Pili, maana yake alisema kwamba jamani wengi wapo na ilikuwa imeshakubalika lakini kwa mtizamo kwamba wale watendaji, kwa sababu halikuwa na maslahi mbele yao na pale mimi

ninasema bado hatujaridhika, na lolote litakalotokea pale, maana yake hata hawakuthamini zile nguvu ambazo sisi tumezitupa, shilingi milioni tatu, hivi sasa mtu aende aseme mwenyewe tu pale anatembea tu aone tu tatizo lililokuwepo pale ni lipi, la kwamba sisi hatukuruhusiwa kujenga kituo cha Polisi. Kwa hivyo mimi kwanza nijibiwe ni lini hiyo barabara inayotoka Makunduchi mpaka mjini, na kama sikujibiwa na mimi ninakaza buti, mwanamke safari hii na mimi ninakaza buti. (*Makofi*)
Mhe. Mwenyekiti, kama wenzangu walivyosema kwenye Shirika la Umeme …
Mhe. Mwenyekiti (Mhe. Mgeni Hassan Juma): Mheshimiwa una dakika 5 zilizobakia.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, sizimalizi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwenye Shirika la Umeme. Kwenye shirika hili mimi ninahisi kwamba watu waliokuwepo wamefanya mambo mengi. Kusema kweli shirika hili wao wapo kibiashara. Wenzangu asubuhi walisema hapa kwamba serikali ichukue jukumu lile, lakini sio serikali, serikali kama serikali ina wizara yake na kila moja ina majukumu yake na mashirika pia yana majukumu yao.

Ina maana ikiwa kwamba tatizo lile libebe serikali, ina maana shirika lenyewe libebe na lile shirika linakwenda kibiashara. Mimi nimebahatika nimekwenda pale siku moja kununua umeme. Nilifarajika nikapata maelekezo. Unapeleka shilingi yako elfu kumi, lakini uzingatie kwamba wewe siku nyengine ile mita ya TUKUZA hujailipia.

Huko nyuma ambapo mita yako imetolewa una deni. Sasa wewe unapeleka shilingi elfu kumi yako, inabidi madeni yale yote ulipe deni la mita ile, unakatwa na deni lako na nyuma, inayobakia ndio unapewa hizo *units*. Sasa hapo ndio palikuwa na matatizo kidogo ya kuwa anayepeleka shilingi elfu kumi lakini unapata umeme tofauti.

Mimi nilifahamishwa hivyo na mimi nikaridhika. Lakini sasa kama Shirika la Umeme basi wawe wanatoa elimu kwa wananchi. Juu ya kuwa na umeme pia umepanda, walitueleza kwamba kuna *units* ambazo zinaletwa huko Shirika la Umeme TANESCO, bado linakuwa ni jukumu lao wao na siku chungunzima walikuwa wanalidhibiti wao lile deni wanalibeba wao. Lakini bado ikawa ni tatizo na hili niseme kwa upande wao ni lazima wawaeleze wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo nasema ninashukuru sana na nimuambie Mhe. Waziri kwamba wizara yake hii, ni mtu ambaye ninamstahi sana na kumuheshimu sana, maana yake alikuwa ni Waziri wangu siku nyingi ni mtu

wangu wa karibu, kwa hivyo ninasema Mhe. Mwenyekiti, waziri aniambie hili tu moja, ninauliza hili suala la kuhusu ujenzi wa kituo cha Polisi, niambiwe lini ile barabara itakayopita hewani huko ikaja ikatua pale kwenye kituo cha Polisi tu.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa dhati. Nitajitahidi kukidhi huu wakati na kama unavyofahamu sina uchangiaji wa muda mrefu. Nitakwenda kwenye *point direct* ili niweze kumaliza haraka.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niendelee kukushukuru, nimshukuru Mhe. Waziri, mzee wangu, babu yangu, mlezi wangu, maalim wangu, alhaji Maalim Ramadhan. Lakini pia niwashukuru watendaji wake na hususan nimshukuru zaidi Katibu wangu wa Ardhi Ndugu yetu Mwalimu, kiongozi wetu lakini pia akiwa ni mwananchi wangu katika Jimbo la Kwahani, amenilea na kunifunza na leo ninadiriki kuwatetea wananchi wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninakwenda ukurasa wa 15. Hapa nina maombi tu kwa Mhe. Waziri kuhusu Mahakama ya Ardhi. Nimuombe Mhe. Waziri kujitahidi kutoa msisitizo katika eneo hili kwani Mahakama zetu zimekuwa zinaendesha kesi katika hali ya kudhorota sana, na matokeo yake migogoro inakuwa inapandiana siku hadi siku.

Ukiangalia takwimu kesi 188 lakini zilizopata ufumbuzi ni 95, kwa kweli takwimu ni ndogo na hairidhishi kutoa ufumbuzi kwa wananchi katika masuala haya ya migogoro katika chombo hiki cha kutunga sheria.

Nikitoka hapo Mhe. Mwenyekiti, naomba niende ukurawa wa 55 kuhusu Shirika la Umeme. Wengi wamelizungumzia lakini kila Mheshimiwa amelizungumzia kwa namna yake. Mimi hapa tu Mhe. Mwenyekiti, bado nimuomba Mhe. Waziri aangalie kwa kina juu ya eneo hili. Ni eneo ambalo hivi sasa linaleta usumbufu kwa wananchi wetu kutokana na ongezeko kubwa la kupanda kwa umeme katika kipindi kifupi. Sijui tunaangalia vigezo, lakini kama tungekuwa tunaangalia vigezo vya wananchi basi tusingefanya suala hili la kupandisha umeme katika hali hii.

Kwa sababu unapoangalia vigezo vya mwananchi, unatakiwa umuangalie mwananchi wa nchi wa kima cha chini walio wengi wanapata mshahara wa kiasi gani. Ukishaliangalia hilo ndio utapata kupima namna gani basi ya kupandisha kodi za aina nyengine. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, wananchi wa kima cha chini ambao hawatumii umeme kwa nguvu sana wastani wao walikuwa wanatumia umeme wa shilingi ishirini elfu mpaka thalathini elfu.

Lakini baada ya ongezeko watu wametoka shilingi arobaini elfu mpaka sitini elfu, mtu anapokea mshahara wa shilingi laki moja na ishirini elfu. Maisha yake ataendeshaje. Kwa hivyo hili wenzangu wamelizungumza. Huna haja ya kutizama Mhe. Mwenyekiti, na wengi hapa wamesema kwamba mapato yapo mengi. Hebu tukidhi yale mapato, tukusanye zile kodi ambazo watu hawalipi, tudhibiti ule wizi ambao upo pale, tukishadhibiti hayo mimi ninafikiri hata zile huduma za uendeshaji basi zingekuwa zinajifidia na hali inakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo ninakwenda ukurasa wa 13 kuhusu Idara ya Ardhi. Mhe. Mwenyekiti, kuna eneo mbele ya Hoteli ya Bwawani pembeni ya Shirika la Biashara linalouza gari na pikipiki ambalo sasa linauza vyarahani.

Mhe. Mwenyekiti, lile eneo kwa kweli halipo katika hali nzuri. Eneo lile hivi sasa limekuwa kama jaa, eneo la kuweka makontena pasipo mpangilio, watu wanatupa taka bila ya utaratibu. Sasa mimi ninataka kujua tu kwamba lile eneo lipo kwake au halipo, lakini kwa habari za mbali sana, sasa hivi Mhe. Waziri atakapokuja atakuja kunieleza kwamba lile eneo kuna mtu anataka kupewa.

Sasa nilikuwa ninataka kujua tu wanataka kutoa wenyewe Hoteli ya Bwawani au Mhe. Waziri, wizara yake ndio inayotaka kumpa huyo mtu, na kama wanataka kumpa huyo mtu ni mtu gani na kwa malengo gani. Hili atakapokuja Mhe. Waziri atanisaidia.

Lakini hapo hapo Mhe. Mwenyekiti, katika suala la ardhi. Mimi ninataka nije hiyo kadhia ambayo imezungumziwa na Waheshimiwa wengi na mimi ninataka nizungumze maeneo kama mawili tu ambayo kwa kweli haya maeneo yananiumiza kichwa na yananisononesha kwa wananchi ambao wenye maeneo kuchukuliwa maeneo yao.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu ilipokuwa kazini Pemba, tulitembelea eneo la Mtondooni. Lile eneo Mhe. Mwenyekiti, wakati tunapita na gari zetu pale kamati wananchi walitusimamisha wakalia sana, wakatusikitikia sana juu ya eneo lao kuchukuliwa na kiongozi wa serikali. Ndio maana tukasema haya maeneo au haya matatizo basi tusiiwachie wizara hayapati ufumbuzi, kwa sababu waliochukua wengine ni viongozi wa nchi. Mtu hawezi akajihukumu yeye mwenyewe hata siku. Ndio tukafikia pahala lazima tume ziundwe kwenda kuchunguza hii kadhia ili kuwanusuru watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, lile eneo kiongozi aliyechukua, tume itakapokwenda itamtambua sina haja ya kumtaja hapa. Yeye amemsingizia kiongozi wa nchi

kwamba ndiye anayelihitaji, lakini hatimaye baada ya kukamilisha na kuwachukua wananchi kwa nguvu kubwa, ile minazi ya eneo lote basi kaiandika jina lake. Sasa tume itakapoundwa na nina imani safari hii tume ipo katika suala hili itakwenda kuona hiyo kadhia na tuwasaidie wananchi wa Mtondooni Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, katika kadhia hiyo hiyo ya ardhi. Hapa kidogo ningetoa maelezo ya kuchekesha. Sisi Wazanzibari tulikuwa tukisikia Mhe. Mwenyekiti, labda mkorogo wanatia watu, kumbe mkorogo hivi sasa upo serikalini. Mhe. Mwenyekiti, nikizungumza mkorogo kutia watu kwa sababu hivi sasa imekuwa ni *fashion*. Unamkuta mwanamama mguu ni mswahili, mikono mwarabu, nywele muhindi. (*Makofi*).

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mkorogo huu umeingia katika taasisi za serikali unatushtua na hatufiki kwa hali hii, kwa sababu niseme hivyo. Pale Maruhubi pana eneo. Sasa sababu ya kusema hivyo Mhe. Mwenyekiti, unakuta mtu kapewa *lease* lakini matokeo *lease* kafutiwa, lakini baada ya kufutiwa yeye anajenga, na huku *lease* kapewa mtu mwengine. Sasa huu ndio mkorogo, *lease* kapewa kafutiwa na anajenga na aliyepewa mwengine hana uwezo wa kujenga. Sasa imekuwa ni tatizo. Eneo moja unakuta linaingiliwa na watu wawili. Huyu kachukua mguu, huyu kachukua kichwa muhindi.
Mhe. Mwenyekiti, hii ni hatari na kwa kweli hatufiki na hatutopata ufumbuzi. Mfumbuzi wa masuala haya kumuomba Alhaji Mhe. Waziri wetu katika hili, ninajua hapa watoto wa mjini wanasema *anabeba gunia la misumari* tunataka kumtua kwa maslahi ya wananchi wetu Mhe. Mwenyekiti. Tuunde kamati teule tukaondoshe matatizo haya.

Hapa Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaungana na wenzangu hakieleweki kabisa na hatuelewani kwa sababu matatizo yamekuwa mengi, kero ni nyingi, imekuwa mnyonge hana haki. Tufute ile hali halisi ambayo tunazungumzia kwamba *mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni.*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kama nilivyozungumza huwa sipendi sana kuchukua muda mrefu, ninapenda nimalizie katika kilio cha watu wengi. Mimi sitolia kama yule Mbunge aliyefika kulia machozi kumbe alitakiwa aliye kwa kutoa *points* za msingi kwenye Bunge ili hoja zake ziwe za msingi na kufanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, ni sikitiko katika masuala mazima ya maji. Mamlaka tunaionea huruma. Tunashindwa kufahamu. Mwenyekiti wangu hapa alisema labda lipelekwe jeshi. Sijui na mimi ninafikiri labda Mhe. Waziri atakapokuja atatujibu masuala ya msingi sana katika hoja zetu.

Mhe. Mwenyekiti, bado tunapata kigugumizi. Serikali Mhe. Mwenyekiti, ilitutamkia viongozi mbali mbali na katika majukwaa mbali mbali kwamba mradi wa JICA utakapomalizika tatizo la maji katika Mkoa wa Mjini/Maghiribi litapungua kwa kasi. Hii tathmini hatuioni. Kwa sababu na mimi jimbo langu lipo katika Mkoa wa Mjini/Magharibi lakini sijaona badiliko lolote katika mradi huu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri aje atueleze ni tatizo gani kwenye mradi ule. Ukija visingizio kibao, kila mtu analeta visingizio. Ukija kwa *engineer* anakwambia hili, akija kwa fundi msaidizi anakwambia hili, yaani kauli zinatofautiana.

Mhe. Mwenyekiti, mwenzangu amelizungumza suala la SEMUSO. Hapa babu Mhe. Alhaji Mhe. Waziri Maalim Rama ninataka nimpe hadithi moja tu. Mhe. Waziri hili eneo linachekesha bwana. Siku inayotangaziwa kwamba kesho kutakuwa na mkutano wa chama cha siasa katika eneo lile, iwe Chama cha Mapinduzi au CUF basi tangi lile linajaa na maji yanatoka. Sasa tunajiuliza tatizo ni kitu gani. Tatizo ni miundo mbinu au tatizo ni watendaji.

Mhe. Mwenyekiti, na hili kama tunataka kufanya ubishi ingetangaziwa tu kwamba kesho Mhe. Shein anahutubia pale Kibanda Maiti, halafu nije nikuchukue huko nyumbani Fuoni, nije nikwambie ulione tangi la SEMUSO linavyomwagika maji. Wanajaza na tumeshafanya utafiti wa kutosha, tumefika Mamlaka ya Maji mpaka tumechoka. Tukasema tutaanza kufuata *line* kutoka Welezo mpaka chini, lakini ukipanga na wafanyakazi wanaingia mitini, hakieleweki.

Mhe. Mwenyekiti, tangi linalosababisha leo tupate maelekezo, fedha nyingi za wahisani zimepotea, tusije tukafika pahala wahisani wakaanza kurudi nyuma kwa kutoa fedha zao kwa miradi ambayo haitekelezeki. Mhe. Mwenyekiti, safari hii Mwenyekiti wangu alisema pale tunakwenda *with evidence*, tuna *documents*, watundu, wenyewe watendaji wanabishana Mhe. Mwenyekiti, wenyewe kwa wenyewe wanabishana. Huyu anashituka na tatizo hili akenda kwa mkubwa anakwambia mimi ninashituka na tatizo hili, *documents* zinaeleza mpaka maneno ambayo hayaeleweki.

Mhe. Mwenyekiti, mtafiti anakwambia anashangazwa na kuungwa kwa mashine Unguja, uungwaji wake hata mtoto mdogo hawezi akafanya kazi hiyo. Sasa hii hali inatisha. Ili kupata ufumbuzi Babu yangu ninamuamini kaipata hii wizara muda mdogo lakini jitihada tunazijua, jitahidi zake tunaziona, mimi sina wasi wasi na Maalim Ramadhani ninafahamu tu kwamba mabadiliko yatakuwa, isipokuwa tunampa zile *hints* ili aone ile hali halisi apate pale pa kuanzia katika kupata ufumbuzi wa masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kuna kitu nimekisahau kwenye ardhi. Hicho ndicho kitu ambacho ninachotaka kumalizia, meza nimeshaweka safi usiwe na wasi wasi, dakika bado ninazo.

Kuna suala la ujenzi holela ambalo Mhe. Jussa lilimsikitisha katika maeneo ya Mji Mkongwe kwamba watu wenye uwezo nchi hii wanaifanya wanavyotaka. Pasipostahiki kujengwa mtu ndio anakwenda kujenga. Hapa ninamuomba Alhaji sana kidogo yeye na yeye ageuke kidogo kama alivyogeuka jana alivyotusomea ile *speech* yake, hakuvaa kofia, alivaa suti nzuri tu. Sasa na hapa abadilike igeuke kwa kusimamia sheria za nchi hii. Tuangalie mifano ya nchi za wenzetu Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Hamza Hassan Juma kamtolea mfano wa Mizengo Pinda, mimi ninamtolea mfano mama yetu Anna Tibaijuka, kapiga doza nyumba ambazo zimejengwa katika maeneo ambayo hayastahiki. Sisi tunaona taabu ya nini. Watu wanajenga mpaka kwenye vianzio vya maji halafu tunakaa tunalalamika tu, mbona Wazanzibari tumekuwa walalamikaji bila ya vitendo, tubadilike.

Mtu amejenga pasipohusika piga doza, tuwe nchi safi, watu waende kwa mujibu wa sheria Mhe. Mswenyekiti. Ndio yale Mwenyekiti wangu anapofika pahali akasema bora sheria zote tuzichome moto twende hivi hivi kila mtu atoe maamuzi yake basi, lakini tutafika wapi na kwa sababu nchi inaongozwa kwa mujibu wa sheria. Tunaomba sheria zisimamie Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Baada ya hayo na mimi siungi mkono hoja mpaka nipate maelezo ya SEMUSO naomba kukaa. (*Makofi*).

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuzungumza machache katika kuchangia kwenye bajeti yetu hii ya Wizara ya Maji.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze na kitabu chetu hiki cha Tume ya Mipango Afisi ya Fedha, Uchumi na Maendeleo ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu, “Sekta ya maji. Sekta hii ina lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wote watafaidika na huduma ya maji katika maeneo ya karibu, bila ya sekta hii ni kuimarisha miundombinu na huduma za maji kwa wananchi na watumiaji wengine. Vile vile sekta hii inatekeleza lengo la Mkuza 11 la kuimarisha ufikiaji wa huduma ya maji na miundombinu imara ya michirizi ikiwa ni shabaha ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa asilimia 60 mwaka 2010 hadi asilimia 75 mwaka 2015 kwa

maeneo ya vijijini, na kwa maeneo ya mijini kutoka asilimia 80 mwaka 2010 hadi asilimia 95 mwaka 2015".

Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia kitabu hiki cha bajeti kilichokuwa kimewasilishwa hapa Mhe. Waziri siku ya leo. Lakini naona eneo la maji halikwenda *deep* zaidi kwa ajili ya kutatua tatizo tulilonalo la maji, mimi ninasema kwa mji wa Zanzibar hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo tulilonalo la maji katika Mkoa wa Mjini/Magharibi bado ni kubwa sana. Wenzangu walionitangulia walikwisha kuchangia katika sekta hii. Lakini kusema kweli katika maeneo ya mjini hususan ndani ya Jimbo la Kikwajuni Mhe. Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa sana la maji kwa wakaazi wa jimbo hili.

Sasa sijui Mhe. Waziri atakapokuja hapa atatuelekeza nini juu ya kuondoa kadhia hii ya maji katika eneo la Jimbo letu la Kikwajuni hususan ukitilia maanani kwamba programu hii kila inapokwenda mbele kutokana na mapungufu ya fedha yanavyokuja ina maana kwamba hii programu inafikia mwisho hivi sasa kuwa hili zoezi linakaribia kukamilika.

Lakini la maji bado lipo pale pale. Tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa aje atuelekeze hasa nini tatizo letu baada ya mipango yote ya serikali pamoja na wataalamu kwisha kukamilisha juu ya upatikanaji wa maji safi na salama.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mara nyingi hukaa ninajiuliza, ninapoona takwimu zinazokuja hapa kuambiwa kwamba tatizo la maji kwa Mkoa wa Mjini/Magharibi tumelitatua kwa asilimia 80, mpaka kufikia mwaka 2015 tutakwenda kwenye asilimia 95. Asilimia hizi zinazozungumzwa ningelipenda Mhe. Waziri atakapokuja hapa aje atufahamishe ni asilimia ya kuwa na mifereji ya kuwa na bomba zile za kupelekea maji au ni asilimia za watu kukosa maji.

Kwa sababu tatizo la maji ni kubwa sana na hivi sasa imekuwa ni sare, Wazanzibari hususan katika Jimbo la Kikwajuni kutembea na mageloni yanayotiwa mafuta, sasa ndio yanayotiwa maji kama ndio *handbags* zetu za kutembea katika maeneo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa vile vile aje atupe uhakika wa uwezo wa upatikanaji wa kisima kile ambacho ilikuwa tumemuomba awasadie wananchi wa Jimbo la Kikwajuni katika Wadi wa Miembeni Shehia ya Kilimani.

Vile vile tulikuwa tunaomba Mhe. Waziri aje atupe ufafanuzi wake hapa, kwa sababu katika maelekezo yaliyokuwa yametoka humu, namna ambavyo kuna maeneo yalikuwa yametajika katika suala la kupatiwa huduma ya maji, eneo la Jimbo la Kikwajuni sijaliona humu. Pamoja na harakati zote ambazo zilikuwa zinaendelea kwa upande wetu.

Kwa hivyo atakapokuja Mhe. Waziri hapa atusaidie kutuelezea kwa kina namna gani wananchi wa Jimbo la Kikwajuni wataweza kunusurika na kadhia na matatizo ya maji yaliyokuwepo katika eneo lile, hususan ukitilia maanani katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

Nikiondoka hapo Mhe. Mwenyekiti, nakuja katika kifungu cha 74 cha kitabu chetu hiki cha leo. Naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hicho kuna matengenezo za nyumba za serikali. "Mhe. Spika, matengenezo madogo madogo yanaendelea kufanyika katika nyumba za maendeleo za Michenzani, Mombasa na Kikwajuni kwa Unguja na Mkoani, Wete na Chake-Chake kwa Pemba".

Mhe. Mwenyekiti, mimi ndiye Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni. Maeneo ambayo yana nyumba hizi za maendeleo ni Michenzani, Kikwajuni yenyewe pamoja na Kilimani, sijawahi kuona matengenezo ya nyumba katika nyumba za maendeleo katika mwaka uliopita wa fedha. Kwa hivyo Mhe. Waziri atakapokuja hapa aje atuelekeze ni nyumba zipi zilifanyiwa ukarabati katika mwaka huu tunaokabiliana nao.

Tukiondoka hapo Mhe. Mwenyekiti, ninakuja katika *paragraph* ya 75. Hapo Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la kamati ya kuwatambua wanaodai kupewa nyumba na Marehemu Mzee Karume. Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa nilipo nina orodha. Nina orodha mbili hapa.

Moja ina wananchi 31 hawa wanatoka Michenzani ambao walipewa nyumba na Mhe. Marehemu Mzee Abeid Karume, na ikiwa bado wanasubiri kupewa hati miliki za nyumba zile na mpaka leo hii bado hawajapata hati miliki za nyumba zile. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa aje atusaidie kutuelekeza sababu zipi zilizosababisha mpaka leo watu hawa pamoja na harakati kubwa sana ambazo zimefanyika kutokana na Rais aliyemaliza muda Mhe. Amani Abeid Karume katika awamu yake ya sita kuelekeza, kufahamisha na kutoa maelekezo, kwamba watu hawa wapewe nyaraka katika nyumba zao ambazo wamepewa na Marehemu Mzee Abeid Karume.

Lakini kama hiyo haitoshi Mhe. Mwenyekiti, pia nina waraka wa watu 36 kutoka katika nyumba za maendeleo za Kikwajuni. Nao pia wana matatizo hayo hayo ambayo tumeyazungumza hapa. Kwa hivyo atakapokuja Mhe.

Waziri hapa naomba anisaidie katika maelekezo hayo mawili ambayo nimemfahamisha juu ya wananchi ambao wanataka kupewa hati za nyumba zao wanaendelea kuishi hadi hivi leo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo sasa nitakuja katika kadhia nyengine ya mwananchi katika jimbo langu ambaye anaitwa Claudia Claudi Pesa. Mwananchi huyu Mhe. Mwenyekiti, yumo katika orodha ya watu ambao walipaswa kulipwa nyumba. Kwa bahati nzuri na mbaya Mhe. Mwenyekiti, mtu huyu alikuwa anadai nyumba tatu kutokana na familia zao na yeye alikuwa kama msimamizi.

Nyumba mbili wamelipwa lakini nyumba ya tatu haijalipwa hali ya kwamba katika orodha ya kulipwa nyumba yumo, katika vikao vilivyoidhinishwa ameidhinishiwa lakini hadi leo hii nyumba hii hajakabidhiwa, na bado katika familia hizi tatu zingali zinahangaika kwa ajili ya kupata eneo la fidia kwa nyumba yao ambayo imebakia katika serikali. Kwa hivyo Mhe. Waziri atakapokuja hapa aje anielekeze juu ya suala hili vile vile.

Eneo jengine ambalo Mhe. Mwenyekiti, ninataka kulizungumzia kwa masikitiko makubwa sana. Mhe. Mwenyekiti, ni suala zima la kadhia ya mzee wetu, muasisi wetu, mwenzetu na kwa mimi nasema ni mwananchi wa Jimbo la Kikwajuni.
Mhe. Mwenyekiti, kidogo naanza na historia. Zamani tulipokuwa *youth league*, kulikuwa kuna picha moja kubwa sana limewekwa unapotembea katika nyumba za serikali. Lakini picha hiyo nilifanikiwa kuiona katika Jimbo langu la Kikwajuni pia. Mzee Karume amevaa nguo za *youth league* amekamata kifimbo na kofia yake na amenyoosha kidogo. Katika picha ile Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa kuna maneno yameandikwa. "*kilichokufa na kuzikwa ni kiwiliwili, lakini hekima na busara bado zipo na zitaendelezwa.*

Mhe. Mwenyekiti, hayo ni maneno yaliyokuwa yameandikwa katika ile picha kubwa na ni maneno ya hekima kabisa. Sisi tunavyomtambua Mzee Karume, alikuwa ni jemedari wetu wa Mapinduzi yetu matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964. Mhe. Karume yeye alikuwa ni jemedari, lakini tutakapomtaja Mzee Karume ni lazima tutakuwa tunawataja na wale wafuasi wake 14 ambao walijitolea muhanga katika kutekeleza na kuleta Mapinduzi matukufu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kinachonihuzunisha Mhe. Mwenyekiti, ni kuona kwamba ikiwa mwenzetu, mwanamapinduzi huyu na muasisi huyu anafika pahala akaweza kufanyiwa vitendo ambavyo vinahuzunisha, mimi ninasikitika sana Mhe. Mwenyekiti. Ninachotaka kuzungumzia hapa ni suala zima la kadhia ya ndugu yetu, mzee wetu, Mzee Saidi Iddi Bavuai na shamba lake la Buyu.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nilipo nina nyaraka, nategemea kwamba zinatosha kabisa. Nyaraka hizi zimepita katika maeneo matakatifu sana kwa upande wangu mimi, na kwa kweli imenihuzunisha sana. Hata leo mchana watu hawa walikuwepo ofisini kwangu, wamekuja na vilio na masikitiko. Kwa kweli ni jambo ambalo linasikitisha sana. Hapa nina barua ambayo iliwahi kwenda kwa Mhe. Waziri Kiongozi na pembeni yake nina barua nyengine ambayo ilipelekwa katika Tume ya Baraza la Wawakilishi, juu ya suala zima la kadhia ya shamba la mzee wetu, Mzee Saidi Iddi Bavuai.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema, ikiwa tumefika pahala sasa tukaona kwamba mzee wetu huyu kwa vile amekwisha kwenda mbele ya haki, ikawa na mambo yake ambayo alikuwa ameyafanya hatuyaoni tena umuhimu wake, hii ni hatari. Lakini kama hiyo haitoshi kuna vyombo vizito ambavyo vilichukua hatua katika suala hili, na kufikia maamuzi kwamba hili lirejeshwe katika mikono ya familia ya marehemu Saidi Iddi Bavuai. Lakini cha kusikitisha hadi leo hii shamba hili bado hawajarejeshewa wenyewe.

Ninachokiomba Mhe. Mwenyekiti, atakapokuja Mhe. Waziri hapa atuelezee, nini kinachoendelea juu ya kadhia ya shamba hili la marehemu Saidi Iddi Bavuai na familia yake kwa ujumla. Baada ya maelekezo hayo Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika suala zima la mgogoro wa ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu waliotangulia wameshazungumza mengi katika suala la ardhi. Lakini hapa nilikuwa nina angalizo kwa Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, sisi Wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi tuliokuwemo humu ndani tuna imani sana na wewe, tunakuheshimu sana, lakini Mhe. Waziri tunaomba suala la ardhi katika wizara yako uende ukalishughulikie na ukalisimamie kwa kidete kabisa, na ukalisimamie pasi na kumuonea haya mtendaji yeyote, ili uweze kurejesha imani za Wazanzibari ambao wameweza kupata kadhia na matatizo ya namna moja au nyengine katika suala zima la ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, ninavyofahamu mimi, sababu moja wapo kati ya sababu za kufanya mapinduzi matukufu ya mwaka 1964 moja ilikuwa ilikuwa ni ardhi. Kwa msingi huo nitaomba sana Mhe. Mwenyekiti, atakapokuja hapa Mhe. Waziri atuahidi na achukue dhamana ya kulishughulikia suala la ardhi ndani ya Zanzibar hii, ili imani za wananchi wetu ziweze kurejea na vile vile waweze kuyatunza na kuyaenzi Mapinduzi ya mwaka 1964.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa heshima na taadhima na kwa unyenyekevu mkubwa mno, nitaunga mkono bajeti ya wizara hii endapo nitafafanuliwa, nitaelekezwa na nitapewa ufafanuzi utakaonitosha

kutokana na maelekezo ambayo nimewasilisha hapa. Baada ya maelekezo hayo Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia na mimi fursa hii nikaweza kuchangia katika hotuba hii. Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza sina budi kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ametujaalia uhai tukaweza kukutana hapa jioni hii.

Lakini pia nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia hii nafasi. Pia nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa juhudi kubwa ambazo wanazichukua.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka nianze katika ukurasa wa 8 kwenye Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Mhe. Mwenyekiti, katika idara hii tumeelezwa kwamba kuna wafanyakazi 66 ambao wameajiriwa. Mimi tu nilikuwa nataka kujua hapa kama vigezo muhimu ambavyo vinatakiwa kwa wafanyakazi hawa vimetumika, lakini pia ni wafanyakazi wangapi wanawake ambao wameajiriwa na wanaume ni wangapi. Pia kuna ambao wamekufa. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kujua kama hao wameshaondolewa katika orodha hii ya watumishi, ili kuepusha ule uchakachuaji wa kulipa wafanyakazi hewa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu, nije katika Idara ya Ardhi na Usajili. Mhe. Mwenyekiti, katika idara hii niseme ina jukumu kubwa la kuhakikisha hati zote zinazosajiliwa zinawekewe kumbukumbu nzuri, ili kuona idara inaepusha migogoro isiyo ya lazima. Madhumuni ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, kuna watu ambao wamepewa hati na wamesajiliwa vizuri tu pale, lakini matokeo yake ardhi yao imeweza kupewa mtu mwengine na wao kubakia na hati tu zile mikononi. Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri kuliangalia kwa kina tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende kwenye ukurasa wa 15 kwenye Mahakama ya Ardhi. Mhe. Mwenyekiti, kwenye mahakama hii naomba ninukuu kifungu cha 8 ambacho kinasema, kufanya tathmini na ugawaji wa ardhi kwa shughuli mbali mbali, kikiwemo kilimo, makaazi na biashara ili kukuza kipato cha wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka kulisema hili na nimuombe sana Mhe. Waziri, kuwapatia hasa wanawake na wao ardhi wana haki kisheria sawa na wanaume kuweza kumiliki ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme wenzetu wanaume wengi wamebahatika kupata ardhi na hatimaye wanaziuza, kwa kuhadaika na pesa nyingi tu na hatimaye

wanashindwa kutambua kama wao wana watu ambao wanawategemea, ni watoto ambao wanaweza kuja kuwarithisha mali hiyo wakaweza kutumia baadae.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe tu Mhe. Waziri atuangalie sana wanawake kutupatia na sisi ardhi kwa kuona tunaweza kuitumia vizuri katika kilimo na majenzi. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri pia kwa kupitia hii ardhi basi aweze kuwashauri sana, kwa sababu ardhi ni mali ya serikali, na imeamua serikali kutupa sisi wananchi wake kwa kutaka tuitumie ardhi ili tupate mafanikio.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri basi kuweza kutuelimisha sisi wananchi juu ya matumizi bora ya ardhi yetu ile na tuachane tu na tamaa ya kuuza uza ovyo, hatimaye inapelekea sasa hivi ardhi imebaki kidogo, imekuwa sasa tunagombana wenyewe kwa wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atuelimishe kama hivi sasa tunavyoona ardhi nyingi imebebwa na wawekezaji, hali ambayo serikali ingechukua jukumu la kuwaelimisha wananchi, basi wangeweza kuwekeza katika ardhi ile kwa njia ya ubia, hali ambayo ardhi ingebaki kuwa mikononi mwao na wakaweza kujipatia kipato siku hadi siku. Lakini leo ardhi imeuzwa, maana yake tena umeuza ndio umeshauza huna chako unabaki kupita pale unaangalia tu mali ile sio yako tena. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika hii Mahakama ya Ardhi, kuna maafisa ambao pale hawapati posho zao vizuri, wanachelewa kupata posho, inawezekana ikawa miezi miwili au mitatu hawajapata. Kwa hivyo, nakuomba sana Mhe. Waziri uweze kuwapatia posho hilo kwa sababu liweze na wao kuwasaidia kwa mahitajio yao mbalimbali, au ikiwezekana pia kufunga nao mkataba wakaweza kulipwa pesa zao hizo kimkataba.

Vile vile katika suala zima la mahakama niseme pale katika Wilaya ya Kaskazini ‘A’ Gamba, ipo Mahakama ya Ardhi. Mimi nataka kujua kwa nini mpaka sasa hivi ikawa mahakama ile imeshindwa haijafunguliwa mpaka leo, ili ikaweza kuwapunguzia usumbufu wananchi wanaoishi katika eneo lile, inapotokea migogoro ya ardhi katika wilaya yao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba na mimi niende katika ukurasa wa 43 kwenye usambazaji wa maji vijijini. Mhe. Mwenyekiti, hapa pia nimuombe Mhe. Waziri, maelezo tuliyoyapata katika kitabu hiki katika ukurasa huu ni mazuri sana na yanatia moyo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aweze kusimamia utekelezaji wake ili tuweze kupata mafaniko mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, akiacha Mhe. Waziri kuyatekeleza hayo basi aelewe kama wanawake wa vijijini wanapata dhiki kubwa sana na wanapoteza muda mwingi sana kwa ajili ya kufuatilia maji wao na watoto wao. Kwa hivyo, kuwapatia maji wanawake wa vijijini basi kunaweza kuwafanya wanawake hao kupata muda mzuri wa kuwashughulikia watoto wao kwa ajili ya kwenda skuli, lakini pia na wao inaweza kuwapatia muda wa ziada wakaweza kushiriki katika hali ya uchumi na maendeleo kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, wanawake wanapoteza muda mwingi na ndio maana ukaona maendeleo ya elimu katika vijiji yanakosekana, kwa sababu muda mwingi unapotea katika shughuli kama hizo, wakati wenzetu huku wanapoteza muda wanakesha kwa ajili ya kusoma, lakini kule vijijini watu wanakesha kwa ajili ya kutafuta maji.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende kwenye ukurasa wa 34 kwenye Idara hii ya Nyumba, Maendeleo na Makaazi. Mhe. Mwenyekiti, hapa wenzangu wamesema sana na mimi naomba niendelee kusema kidogo. Kwanza nianze na kumpongeza Mhe. Hayati Abeid Aman Karume, kwa kutaka wananchi wake waweze kuishi katika makaazi bora.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abeid Aman Karume alikuwa na mtazamo wa mbali, tukiangalia jinsi nyumba zile alivyoweza kuzijenga kwa kila sehemu zikaweza kufika, nyumba hizi za maendeleo ni jambo la kumpongeza na la kuthaminiwa sana. Kama ingekuwa nyumba zile hazikujengwa kwa sasa sijui tungekuwa tumeshafika mpaka wapi kwa ajili ya kujenga tu. Lakini tuelewe kwamba nyumba zile zimebeba wananchi wengi ambao wanaweza kuishi pale. kwa hivyo, mimi naomba sana Mhe. Waziri tuweze kuziendeleza nyumba zile ili wananchi wetu waweze kupata makaazi bora kama ilivyokusudiwa hapo mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, serikali iangalie sana juu ya nyumba zile, kwa sababu serikali imewacha kuwapitia wapangaji wake kwa muda mrefu, bila ya kujua nyumba anayo nani na kampangisha nani. Lakini hata uangalizi wa nyumba zile ambapo zinaonekana ziko katika mazingira yasiyoridhisha. Mhe. Mwenyekiti, zile ni nyumba za serikali na zinafaa watu wengi, ni lazima tuzidumishe na tuzitunze.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile serikali iendelee kutujengea nyumba zile na iweze kutukopesha wananchi kwa mikopo nafuu. Niseme zile nyumba zenyewe zinapojengwa, kwa sababu

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Bi Panya malizia. Kuna muda mchache umebakia malizia.

Mhe. Panya Ali Abdalla: *Inshaallah.* Kwa kuwa zile nyumba zinaweza kuchukua familia kubwa kabisa kwa sehemu ndogo, ningependekeza sana Mhe. Waziri kuziendeleza nyumba zile kuzijenga kwa kutegemea sasa ardhi yetu imekuwa ndogo, kwa hivyo tungeweza ku-*save* pale kuwajengea wananchi wetu nyumba, ili wakapata pahala pa kukaa na ardhi iliyobaki tukaweza kutumia kwa matumizi mengine, hili ni jambo muhimu sana Mhe. Waziri ulitilie maanani.

Pia Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukupongeza na kukutakia kila la kheri pamoja na kupata wizara hii. Naamini kabisa kwa Waziri tuliyempata kwa utendaji wake bora, basi naamini tunaweza tukafikia katika hali nzuri ya kuweza kutatuka na migogoro hii ya ardhi. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nina tangazo dogo sana, lakini kubwa kwetu, kwa sababu limewahusu vijana wetu ambao wamekwenda Burundi kushiriki katika mashindano ya vijana wa umri wa chini ya miaka 20. Kwa hivyo, tunaambiwa kwamba kwa jumla vijana hawa wamepata magoli 7 na wamefanikiwa kuingia katika robo fainali. Tuwapongeze sana vijana wetu. *(Makofi).*

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo nachukua fursa hii kuwashukuru kwa mashirikiano mema. Ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe, wale ambao wameleta majina yao, kwa sababu bado tuna majina karibu 14 ya Wajumbe wa kuchangia kesho. Kwa hivyo, ningewaomba Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi, Mhe. Suleiman Hemed Khamis na Mhe. Nassor Salim Ali, kesho tukijaaliwa wafike mapema kwa ajili ya kuanza kuchangia.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo tunaakhirisha Baraza letu mpaka kesho saa 3:00 za asubuhi. Ahsanteni sana.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 13/07/2012 saa 3:00 asubuhi)